ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili – Tarehe 17 Juni, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kwenda kwenye swali, kuna taarifa moja nzuri sana. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwapeni taarifa kwamba katika mashindano ya kombe la mabenki ambapo jana timu yetu madhubuti ya Bazara la Wawakilishi, ilipata nafasi ya kucheza na timu hafifu ya ZRB na matokeo ni kwamba timu madhubuti kabisa ya Baraza la Wawakilishi ilipata magoli matatu, kwa kuishinda timu ya ZRB iliyopata magoli mawili. *(Makofi).*

Wachezaji wetu mahiri wa timu yetu ya Baraza la Wawakilishi ni Mhe. Ussi Jecha Simai ambaye amefunga magoli mawili kwa timu hiyo ZRB, akisaidiwa na mtendaji wetu mahiri vile vile Hassan Shahiri yeye amefunga goli moja. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati timu yetu hiyo mahiri kwa ushindi huo mkubwa. tunategemea mechi ijayo ya siku ya Jumatano tarehe 19/06/2013 ambapo timu yetu itaingia uwanjani hapo Mao kucheza na timu ya SUZA. Mategemeo tunategemea yatakuwa mazuri. Mkiona kimya sijatangaza basi mjue mambo sio mazuri. Mambo yakiwa sio mazuri pia taarifa nakuwa siletewi hapa.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wachezaji wetu kwa mchezo huo mzuri ambao tumechukua ushindi. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 55

Kuhusu Uteuzi wa Viongozi Wakuu wa Taasisi za Muungano

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya swali langu nambari 55 kujibiwa naomba uniruhusu kwa muda mchache kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kutoa pole kwa Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na familia yake kwa kufiliwa na kaka yake Marehemu Mzee Ismail Sharif Hamad inshaallah Mwenyezi Mungu ailaze roho yake pahala pema peponi amina. Pia naiomba familia iwe na uvumilivu katika kipindi chote hiki cha msiba.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Yussuf Salim Mbunge mteule wa Jimbo la Chambani, kwa kuweza kushinda kwa kura nyingi katika uchaguzi uliofanyika jana. Vile vile nawapa pongezi ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi kwa kushika nafasi ya pili.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana, naomba swali langu nambari 55 sasa lijibiwe.

Bunge la Jamhuri ya Muungano linajumuisha pande zote mbili za Tanzania kwa maana ya Tanzania Bara na Zanzibar, na kwa kuwa pande zote mbili zinaingiza Wabunge wake kwa mujibu wa majimbo na nafasi nyengine zilizotamkwa kikatiba. Kwa kuwa Waziri Mkuu hutoka miongoni mwa Wabunge na ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(a) Je, uteuzi wa Waziri Mkuu unaofanywa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huangalia vigezo gani ukitilia maanani kuwa utendaji wake ni wa pande zote mbili za Muungano.

(b) Tangu kuasisiwa Muungano huu Zanzibar imetoa Mawaziri Wakuu wangapi.

(c) Kwa kuwa Bunge hili linaongozwa na Spika akisaidiwa na Naibu Spika, Je, Zanzibar imetoa viongozi hawa mara ngapi na Tanzania Bara mara ngapi

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, na mimi kabla sijajibu swali naomba nitoe salamu za pole na kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kufiliwa na kaka yake mkubwa bwana Ismail Sharif Hamad. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

Aidha, Mhe. Spika, napenda pia nipokee pongezi kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa mshindi wa pili katika uchaguzi wa Jimbo la Chambani hasa kwa uongozi wa asilimia katika uchaguzi ule.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 55 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ambayo hadi sasa ndiyo inayotuongoza haikueleza vigezo vya uteuzi wa Waziri Mkuu bali imetoa mamlaka ya uteuzi wa Waziri Mkuu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

b) Mhe. Spika, tangu kuasisiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar imetoa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara moja ambaye ni Mhe. Dk. Salim Ahmed Salim.

c) Mhe. Spika, tangu kuanzishwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar haijawahi kutoa Spika wala Naibu Spika isipokuwa imewahi kutoa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mhe. Salvester Kabumbu, Mhe. Zubeir Ali Maulid na Mhe. Mohammed Seif Khatib katika vipindi tofauti. Kwa hivyo, mara zote tangu kuasissiwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika na Naibu Spika amekuwa akitokea upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya mdogo wangu hapa Mhe. Waziri Mohamed Aboud Mohamed, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Bunge hili linaendeshwa na fedha za walipa kodi wa pande zote mbili wa Jamhuri ya Muungano. Kwa kuwa Mhe. Mohamed Aboud Waziri anayesimamia mambo ya Muungano amekubali kwamba tangu Bunge hili kuasisiwa Zanzibar haijawahi kutoa Spika wa Bunge hili na kwa kuwa hakuna vigezo katika kutoa Waziri Mkuu na hatimaye kupelekea Zanzibar kutoa mara moja tu Waziri Mkuu.

(a) Je, suala hilo haoni Mhe. Mohamed Aboud ni kuidhalilisha Zanzibar katika Muungano.

(b) Kwa kuwa hakuna vigezo vinavyogawa nafasi hizi. Haoni kwamba Zanzibar inachangia uendeshaji wa Bunge, lakini hakuna vigezo vya kutoa watendaji pamoja na watu wakubwa wa Bunge hili. Huko si ndio kutumia matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi wa Zanzibar, kwa sababu hawana

tija wanayoipata katika Bunge hili kwenye kuhoji gharama kubwa pamoja na hizi za utendaji.

(c) Anaweza akanieleza kwamba ni watendaji wangapi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Zanzibar. Wote ni wangapi na ni watendaji wangapi wanaotoka Zanzibar katika Bunge hili.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba lile swali la tatu la (c) naomba arudie.

Mhe. Spika: Hebu Mhe. Mjumbe rudia kwa sauti kidogo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa heshima kubwa Mhe. Spika, na unyenyekevu wa hali ya juu, naomba nirudie kipengele (c) cha swali langu.

Je, ni watendaji wangapi wote katika Bunge lile la Jamhuri ya Muungano na katika hao ni wangapi kutoka Zanzibar.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba kwa upande wa Bunge sio Spika, wala Naibu Spika, aliyetoka kwa upande wa Zanzibar. Vile vile kwa upande wa Serikali ni Mzanzibari mmoja tu ndiye aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, haya ni baadhi ya tunayoita kero na ndio maana serikali kwa makusudi ilianzisha kamati maalum ya kushughulikia kero za Muungano. Kwa kuwa Mhe. Spika, licha ya kuzishughulikia kero hizo ambazo hatukuweza kuzimaliza zote mpaka sasa na kwa kuona kuwa upo umuhimu wa kila kero kupata ufumbuzi unaotokana na wananchi wenyewe wa nchi hii. Kwa msingi huo ndio maana serikali imeona umuhimu wa kuanzisha mchakato wa Katiba ili kila tatizo na kila ambalo linadhalilisha upande wetu wa Muungano, liweze kupata ufumbuzi sahihi kwa nia njema ya kuimarisha Muungano wetu.

Hata hili suala la watendaji Mhe. Spika, katika ngazi zetu hizi za taasisi ya Muungano, tumekubaliana kabisa kwamba yapo mapungufu na watendaji wengi wameajiriwa kutoka upande mmoja, kwa maana ya upande wa Tanzania Bara, ndio maana kwa sasa tumekubaliana mgao maalum utumike ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa taasisi ya Muungano watoke katika pande mbili za Jamhuri yetu. Kwa msingi huo sasa Zanzibar itatoa asilimia 21 ya wafanyakazi katika taasisi yoyote ile ya Muungano na wenzetu wa Tanzania Bara watapewa asilimia 79. Lakini bado Mhe. Spika, tunayo nafasi

ya mapendekezo yote ambayo wananchi watayasema, katika mchakato huu wa Katiba ili kutoa ufumbuzi wa matatizo ambayo yanajitokeza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, na mimi naomba nianze kwa kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa msiba uliomfika yeye na familia yake kwa kuondokewa na kaka yake, namuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi.

Vile vile na mimi nichukue nafasi hii kukipongeza Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa ushindi mkubwa kiliopata, katika uchaguzi wa kujaza nafasi ya Ubunge wa Jimbo la Chambani na niwapongeze watani wetu Chama cha Mapinduzi kwa kushika nafasi ya pili, chini ya asilimia imeshuka kuliko uchaguzi mkuu uliopita.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa hati ya makubaliano ya Muungano, *article of union* ambayo ndio sheria kuu, inayoongoza Jamhuri ya Muungano, nafasi ya Waziri Mkuu haikuwa imetajwa na badala yake muundo wa Jamhuri ya Muungano ulitajwa kuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wawili wa Rais, mmoja wapo akiwa ni Rais wa Zanzibar.

(a) Swali langu Mhe. Spika, ni kwamba je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kile kitendo cha kuianzisha nafasi hii ya Waziri Mkuu miaka kadhaa baada ya Muungano kilikuwa ni ukiukwaji wa hati ya msingi ya makubaliano ya Muungano.

(b) Ziko taarifa kwamba moja wapo ya mambo yaliyopelekea tofauti baina ya waasisi wa Muungano huu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Mzee Abeid Aman Karume, ilitokana na Mzee Karume kutokukubaliana na nafasi ya kuanzishwa Waziri Mkuu mtendaji, katika Serikali ya Muungano ambayo haikuwemo katika makubaliano. Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inazo taarifa hizi na kama inazo imechukua hatua gani katika marekebisho ya sasa, kuhakikisha kwamba ukiukwaji ule wa hati za Muungano zinaondoshwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli ipo hati ya makubaliano ya Muungano. Lakini vile vile Mhe. Spika, kwa sababu ya mabadiliko mbali mbali yanayotokea ulimwenguni, Jamhuri ya Muungano ilianzisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo iliridhia na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya wananchi

wote wa Tanzania. Nakusudia kusema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar na kwa niaba ya wananchi wa upande wa Tanganyika.

Kwa msingi huo mabadiliko yote yaliyofanyika yalifanyika kwa njia za kihalali na sheria na ndio maana mpaka leo tunaitumia Katiba hii na ndio maana tunaitekeleza na kuifanyia kazi. Kwa msingu huo Mhe. Spika, nataka niseme kwamba hakuna makubaliano yaliyokiukwa, isipokuwa ni utaratibu ambao tumekubaliana kuuanzisha ili kufanya kazi zetu kwa vizuri zaidi na kutoa nafasi kubwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuweza kutekeleza wajibu wake wa kuwahudumia wananchi na kuimarisha Muungano wetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza. Mhe. Spika, ninavyojua kuwa pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kwamba Tanzania ni nchi moja ndani ya Jamhuri ya Muungano. Wakati ukweli ulivyo ni Muungano wa nchi mbili wa Tanganyika na Zanzibar.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa tuliungana ili tuendelee kwa mashirikiano na mambo mengine ya kiutendaji. Je, tokea kuanza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano mpaka leo ikawa bado nafasi ya Waziri Mkuu Zanzibar imepata mara moja tu, kwa sababu Zanzibar hakuna wasomi na wenzetu hawajui umuhimu wa kutushirikisha na kuendesha ilani zetu kwa pamoja.

(b) Tunazungumza masuala ambayo ni ya Muungano yaliyokuwa ni kero na siku zote kero zinatoka Zanzibar tukifanyiwa na wenzetu wa Tanzania Bara, kwa sababu kero hizi zina maslahi yao na wizara kwa upande wetu, je hatuoni kuwa watu wanafanya kero hizi kwa makusudi na kuendesha shughuli zao na sisi kwa nini hatuoni kuwa kweli kwa huu Muungano ambao kila nchi itakuwa wenye mamlaka kamili ndio suluhisho la kuondoa matatizo haya.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba Muungano huu ni Muungano wa nchi mbili zilizokuwa huru, zikaungana na zikaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sio kweli kwamba Zanzibar haina wasomi wanaoweza kumudu nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Mfano hai ni alipochaguliwa Dk. Salim Ahmed Salim ni Waziri Mkuu aliyekuwa mahiri aliyefanyakazi zake kwa vizuri na aliyepigiwa mfano sio kwa Tanzania tu, bali hata nje ya Tanzania. Kwa hivyo, hii inaonesha wazi kwamba Wazanzibari wana uwezo mkubwa wa kuongoza Zanzibar na Jamhuri nzima ya Muungano wa Tanzania. Mliona uongozi mzuri wa mzee wetu Mzee Mwinyi wakati

alipokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, Wazanzibari wana uwezo mkubwa katika kuongoza nchi kwenye maeneo tofauti ya Jamhuri yetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa kama nilivyosema awali kuwa hizi ni baadhi ya kero na ni baadhi ya matatizo yaliyojitokeza ndani ya Muungano wetu na ndio maana tukaamua kwa makusudi kuanzisha mchakato wa Katiba mpya ambayo itaasisiwa na wananchi wenyewe kwa mara ya mwanzo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msingi wake mkubwa ni kuondosha kasoro zote hizi na kuweka msingi na muundo ambao Muungano utadumishwa, utaendelezwa na kuimarika. Kwa hivyo, ningependa kabisa kuwahakikishia wananchi wote wa Tanzania, kwamba maoni yatakayotolewa na wananchi ndio yatakayoheshimiwa na ndio yatakuwa kigezo cha kuendesha Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania, Muungano ambao utakuwa na maslahi ya pande mbili, Muungano ambao utaheshimu kila upande wa mwenzake na kuhakikisha kwamba haki ya kila upande inapatikana.

Nam. 20

Kampeni ya Upandaji Miti ili Kutunza Mazingira

Mhe. Saleh Nassor Juma Aliuliza:-

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ongezeko la hewa Ukaa limegusa kila pembe ya ulimwengu, na kwa kuwa nchi za wenzetu katika kuhakikisha suala la upandaji miti limefanikiwa wamekuwa wakitoa zawadi aidha kwa mtu mmoja mmoja, taasisi na vikundi mbali mbali vilivyofanikisha vyema kampeni ya upandaji miti.

(a) Je, Zanzibar tumeandaa mikakati gani katika kufanikisha zoezi hili.

(b) Tanzania Bara walikuwa na kauli mbiu ya kata mti panda miti. Je, Zanzibar ina kauli mbiu ipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe naomba unipe ruhusa kwa masikitiko makubwa, kwa niaba yangu na familia yangu, lakini pia kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kutoa mkono wa pole kwa kiongozi wa Ofisi yetu Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na familia yake, kutokana na msiba uliowapata wa mpenzi wao Bwana Ismail Issa Sharif. Tunamuomba Allah amlaze marehemu mahala pema na kuwapa wafiwa wote moyo wa subra.

Vile vile nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kukipongeza chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kuibuka na ushindi mkubwa wa asilimia zaidi ya 80 katika uchaguzi mdogo uliofanyika jana katika Jimbo la Chambani. Tunampongeza sana Mbunge mteule mpya na tunamuombea afya na mafanikio katika kazi yake ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika baada ya hayo sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mjumbe nambari 90 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha suala la upandaji miti linafanikiwa wizara yangu inaendelea kuandaa programu endelevu ya upandaji wa miti. Hivi sasa chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, wataalamu wa Idara ya Mazingira, Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, Idara ya Mipango Miji na Vijiji pamoja na Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanaendelea na utayarishaji wa programu hiyo. Lengo la programu hiyo ni kuwa na mpango endelevu wa kudumu wa kupanda na kuitunza miti ikiwemo ya matunda kwa kuwashirikisha wadau wote husika. Programu hiyo inakusudiwa kuzinduliwa mwaka huu mara tu mvua zitakaposhamiri na ardhi kuwa tayari kwa upandaji miti.

   Mhe. Spika, sambamba na hili, serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka imekuwa ikiendelea na harakati za kila mwaka za kupanda miti. Kwa mfano katika kipindi cha mwaka jana jumla ya hekta 270 zimepandwa miti kwa misimu ya masika ekari (240) na kwa msimu wa Vuli (30) katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba.

b) Kauli mbiu ya Zanzibar kuhusu suala la upandaji miti kwa mujibu wa taasisi iliyopewa jukumu hilo ambayo ni Idara ya Misitu, ni kwamba **TUPANDE MITI KWA WINGI, KUHIFADHI MAZINGIRA YETU.** Kauli mbiu hii imekuwa ikitekelezwa kwa mashirikiano makubwa na taasisi mbali mbali. Hata hivyo, imekuwa na changamoto kubwa ya uchache wa mvua hasa za misimu ya hivi karibuni.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Spika, mabadiliko ya tabia nchi yanaongeza kwa kasi kubwa hewa ya ukaa katika nchi, jambo ambalo linaleta dhara kwa wananchi wetu.

Kwa kuwa hewa ya ukaa inaleta dhara kwa binadamu, lakini hewa ya ukaa inatumika vizuri na inahitajika sana kwa miti, ikijitengenezea chakula chake kwa kupitia njia inayoitwa *photonthesis*. Kwa mnasaba huo miti ikiongezeka katika mazingira yetu ndio kwa kiasi kikubwa hewa ya ukaa inapunguzika katika nchi.

Je, kuna vikundi mbali mbali vinavyojishughulisha na *NGO* mbali mbali. Kwa mfano, kule jimboni kwangu kuna (*VECA*), yaani *Vitongoji Environmentary Conversation Association*. *NGO* hii inajitahidi sana katika kupanda miti. Je, kuna zawadi yoyote ambayo inatolewa kwa ajili ya kuwahamasisha hawa *NGO* kwa kazi yao hii ya kupanda miti ili kupunguza hewa ya ukaa na kutunza mazingira yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba nikubaliane naye kwamba uwepo wa miti kwa wingi kunasaidia mno kuondoa hewa ya ukaa ambayo inakuwepo na inaharibu mazingira ya nchi.

Ni kweli vikundi mbali mbali ambavyo vinajihusisha na upandaji miti vinasaidiwa na serikali hasa hivi vikundi ambavyo wananchi wenyewe wamejiunga kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Mimi binafsi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira, tumevitembelea vikundi hivi kwa wingi sana na kuvipatia misaada ya fedha taslimu. Vile vile misaada ya kuwapa miti kwa ajili ya kupanda. Pia kuwapa utaalamu na ushauri ni miti ya aina gani inahitajika kupandwa katika eneo gani.

Kwa hivyo, zawadi hasa sijui kwa Idara ya Misitu ambayo ndio hasa yenye jukumu hilo, lakini kwa upande wetu sisi kama wahusika, sisi tunavisaidia sana vikundi hivi na tunaendelea kuvihamasisha viendelee kufanya shughuli hizo za kupanda miti kwa wingi. Kama ofisi yetu haijafika Vitongoji, namuahidi tu Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba na kikundi hicho tutakwenda kukitembelea ili kuziona jitihada zao na kujua jinsi gani na wao tuwape motisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Katika Jimbo la Chaani eneo la Chaani Masingini miti mingi sana imepandwa katika awamu hii na zaidi ya miche elfu 50 imekuwa iking'olewa na kukatwa na baadhi ya wananchi wanaolitumia bonde hili.

Je, Mhe. Waziri ni hatua gani za dharura ambazo wizara yake itachukua katika kuhakikisha kulinusuru bonde hili, ili wananchi wetu wale wapate miti kwa ajili ya ujenzi na pia kwa matumizi kama kuni, ili kuweza kupunguza

tatizo la ukataji miti kiholela katika maeneo mengine. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana kwa jitihada yake ya kutembelea maeneo na kuona jitihada zinazofanyika za kupanda miti, vile vile kuona uharibifu ambao baadhi ya wananchi nao wanaofanya katika maeneo ambayo jitihada za kupanda miti zinafanywa.

Kwa kweli sheria ambayo inadhibiti ukataji wa miti ovyo ipo katika Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na kwa kweli mwananchi anaweza kuchukuliwa hatua kwa kukata miti bila ya kibali, kukata miti ovyo hasa hii ambayo inaendelea kupandwa na wananchi katika jitihada za kuhifadhi mazingira. Hata hivyo, kwa kuwa suala hili amelileta kwangu basi nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutalifuatilia kwa pamoja sisi kama mazingira na pia kwa kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka kuona kwamba wakataji wa miti hao wanadhibitiwa na miti hiyo inaendelea kupata uhai wa kuota.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa vile huu ukaa unatokea kwenye nchi zenye viwanda ambazo ni nchi zinazoendelea na zimeshaanza kusaidia nchi zilizoathirika na huo ukaa ikiwemo Zanzibar. Je, ni kiasi gani ambacho sasa tumepata kama ni fidia ya kuathirika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi zilizoendelea muda mrefu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na shughuli zao wamechafua kwa kiasi kikubwa mazingira ya dunia hii ambayo tunaishi.

Kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa nchi hizi zimetakiwa kuzichangia nchi zinazoendelea na hasa nchi ambazo ni masikini katika kukabiliana na mabadiliko haya ya tabia ya nchi. Hadi hivi sasa Zanzibar imeshapata ambazo zimeshatumiwa na kutekeleza mradi mmoja ni kama shilingi milioni 500, ambazo zilishughulikia uchimbaji wa kisima kwa ajili ya kuwapatia maji safi wananchi wa Nungwi na kuondokana na matumizi ya maji ya chumvi ambapo visima vingi vilianza kutoa maji ya chumvi katika eneo hilo.

Hata hivyo, tunategemea kwamba fedha zaidi zitaweza kupatikana katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Tatizo ni moja kwamba ahadi zinakuwa nyingi, lakini wenzetu wa nchi zilizoendelea wanakuwa wagumu sana katika kutekeleza ahadi hasa ya kutoa fedha.

Nam. 14

Usafi wa Soko la Samaki la Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante sana na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kutoa mkono wa pole, msiba huu kwa namna moja na sisi sote tuko njiani kuelekea safari hiyo ambayo imetukabili na hatujui wakati gani. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 14 lipate jawabu.

Kwa muda mrefu kumekuwepo na kilio cha samaki kutayarishwa katika mazingira machafu na kusababisha watalii kuziba pua wanapotembea soko la samaki Darajani, hali inayoendelea kufanyika licha ya kuwepo Wakuu wa Soko na Maafisa wa Afya.

(a) Kwa kuwa serikali imeshindwa kuondoa tatizo hilo kwa nini isitoe zabuni kwa mtu binafsi.

(b) Kitu gani kinasababisha samaki hadi sasa kuendelea kutayarishwa chini ya barabara tena katika mazingira machafu tofauti na utamaduni wa Mzanzibari.

(c) Kitendo hicho kinasaidia vipi kutangaza utalii wa Zanzibar nje ya nchi kama watalii na wageni wengine wanafika na kushuhudia uchafu katika sura ya nchi.

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 14 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kwanza na mimi niungane na wenzangu wote waliotangulia kutoa pole kwa kifo cha ndugu yake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, hivyo naungana na wenzangu na sote tuko kwenye msiba huu na tunamuombea maghufira marehemu.

(a) Serikali inaelewa hali isiyoridhisha kiafya ya Soko Kuu la Darajani na mazingira ya soko la samaki. Kwa kweli soko hilo ni la zamani na limejengwa katika miaka ya 1904 na 1905, hivyo kutokukidhi mahitaji makubwa ya wauzaji na wanunuzi kwa hali ilivyo sasa ya idadi ya watu.

Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, serikali imejipanga kulifanyia matengenezo makubwa soko la samaki katika mwaka ujao wa fedha, ili liwe la kisasa na kurekebisha kasoro nyingi zilizopo ili liweze kukidhi haja ya wakati ulivyo hivi sasa. Mhe. Spika, serikali imeshafungua milango siku nyingi kukaribisha watu binafsi kushiriki katika kazi za usafi wa miji yetu na hata masoko kukidhi haja kwa wakati uliopo na tayari vikundi kadhaa vimejitokeza kuanza kazi hizo.

(b) Kwa bahati mbaya sana tabia ya kuuza samaki chini imejengeka kwa baadhi ya wachuuzi wa samaki na biashara nyengine ndogo ndogo. Serikali imekuwa ilitoa elimu kwa ujumla pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wanaoendelea kuhalifu sheria. Nawaomba sana Waheshmiwa Wawakilishi wenzangu kwamba tushirikiane na Waheshimiwa Madiwani na Baraza la Manispaa kuzidi kutoa elimu kwa wapiga kura wao juu ya umuhimu wa kuweka mazingira ya usafi, yaani sote tukerwe na uchafu.

(c) Serikali haipendezewi na hali iliyojengeka sasa ya kuwa na masoko machafu sio tu kwa kukuza utaalii bali hata kwa afya ya wananchi wenyewe. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma na pia kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaokaidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kutokidhi swali la msingi karibu miaka mitatu au miwili ndani ya Baraza hili tumekuwa tukilipigia kelele suala hili.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza kutuambia watendaji wangapi waliochukuliwa hatua baada ya kushindwa majukumu yao kama wao wanavyochukua majukumu kwa watendaji wengine.

(b) Kuna umuhimu gani wa kuwaajiri maafisa wa afya wakati wanashindwa kusimamia Halmashauri zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Spika, wiki iliyopita nilijibu swali linalolingana kama hili na nilisema kwamba Baraza la Manispaa lilifungua jumla ya kesi zipatazo 189 za wafanyabiashara wadogo wadogo wanaohalifu sheria hii ya kufanya biashara kiholela na kufanya uchafu. Mhe, Spika, kuhusu suala lake kwamba tutaendelea mpaka lini hali hii.

Mimi nafikiri sote suala hili tusaidiane kwa sababu hivi asubuhi mimi nimeamkia marikiti Mhe. Spika, na iko safi na inapendeza kabisa. Sasa njoo saa 8 au 9 wanaochafua yale mazingira nani lazima tujiulize wanaochafua nani. Kwa hivyo, ndio maana tunavyosema kila mmoja afanye wajibu wake. Kwa mfano, hivi sasa mimi niko tayari kwenda tena twende zetu mimi na yeye twende marikiti hivi sasa kunapendeza, lakini wakati wa saa 8 au 9 kwa kweli tunatupa uchafu kiholela badala ya kuweka taka zikachukuliwa.

Mhe. Spika, jambo la kufurahisha siku hizi lile gari la taka kwenye jaa letu pale zamani tukisema harufu mbaya ya samaki lipo muda wote pale na wala haliondoki siku hizi, kwa hivyo zile taka za mavumba kunuka nashukuru na sijui Mhe. Mwakilishi samahani *sense* zake za kunusa ziko vipi, lakini kama ziko vizuri basi nafikiri kuna tofauti pale, ndio maana nasema sijui kwani kila mmoja anazo *sense* zake za kunusa. Lakini naamini kabisa vumba kali sote tunakerwa na uchafu ule.

Kwa hivyo, yapo mabadiliko makubwa Mhe. Mwakilishi, lakini naomba tujitahidi sote tuwaelimishe watu na wala haina maana kwamba Manispaa wao wafyagie tu au wasafishe tu na wengine wachafue tu aah! Hiyo haipendezi. Kwa maana hiyo, hili ni suala letu sote tushirikiane kama nilivyosema tena ninao mfano mzuri sana, nenda pale marikiti upande wa nyuma kule kwenye soko la matunda na mboga mboga wamekubali na wameelekezwa wamejenga vichanja na wamepanga vitu vyao na inapendeza kabisa na utakuta watalii mule ndimo wanamopiga picha hasa, lakini wale wamekubali na wako wengine hawakubali na wanakuwa wanafanya ubishi hasa. *(Makofi).*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mbali ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri katika Soko la Darajani mbali na kuzuka kwa wimbi hili la uchafu wa samaki. Lakini kumezuka wimbi la wafanyabiashara wa vitu chakavu ambapo wakati wa jioni wafanyabiashara wengi humiminika pale kwa ajili ya kuuza biashara zile ambapo huleta msongamano na kuleta hali ya uchafu katika maeneo yale.

Vile vile tumeondoa yale mazoea ya biashara ile ya siku ya Jumapili na Jumatano, ambapo tumeziweka kwa ajili ya kuuza vifaa mbali mbali ambapo wafanyabiashara hufanya biashara zao pale. Mhe. Spika, hivi sasa watu kuanzia siku ya Jumatatu hadi Jumapili hufanya biashara zao kwa vitu chakavu.

Je, utaratibu ule haoni Mhe. Waziri kwamba unasababisha kule hali ya uchafu katika soko la Darajani.

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli wapo wafanyabiashara wanaotumia magari kuuza vyombo na hata baadhi ya mitumba. Lakini kwa kweli sisi tunawatafutia mahala wale wakae kwa ajili ya kuuza vitu vyao na sio kwenye barabara kubwa kama vile Darajani wana-*block* upande mzima wa barabara wanaweka gari zao na wala haipendezi.

Lakini hata juzi na hivi sasa tuko kwenye msimu wa machungwa basi utaona vi-*carries* vingi vimekaa Darajani pale wanauza machungwa na hivi sasa machungwa ni mengi na watu wengi wamezongea na wana-*block traffic*, kwa kweli haya ndio mambo niliyoyasema ya kuhalifu sheria.

Sasa tujajitahidi kwa kushirikiana na Kitengo cha Usalama Barabarani kwanza kuwatafutia mahala wale na halafu kuweza kuondosha mambo kama haya madogo madogo na ushauri wako tumeupokea Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kwa kifo cha kaka yake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema peponi roho ya marehemu. Vile vile niungane na wenzangu kukipongeza Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kupata ushindi katika Jimbo la Chambani na pia nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kushika nafasi ya pili kwa kupata kura 399. (*Amin*). *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa naomba nimuulize swali Mhe. Waziri. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kama lile jaa ambalo lilikuwa likiweka harufu mbaya zaidi pale Darajani kwa kiasi fulani ile harufu imepungua wanajitahidi kusafisha, ili harufu ile iondoke na kuweka mazingira mazuri ya mji wetu.

Pamoja na hayo, Mhe. Spika wananchi wa Zanzibar wameitikia wito wa serikali kujiajiri na kujipunguzia umasikini. Sasa Mhe. Spika, niungane na wenzangu kusema kama wapo wananchi wanaouza samaki chini, basi serikali kuna haja ya kuwawekea mazingira mazuri wakauza samaki wao bila ya fujo. Vile vile kitendo cha askari kwenda kuwavamia wananchi na kuwapiga marungu na kuwanyanyasa, hali hii haileti sura nzuri kwa nchi yetu kwa sababu inakuwa wale wananchi tunawanyima uhuru. Kwa hiyo, kama kuna mazingira mabaya, hivi Mhe. Waziri haoni kama kuna haja ya kutoa elimu na

kuwaelimisha pamoja na kuwatafutia mazingira mazuri bila ya fujo wala ghasia na kuliko kuwapiga marungu na kuwanyanyasa.

Mhe. Spika, kama hivyo ndivyo basi ni lini Mhe. Waziri atawapa elimu nzuri na kuwapa sehemu nyengine, ili wafanye biashara zao kama nchi nyengine wanavyofanya biashara zao bila ya ghasia na wajione kama wao katika uhuru ndani ya nchi yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza mimi nakubaliana kabisa na rai aliyoitoa Mhe. Mwakilishi, kwamba tujitahidi tuwaelimishe wafanyabiashara wetu na wao wanatafuta riziki na hilo tunakubaliana nalo.

Lakini ninachosema na nilisema kwenye jibu langu mama kwamba tunajitahidi kutoa elimu na tunawafahamisha tena nasema tunawabembeleza hasa na tofauti, na kwengine na hili nalisema mara nyingi sana kwa sababu sisi huwa tunawauliza Wakurugenzi wa Mabaraza ya Miji au Manispaa kama vile Kinondoni au Mwanza ama Moshi nyinyi munaweza vipi kutunza miji yenu. Wanasema tunatumia FFU kwa ajili ya kuwaondoa kwa sababu watu wakaidi lakini sisi tunasema hatufiki huko, kwani FFU (Fanya Fujo Uone) na wala sisi hatupendelei twende huko na siku zote huwa ninatoa mfano huo na sisi hapa ni wenyewe kwa wenyewe.

Lakini Mhe. Mwakilishi tunaomba utusaidie kama sheria inakataza basi tusifanye na sisi tutajitahidi kutafuta mazingira mazuri ya kuwajengea mahala na kuwaweka basi naomba tusaidiane hilo. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwani huwa tunakutana sana pale sokoni wakati mimi niko kwenye kazi zangu basi yeye anazungumza na wale wafanyabiashara, kwa hiyo tusaidiane Mhe. Mwakilishi.

Nam. 65

Ajira katika Vikosi vya SMZ

Mhe. Saleh Nassor Juma Aliuliza:-

Vikosi vya SMZ ni vikosi vinavyoendeshwa kupitia kodi za wananchi wote wa Unguja na Pemba. Aidha sare, vifaa pamoja na stahiki nyengine hutokana na fedha za walipa kodi.

(a) Je, ajira za vikosi hivi zinatolewa kwa utaratibu gani.

(b) Ni sababu gani za msingi zinazopelekea kuwepo kwa malalamiko makubwa juu ya kuwepo kwa upendeleo katika kutoa ajira za vikosi hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Napenda nikubaliane na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba Vikosi vya SMZ ni vikosi vinavyoendeshwa kupitia kodi za wananchi wote wa Unguja na Pemba. Aidha sare, vifaa pamoja na stahiki nyengine hutokana na fedha za walipa kodi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Ajira za vikosi vya SMZ zinatolewa kwa kuzingatia utaratibu kama ulivyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya Mwaka 2011 pamoja na Sheria ya Tume ya Idara Maalum Nambari 6 ya Mwaka 2007.

(b) Mhe. Spika, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora haioni kwamba kuna sababu za msingi na wala haijapata malalamiko rasmi yanayoashiria kuwepo kwa upendeleo katika kutoa ajira za vikosi. Kimsingi utaratibu wa ajira katika vikosi vya SMZ ni ule ulioainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya Mwaka 2011 kifungu cha 57(3) (a) – (c) kinafafanua zaidi juu ya utaratibu wa ajira.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri anayehusika na mambo haya ya utumishi naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu naomba uniruhusu dakika moja nitoe maelezo ya utangulizi kwa swali langu hili.

Wanafalsafa wanasema kwamba “mapendeleo yakiachiliwa mbali nuru ya ukweli na mafanikio hufunika kwenye ukweli siku zote kulikoni uongo”, mwisho wa kunukuu.
Mhe. Spika, pamoja na kusema kwamba Mhe. Waziri hajapokea malalamiko ya dhahiri kuhusiana na manung’uniko ya upendeleo wa ajira hii. Lakini

nataka nimueleze kwamba kuna manung'uniko makubwa kwamba ajira za vikosi hivi zinatoka kwa upendeleo sana, yaani zinatoka aidha katika misingi ya kieneo, kivyama na kadhalika.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza kuniruhusu nikafanya *therapy feasibility study* na nikakuletea jinsi ya nafasi ya wilaya kadhaa ambazo zimepewa nafasi, lakini nafasi zake wamepewa watu aidha kutoka Tanzania Bara au kisiwa chengine kuliko ile wilaya iliyokusudiwa, unaweza kuniruhusu kufanya hivyo.

(b) Katika ajira za mwisho zilizofanywa za vikosi ni nafasi ngapi zilitoka Pemba na ngapi zilitoka Unguja, hivi anaweza kunipa takwimu hiyo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali langu mama kwamba sheria inaelekeza panapokuwa na malalamiko na upendeleo baada ya mchakato wa ajira kukamilika ndani ya miezi mitatu, mtu yeyote anaruhusiwa kupeleka malalamiko yake yaliyokuwa rasmi.

Mhe. Spika, nataka nirejee kusema kwamba ofisi yangu kupitia Tume ya Utumishi Idara Maalum na Kamisheni ya Utumishi wa Umma haijapokea malalamiko rasmi.

Sasa Mhe. Mwakilishi kama hayo malalamiko yapo basi naomba wanaolalamika wafuate utaratibu na malalamiko yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na Kamisheni ya Utumishi wa Umma inapogundua kwamba yapo malalamiko na upendeleo basi ajira hiyo inasitishwa na kutangazwa upya. Kwa hivyo, ninachosema ni kwamba malalamiko hayajakuwepo.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua kwamba nafasi ngapi zimekwenda Pemba na ngapi zimekuja Unguja. Kwanza nafasi hazitangazwi kwa Upemba na Uunguja, isipokuwa nafasi zinatangazwa kwa Wazanzibari na Sheria ya Ajira inasema kwamba watakaoajiriwa ni Wazanzibari awe Pemba au Unguja. *(Makofi).*

Katika mchakato huu wa ajira unaoendelea sasa tunachokifanya ni kwamba mahitaji gani yako Pemba na mahitaji gani yako Unguja, lakini Mpemba anaruhusiwa kuajiriwa Unguja na Muunguja anaruhusiwa kuajiriwa Pemba. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuhusu suala la takwimu nzuri juu ya ajira nafikiri ofisi yangu haijapokea mgawanyo ulikwenda vipi katika vikosi, lakini takwimu inaweza

ikawa katika vikosi kwamba kikosi hiki kina wangapi na chengine kina wangapi, lakini haiwezi kusema Pemba wametoka wangapi na Unguja wametoka wangapi. *(Makofi)*

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna Tume ya Utumishi wa Idara Maalum, tume hii inashirikisha vipi katika uajiri wa askari wa vikosi hivyo na ikiwa inashirikishwa ni lini ilitoa matangazo ya mahitaji ya uajiri kama inavyofanya Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nataka nimthibitishie kwa mujibu wa sheria kila tume ndio inayofanya mchakato wa kuajiri watumishi wake.

Kwa hivyo, Tume ya Idara Maalum ndiyo iliyopewa nafasi hii na baada ya kupata nafasi hizi miezi mingi iliyopita nyuma Tume ya Idara Maalum ilitangaza nafasi hizi za ajira za Vikosi vya SMZ na wala kazi hizi hazikutangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini, isipokuwa nafasi hizi zilitangazwa na Tume ya Idara Maalum ya SMZ. *(Makofi).*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Lakini kabla sijauliza na mimi nataka nielezee kidogo tu, kinachoonekana hapa na kulalamikiwa ni tatizo kubwa la ajira katika nchi yetu kwamba mahitaji ya wanaohitaji ajira kwa vijana yamekuwa ni makubwa, lakini uwezo wa serikali kifedha umekuwa mdogo hata yale mahitaji yenyewe kwa wale wanaoajiriwa, kwa sababu unatakiwa umuajiri mtu kwa nafasi ya kazi ambayo yeye atakwenda kuifanyia kazi.

Sasa kama hivyo ndivyo ilivyo Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara wamejaribu kuanzisha mfumo kupitia vikosi kama hapa JKU na kule wenzetu ni JKT, ili kuona namna gani wanaweza kuwasaidia vijana kuondokana na hili wimbi la ajira.

Kwa mfano, wameanzisha utaratibu wa kuanzisha Skuli za Ufundi, pia hivi sasa wako mbioni kuanzisha kampuni binafsi katika JKT, ili vijana wanapomaliza kupata mafunzo basi waweze kuajiriwa kwenye makampuni binafsi.

Je, Serikali yetu ya Zanzibar imejiandaa vipi na mikakati madhubuti ili kuandaa utaratibu mzuri kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu katika suala zima la ajira.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo kubwa linalosababisha pengine haya malalamiko ni kutokana na mahitaji makubwa sana ya vijana ambao wanahitaji ajira.

Kwa mfano, jana Mhe. Spika, kule kwenye semina tuliambiwa vijana ambao hawana ajira Zanzibar ni laki moja, nafasi ambazo tumezipanga katika bajeti iliyopita nafasi rasmi za ajira kwa Utumishi wa Umma ni nafasi 2552. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba inaonekana tatizo la ukubwa wa ajira.

Je, serikali imejipanga vipi. Nadhani kwenye bajeti iliyopita ambayo imewasilishwa na Mhe. Waziri Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na bajeti za sekta moja moja, basi kila sekta itakuja na utaratibu wa namna gani imejipanga katika kuondokana na hili tatizo la ajira. Kwa mfano, kuanzisha vyuo vya amali, suala la kuwajengea uwezo vijana kujiajiri wenyewe na mambo mengine. kimsingi serikali imeliweka na hata katika bajeti hii nimeona karibu bilioni 1.1 zimetengwa kwa ajili ya kuondosha tatizo hili la ajira ya vijana. Ahsante sana.

Nam. 45

Nyongeza ya Mishahara kwa Mahakimu

Mhe. Nassor Salim Ali Aliuliza:-

Kwa kuwa suala la maslahi ya wafanyakazi wa Mahkama wakiwemo Mahakimu wa Mahkama ya mwanzo pamoja na wafanyakazi wa kawaida linaendelea kuleta manung'uniko ambapo bado ahadi ya Wizara haijatekelezeka.

(a) Je, Waziri anaweza kueleza amekwama wapi juu ya malipo hayo.

(b) Je, nyongeza zao na malimbikizo yatalipwa lini.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 kama inavyofuata:-

(a) Suala la Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo limeshashughulikiwa na kwa sasa Mahakimu hao wanalipwa kulingana na kiwango chao cha elimu. pia wameongezewa na posho maalum la shilingi laki mbili na hamsini elfu kwa kila mwezi.

(b) Hakuna deni wanalodai wizarani na kile ambacho walichokuwa wanadai chote kimeshalipwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, kwa nini kumekuwepo na tofauti ya viwango vya mishahara vya waendesha mashtaka pamoja na Mahakama ya mwanzo, wakati kazi wanayoifanya ni ya aina moja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza waendesha mashtaka na Mahakimu ni watu tofauti na kazi zao ni tofauti, yule mmoja anatoa ushahidi na anaendesha kesi huyo ndio muendesha mashtaka. lakini Mahakimu wao wanasikiliza halafu wanaamua. kwa hivyo kazi zao ni tofauti.

Lakini la pili kama nilivyosema hapa, hawa Mahakimu wa mwanzo walipewa mshahara wao kwa mujibu wa viwango vyao vya elimu. **B**aada ya kuona kwamba wanakazi muhimu zaidi tukawaongezea kwa maagizo ya Mhe. Rais kiasi cha shilingi laki mbili na hamsini elfu (Sh. 250,000/-) kila mwezi, mbali na mshahara wao wanaopata ili kuheshimu kazi yao ambayo wanaifanya.

Nam. 76

Vituo Tembezi vya Ununuzi wa Karafuu

Mhe. Saleh Nassor Juma Aliuliza:-

Zao la karafuu bado linaendelea kuwa zao kubwa la biashara katika visiwa vyetu, kwa kuwa kuna maeneo mengine ya visiwa hivi hususan maeneo ya maweni hayana zao hili la karafuu. lakini wakazi wake wengi humiliki mashamba haya katika maeneo yaliyo mbali na makaazi yao na hivyo kuvuna mazao hayo na kuyahifadhi wanakoishi ambako hakuna vituo vya serikali vya kununulia zao hilo, jambo ambalo hulazimika kusafirisha karafuu zao katika masafa marefu kwa ajili ya kuuza.

Ni lini serikali itaanzisha vituo tembezi vya ununuzi *(mobile units)* kwa ajili ya kununulia karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi na mimi niungane na Waheshimiwa waliotangulia kusema toka asubuhi kwamba tumtakie Mwenyezi Mungu amjaalia kaka yake Makamo wa Kwanza wa Rais kila la kheri katika msiba, wawe na subra na aliyetangulia mbele ya Haki Mwenyezimungu amjaalie malazi mema.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilisi swali lake Nam. 76 lenye kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hivi sasa serikali haina utaratibu wa kutumia vituo tembezi *yaani (Mobile units),* lakini hata hivyo Shirika la ZSTC limeweka utaratibu wa kumfuata mkulima ambaye amevuna karafuu nyingi na anahitaji kuziuza. Pamoja na hatua hiyo ZSTC Mhe. Spika, imejenga vituo vya kununulia karafuu katika maeneo yote muhimu yaliyo na karafuu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri fupi sana lakini makini naomba niulize swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa juzi juzi tu Waziri wa Biashara hapa alitujibu kwamba ukaushaji wa zao la karafuu utaendelea kutumia muangaza wa jua. Na kwa kuwa katika kipindi cha uvunaji wa karafuu Mhe. Spika, maeneo yanayozalisha karafuu kama vile ukanda wa Magharibi wa kisiwa cha Pemba mara nyingi huwa na mvua kubwa sana kiasi ambacho karafuu huwa hazikauki vizuri na huwa zinapatikana mpeta.

Na kwa kuwa ukanda wa Mashariki Mhe. Spika, katika Kisiwa cha Pemba niseme kunakuwa na jua mara nyingi. wakulima wa karafuu kutoka maeneo ya Magharibi hulazimika kuja kukaushia karafuu zao katika ukanda wa Mashariki ambapo jua huwa linapatikana muda mwingi katika kipindi cha mwaka. Lakini wanakumbana na vikwazo vya askari polisi na mageti barabarani pale wanapokuja kuanika karafuu zao katika maeneo ya Vitongoji maeneo ya Uwandani, maeneo ya Muwambe, huwa wanapata vikwazo vya karafuu zao kuzuiliwa.

(a) Je, ni lini serikali itatoa targis kwa maana ya vibali ili wakulima wale kuweza kutoa mazao yao na wakati wa mvua kubwa kuja kuanika katika sehemu ambayo jua linapatikana.

(b) Kwa kuwa mara nyingi huwa wanasumbuliwa kupeleka mazao yao Mashariki, si bora wangeanzisha utaratibu wa kisayansi tukawalipia hizo mashine kuliko karafuu kuwa mpeta nakupoteza bei siku zote.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, utaratibu tunaoutumia katika kukausha karafuu kama alivyosema Mhe. Waziri ni kwa kutumia jua. Utaratibu huu umekuwa ukitumika tokea enzi na dahari na hakuna tatizo lolote katika kuhamisha karafuu kama zinakwenda

kukaushwa kwa ajili ya kwamba zikishakauka basi ziuzwe, hakuna tatizo hilo Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba nitangulie kusema kwamba natoa pole kwa niaba ya wananchi wangu wa Kiwani kwa msiba ambao umempata Makamo wa Kwanza wa Rais na familia yake baada ya kufiliwa na kaka yake.

Vile vile nitoe pongezi sana sana kwa viongozi wetu wawili wa serikali ambao ni Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kuendesha Kampeni Chambani kwa njia ya ustaarabu na heshima kubwa. hatukuwasikia hata siku moja wakitoa lugha za matusi, kwa niaba ya vyama vyao. Kwani wapo waliosimama kwenye jukwaa wakalia, wakatukana na wakaapiza. Lakini hatimae viongozi hawa wameendesha kampeni kwa ustaarabu mkubwa.

Mhe. Spika, kwa msingi huo ni dhahiri kwamba CCM na CUF ndio vyama pekee ambavyo vinaweza kuongoza nchi hii kwa mbadala. Sasa naomba niulize swali (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali imesema kwamba haijazuia kuhamisha karafuu kutoka eneo moja hadi jengine kama kuna lengo la kuanika karafuu hizo. na kwa kuwa eneo la Ngomeni linakarafuu nyingi na ni eneo ambalo mvua haiyondoki kila wakati. Na kwa kuwa wananchi wangu wa jimbo la Kiwani wanaolima karafuu kule Ngomeni mara zote huzuiliwa kuhamisha karafuu Ngomeni na kuleta Muwambe.

(a) Je, mara hii Mhe. Naibu Waziri anaweza kunitamkia hapa kwamba wananchi wangu hawatazuiliwa na hasa kwa vile uvunaji wa zao hilo tayari unaanza.

(b) Kwa kuwa maeneo kama haya ya Ngomeni na maeneo mengine yamekuwa na upungufu wa jua. kwa nini serikali haiyandai kuyatibu kwa kuagizia mitambo ya Bayo gases wananchi wale wakakausha karafuu kitaalamu ili kuendesha usumbufu ambao ungewapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naendelea kusema kwamba kama karafuu zinahamishwa kwa ajili ya kwenda kukaushwa baso hazizuiliwi, ndio utaratibu uliokuwepo kwamba watasimamishwa katika vituo vilivyowekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanakwenda kweli kuzikausha na si vyenginevyo, ikibainika kwamba karafuu zile zinakwenda kwa utarabu wa kwenda kukaushwa

vinaachiwa na zinakwenda kukaushwa. Utaratibu huu umekuwa ukiwempo na unaendelea kutumika kama hivyo.

Lakini nimuelimishe ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba karafuu zinazokaushwa kwa jua ndizo zinakuwa na ule ubora unaotakiwa katika soko la dunia. Na kwa kuwa ni tatizo ambalo kuwa tukiliendeleza tokea huko nyuma na ndilo suala lilopelekea karafuu zetu Zanzibar zikawa zinakubalika kwa kiasi kikubwa katika soko la dunia. Basi bado ni vyema tukaendelea na utaratibu huo huo wa kukausha karafuu zetu kwa jua ili ubora ule uendelee kubaki katika karafuu na tuweze kuziuza vizuri katika soko la dunia.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Nakushukuru Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

(a) Katika maelezo ya suala la msingi lilieleza kuwa ardhi ya maweni hawana zao la karafuu. Na kwa kuwa ardhi ya maweni ni sehemu kubwa ya ardhi ya visiwa vya Unguja na Pemba. Je, Mhe. Waziri kuna utafiti wowote uliofanywa kitaalamu ulioonesha zao la karafuu halistawi katika ardhi hizo.

(b) Kama ulifanywa utafiti huo ulifanywa mwaka gani.

(c) Kama haujafanywa utafiti huo je, wizara yake haiyoni kuna umuhimu wa kufanywa utafiti huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, suala la ufafiti wa mazao ya kilimo ikiwemo karafuu liko chini ya Wizara ya Kilimo, kwahiyo ninavyofahamu serikali kwa sababu ya hiyo *collective responsibility* tunajua kwamba Wizara ya Kilimo imo katika kufanyia utafiti mazao yake ikiwemo miti hii ya karafuu.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa Mwakilishi awe na subra tusubiri matoke ya utafiti huo kutoka Wizara yatu ya kilimo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata kuna wageni ambao taarifa ya wageni hawa imechelewa kidogo kufika. Kwa hivyo baada ya maswali niwatambulishe kweni wageni hao. Wageni hao ni wageni wa Mhe. Nassor Salim Ali mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo. Wageni wenyewe ni ujumbe wa viongozi wanane kutoka jimbo hilo la Rahaleo wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa jimbo hilo ndugu Juma Khamis. Nawaomba wageni hao wote wasimame kwa pamoja ili kuwasalimu viongozi.

Ahsanteni sana wageni wetu karibuni katika shughuli zetu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2013/2014 - Wizara ya Nchi, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja iliungwa mkono tangu mapema na pia Hati ya Mwenyekiti wa Wenyeviti, iliwasilishwa, kwa niaba yake tangu siku ya Jumatano kwa hivyo sasa moja kwa moja tuendelee na mjadala baada ya kuungwa mkono katika chombo chetu hichi cha kutunga Sheria.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Kwanza na mimi tumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kufika hapa tukiwa ni wazima wenye afya njema. Pili niungane na wenzangu waliotangulia kwa kumpa pole Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na familia yake kwa msiba walioupata, tunawatakia Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra.

Mhe. Spika, vile vile tukiendelea nataka niwapongeze wananchi wa jimbo la Chambani kwa kuweza kufanya uchaguzi bila ya kuwa na vurugu, bila ya kuwa na matatizo yoyote na tuwapongeze wale walioshinda. Lakini vile vile jambo ambalo tunalolitaka kwamba kama tunavyojua chaguzi zina mambo mengi kwa hivyo yaliyopita si ndwele watu waendelee kushikamana na kushirikiana katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nataka niendelee tena kukushukuru wewe kwa kuweza kuliongoza Baraza lako tukufu kwa uwadilifu mkubwa na bila ya kujali pande gani inayozungumza. vile vile niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano makubwa ambayo wameipatia Kamati yangu kwa muda wote tuliokuwa tukipitia bajeti hii ya serikali.

Vile vile naendelea kuwapa shukurani Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na wasaidizi wake Makamo wa Kwanza wa Rais Mwalimu Seif Sharif Hamadi pamoja na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Iddi kwa uimara wao kwa kuweza kuisimamia nchi yetu hasa katika kulinda amani na utulivu tuliokuwa nao. tunawaomba wananchi watupe mashirikiano na waipe mashirikiano serikali katika kuweka amani na utulivu ili kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nataka pia niwashukuru wajumbe wangu wa Kamati ambayo kwa kipindi hichi kwa bahati nilikuwa katika safari ya kikazi

lakini walifanya kazi vizuri na leo ndio matunda yake haya tunayaona. Mhe. Spika, nitaomba niwataje wajumbe wa Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Salmin Awadh Salmin	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mjumbe
5. Mhe. Ussi Jecha Simai	Mjumbe
6. Mhe. Omar Ali Shehe	Mjumbe
7. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mjumbe
8. Ndg. Shemsa Maabad Moh'd	Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Tunawashukuru sana kwa mashirikiano waliyotupa.

Mhe. Spika, nikiendelea na hotuba yangu nitaomba radhi tu kidogo kwa sababu kutokana na matatizo ya mitambo hotuba ilichelewa kidogo kupatikana, lakini naamini si muda mrefu itaweza kugaiwa kwa wajumbe kwa sababu kulikuwa na mabadiliko mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alieleza matukio machache yaliyojitokeza ya uvunjifu wa amani katika nchi yetu na pamoja kwamba ameeleza kwamba hali iko shwari, lakini bado katika wiki hii iliyopita kuna baadhi ya matukio yametokea ya vijana kuandamana na mabendera bila ya utaratibu. Bado naomba Mhe. Waziri pamoja na hali hii ya amani na utulivu tuliyokuwa nayo lakini jeshi la polisi pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viendelee kuhakikisha kwamba kila wakati wanaangalia usalama katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri vile vile ameelezea hali ya kiuchumi ya duniani katika Bara la Ulaya na Asia pamoja na Kanda ya Afrika pamoja na nchi yetu sisi. Pia ameelezea mfumko wa bei duniani na katika kanda ya Afrika pamoja na hapa Zanzibar.Hali hii ya mfumko wa bei duniani pamoja kwamba inaendelea kushuka lakini bado tufanye jitihada za makusudi katika kuhakikisha tunazalisha mali kuanzia kilimo na kuweza kuimarisha viwanda. Tunashukuru bei ya mafuta katika kipindi hichi cha mwaka uliopita haikutetereka sana na ndio maana hata bei ya mafuta haikupanda sana kwa hivyo mfumko wa bei kwa kiasi fulani haukuwa mkubwa.

Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Waziri kuelezea hali ya uchumi na kuwa na mwenendo mzuri wa kufikia asilimia 7 ukilinganisha na asilimia 6.7 ya mwaka 2011 lakini bado hali hii kama ingelikuwa na usimamizi mzuri wa miradi ambayo inaendelea ambayo imechukuwa muda mrefu ambao

usiokwisha. Miradi hii inapunguza kasi ya ukuwaji wa pato la taifa na kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, naomba sana serikali yetu hasa katika miradi ambayo imekaa kwa muda mrefu mfano kama Uwanja wa Ndege wa Kimaita wa Zanzibar na pia barabara za kule Pemba basi serikali ihakikishe kwamba ndani ya kipindi hiki zinakamilika ili kuweza kuongeza pato la taifa kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba sana katika jambo ambalo tunaweza tukaongeza uchumi wetu na kupunguza huu mfumko wa bei na urari wa biashara ni vyema kuimarisha maeneo huru kiuchumi. Serikali yetu imeweza kuanzisha maeneo huru ya kiuchumi Fumba na Micheweni lakini bado mpaka leo hatujaandaa mpango mkakati wa kuweza kuboresha maeneo hayo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri vile vile alielezea pato la mtu binafsi limeongezeka kutoka laki tisa na sitini kwa mwaqka ambayo sawa sawa na dola mia sita na kumi na saba ambayo ukifanya mahesabu ya haraka haraka ni sawa sawa na shilingi elfu thamanini kwa mwezi ambayo kwa siku inachukua karibu elfu mbili na mia sita na sitini na saba.

Mhe. Spika, pato la taifa ameelezea na pato la mwananchi wa kawaida limeongezeka kutoka laki tisa na sitini hadi milioni moja na elfu tatu sawa sawa na dola mia sita na thalathini na nane, ongezeko la asilimia 4.5. hiki bado ni kiwango kidogo ukilinganisha na asilimia 11.5 ya mfumko wa bei za bidhaa hapa Zanzibar. ndio maana nikashauri kwamba tuimarishe miundombinu ya maeneo huru ya kiuchumi ili kuvutia wawekezaji na kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wetu.

Kipato hichi cha elfu mbili na mia nane kwa pato la sasa kwa siku bado ni kidogo sana. Inabidi sisi waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuishauri vyema serikali yetu na kuongeza kasi ya uwajibikaji na kubuni miradi mipya itakayoweza kuongeza pato la mwananchi ikiwemo, uvuvi, kilimo na mazingira mazuri ya biashara na kurahisisha taratibu ili rasilimali alizotujaalia Mwenyezi Mungu tuzishughulikie ili neema hii iwafikie wananchi wengi. Naamini tukiweza kufanya hivyo ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo basi pato la mwananchi litaongezeka kutoka mia 960 na kuongezeka mara mbili zaidi hadi milioni nne, laki tatu na ishirini.

Mhe. Spika, hichi ndicho kiwango ambacho wananchi wetu wanachohitaji hivi sasa. Kwa hivyo zinahitajika jitihada za pamoja kwa kutumia maarifa yetu ili kuongeza ukuwaji wa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na ukuaji katika michango ya kisekta na kuimarika kwa huduma katika mchango wa pato la taifa mchango wa huduma ni asilimia 8.6 na ile sekta ya Kilimo mchango

wake kushuka kutoka asilimia 2.7 hadi asilimia 1.3. Hii sio dalili nzuri kwani bado uti wa mgongo wa uchumi wetu tunategemea kilimo. Asilimia zaidi ya 50 ya wananchi wetu wanategemea kilimo ambao wanaishi vijijini.

Mchango mdogo wa kilimo katika pato la taifa hili ni lazima tujiulize ni nini kilichosababisha hali hii. Kwa hiyo tuimarishe na tutoe elimu kwa wananchi wetu na kuwapa pembejeo na mbolea pamoja na mbegu kwa wakati pia kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji. Ni vyema kuwapatia dawa za wadudu waharibifu wa mazao na kuwapatia mikopo wakulima na kuongeza kilimo cha mazao ya biashara ili kupunguza nakisi ya uingizaji wa bidhaa kutoka nje.

Mhe. Spika, serikali yetu iandae mipango bora ya matumizi ya ardhi na kuyatambua na kuyalinda maeneo ya kilimo, kwani hivi sasa maeneo ya kilimo amekuwa yakivamiwa kwa kasi, hii inaweza ikapelekea kila mwaka sekta ya kilimo inaweza kupungua uwezo wake katika kuchangia pato la taifa.

UKUAJI WA SEKTA YA VIWANDA

Pamoja na kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza ukuaji wa viwanda umeongezeka kwa asilimia 9.2. Hapa Mhe. Spika, mimi sijakubaliana na nitaomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa kina kwa sababu bado kwa upande wetu Zanzibar sasa hivi hatujakuwa na viwanda hasa ambavyo tunavyoweza kuzalisha au kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri vile vile ameelezea kwamba pato la taifa limeongezeka, ujenzi wa nyumba za kuishi lakini bado Serikali ilifanyie kazi ya ziada eneo hili kwani eneo hili linaweza sana kuongeza pato la taifa, na mimi nina mawazo yafuatayo:

Serikali iandae mpango maalum wa kutenga maeneo ya ujenzi wa nyumba za kisasa na kuimarisha na kuboresha makaazi ya wananchi wetu kwa kutafuta wawekezaji katika miradi ya "*Real Estate*", kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora za kisasa na maeneo ya biashara. Mhe. Spika, kwani hivi sasa tayari kuna baadhi yameshaanza kujitokeza Zanzibar na vile vile Mhe. Spika, wameonana na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na wana nia ya kuekeza katika miradi hii ya ujenzi wa wa *Real Estate*.

Mhe. Spika, kuna mkutano ambao utafanyika mjini Siato Marekani na Zanzibar tumepata mwaliko huo. Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ajitahidi ende na jopo lake la wataalam katika mkutano huo kwani mkutano huo utawakutanisha wafanyabiashara zaidi ya 140; wafanyabiashara wakubwa ambao miongoni mwao wanahusika na

miradi hii ya ujenzi wa nyumba na makaazi ambaye huyu aliyetoa mialiko yeye ndiye Makamo wa Rais wa kampuni hiyo.

Mhe. Spika, naomba sana katika ziara hiyo basi wataalam wa masuala ya ujenzi lakini vile vile na wataalam wa masuala ya fedha basi washirikishwe, naamini katika ziara hiyo huenda tukapata mafanikio ya kutosha.

Mhe. Spika, pamoja na ukuaji katika mchango wa sekta katika uchumi wetu na huduma kuimarika kutoka asilimia 8.6 hadi 8.7 na ile ya kilimo imeshuka kutoka 2.7 hadi 1.3.

UKUAJI WA SEKTA YA VIWANDA

Samahani ninakuja katika sekta ya ukuaji wa viwanda. Pamoja na kuwa Mhe. Waziri ameeleza ukuaji wa viwanda asilimia 9.2 samahani Mhe. Spika, kidogo kuna *paragraph* zimeruka hapa, Mhe. Spika, suala hili ni kubwa na ni zuri lakini linahitaji mipango bora na usimamizi madhubuti kwani kuna miradi mikubwa sana ya kitaalamu na ushauri wangu ziara ya Makamo wa Pili wa Rais atakayopewa afuatane na wataalam wa Ardhi na Mipango Miji ili wakutano na wataalam wenzao wa kule wabadilishane mawazo, na naamini tunaweza kufanikisha na kufanikiwa katika hili.

Mhe. Spika, naamini tukiweza kufanikiwa hili la ujenzi wa nyumba za makaazi ninaamini mwaka 2015 tutaweza kupata kura bila ya matatizo yoyote kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, suala hili silisemi kwa utani, kwani leo ni mwananchi gani asiyependa kuwa na nyumba bora, mji mzuri anaoishi, uliojengwa na kupangika kitaalamu na huduma za maji, umeme zote zikiwa katika kiwango cha juu cha maakazi, kwani wananchi wetu wengi sehemu kubwa ya maisha yao wanaumiza vichwa pahala pa kukaa na chakula, pamoja na elimu. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali kulishughulikia suala hilo kwani dunia nzima hasa nchi zilizoendelea wananchi wao hupata makaazi yao kwa njia hii ya miradi ya "*Real Estate*" na jukumu la kuwapatia wananchi makazi ni suala la Serikali na kama malengo ya Mapinduzi yanavyosema na wenyewe waasisi wa Mapinduzi wa Nchi hii Mzee Abeid Amani Karume alianzisha mpango huu, lakini sisi tumeshindwa kuendeleleza wakati umefika hivi sasa wananchi wanahitaji makazi ya kisasa, na eneo hili nimelisemea sana kwani ni eneo muhimu kwa maisha ya wananchi wetu.

SEKTA YA NJE

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameelezea na kuonesha kasi ya kupanuka kwa urari wa biashara baina ya uagiziaji na usafirishaji wa bidhaa hadi kufikia 203.9 bilioni ya 2011, kasi inayonesha kukua kwa uwekezaji mkubwa wa bidhaa kulinganisha na usafirishaji, pengo hili litaendelea kukua kama hatutaweza kuwashawishi wawekezaji hasa katika uwekezaji wa viwanda ili na sisi tuweze kutengeneza bidhaa na kuuza nje. Vile vile, kuimarisha zao la karafuu na mwani na hata bidhaa za makombe ya pwani pamoja na majongoo tunaweza kuzisarifu hapa hapa Zanzibar na kuweza kuuza nje ya nchi.

Eneo jengine la kuongeza mapato ya nchi ni Serikati ya Mapinduzi Zanzibar kuweka mikakati ya makusudi ya ujenzi wa bandari ya kiuchumi ya Mpiga Duri, na kumalizia uwanja wa ndege ambao tayari kuna dalili za wamiliki wa kampuni ya Boing wameonyesha nia ya kuja kuwekeza katika *cargo terminal*, katika uwanja wa ndege na hao Mhe. Spika, naamini watakutana nao katika mkutano huu. Ikiwa tukiweza kuwashawishi na kuwawekea mazingira mazuri ya uwekezaji maeneo haya, nahisi kama Serikali yetu itayaweka mipango maalumu naamini ndani ya miaka miwili ijayo, miradi hii inaweza kuanza ujenzi sambamba na eneo linaloweza kubadilisha haraka sana pato la taifa na kukuza uchumi kwa haraka.

Mhe. Spika, lakini pia Serikali kuharakisha na kuandaa mazingira mazuri kwa rasilimali tulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu kwa kuanza utafiti wa kupatikana kwa gesi na mafuta pia linaweza likaongeza mapato ya Zanzibar. Lakini pia kuna dalili ya madini ya *Gypsum* kwa upande wa Pemba ambayo yanaweza kutumika kutengenezea saruji. Serikali pia tunaiomba kuongeza kujifunga mkaja katika utafiti wa maeneo hayo pia Mhe. Spika, ambapo kuna mtu, mzalendo, Mzanzibari, amejaribu kufanya utafiti wa upepo uliopo Zanzibar na amesema Zanzibar kuna upepo mkali sana ambao kama tutaweza kutafuta wawekezaji na kuzalisha umeme basi tunaweza kuzalisha kwa kiwango cha zaidi ya megawati 1000 ambapo tutaweza kumaliza tatizo la kuagiza umeme kutoka Tanzania Bara, na vile vile kuwa na umeme wetu wa uhakika na kwa kuwa matumizi yetu bado yapo chini ya megawati na kwa hiyo tutakuwa na bakaa ya umeme wa megawati 950 ambao tutaweza kuuza nje.

UTEKELEZAJI WA BAJETI

Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti mwaka 2013/14. Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti imeonekana jitihada za Mhe. Waziri kukemea vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma. Hata hivyo, bado jitihada zinahitajika kuongezwa na umakini katika usimamizi.

Mhe. Spika, mapato yetu tunayoyakushanya bado ni madogo, naamini yangeliongezeka kama Waziri angeliweza kutekeleza ushauri tunaoutoa na kuendelea kuutoa kwa Serikali kwa malipo yote ya kodi yalipwe kwa kupitia njia ya benki, hili bado Waziri labda akija aje atueleze sijui suala hili bado lina ugumu gani.

MISAADA YA KIBAJETI

Mhe. Spika, misaada ya kibajeti imeshuka kutoka asilimia 24.1 hadi asilimia 20.5 bilioni ikiwa ni upungufu wa asilimia 17%, hali hii imesababishwa na kukwama kwa sababu za kiutendaji kwa sehemu ya Zanzibar ya misaada inayopitia SMT.

Mhe. Spika, naomba sana serikali hasa kupitia Wizara ya Fedha basi kujitahidi kushughulikia kwa haraka lakini vile vile kuweka mkakati maalum kwa sababu si vyema kuona kwamba fedha zimekwama hasa kutokana na upande wa wenzetu, kama alivyoeleza Mhe. Waziri.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, hadi mwezi wa Machi 2013 kama alivyoeleza Mhe. Waziri deni la taifa limefikia Tsh.252 bilioni ambazo ni sawa na 18.6% pato la taifa sawa na ongezeko la 209 kufikia Machi 2012. Deni la ndani ni 40 milioni ambazo kama alivyoeleza Tsh. 3.1 ni za kiinua mgongo lakini vile vile kulipwa kwa wastaafu.

Mhe. Spika, tunaishukuru serikali yetu kwa kuendelea kulipa deni la kiinua mgongo lakini vile vile Mhe.Waziri kwa kuekezea muelekeo mpaka wale ambao wanategemea kustaafu na idadi ya fedha ambazo watakazoweza kulipwa. Tunaomba sana serikali yetu iendelee na jitihada zake ya kuweza kuwalipa kiinua mgongo watumishi wetu pale mara tu wanapomaliza muda wao wa kazi.

Mhe. Spika, suala la deni la taifa sio tatizo ikiwa fedha hizo zitakopwa kutoka kwa washirika wa maendeleo na zitatumika na kusimamiwa vizuri na kuona miradi mikubwa inakamilika kwa wakati kunategemewa kuwa ndiyo njia moja ya kupata mapato ya kuendesha nchi yetu lakini vile vile kuweza kurejesha mikopo hiyo.

Mhe. Spika, kwa hiyo tunataka Serikali ikope pesa kwa washirika wa maendeleo ili kujenga bandari yetu ya Mpiga Duri, na miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya watu ili wananchi waweze kupata faida. Deni hilo la la taifa lakini ikiwa deni la taifa limekuwa katika miradi inayojengwa lakini

ikiwa deni la taifa limekuwa na miradi inayojengwa kupitia deni hilo imekwama njiani kama ilivyoeleza hapo mwanzo miradi kama ya uwanja wa ndege na barabara za Pemba, deni hilo kwetu linakuwa ni mzigo wa makusudi na tunataka deni lenye faida na sio deni lenye hasara. Tunaamini Serikali yetu imekopa pesa nyingi ikiwa miradi hiyo itazalisha basi deni hilo litakuwa ni daraja la kwenda katika maendeleo na kuweza kulipa hilo deni. Mhe. Spika, kwa hivyo sisi tuko tayari kuwaruhusu wakope zaidi ili kuekeza katika miradi hiyo ya maendeleo.

PROGRAMU YA MIRADI YA MAENDELEO UTEKELEZAJI WA MKUZA 11

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri program 38 miradi 184 kupitia klasta 11. Mhe. Spika, bado kamati yangu inashauri kuangalia hizi program kuweza kuzipunguza ili kuweza kukamilisha miradi kwa wakati.

Mhe. Spika, katika klasta ya kwanza ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini na kuondoa umaskini mradi mmoja tu mkubwa ndio uliomalizika, mradi wa utengenezaji wa waya wa umeme uliothaminiwa na Wamarekani kupitia miradi ya *MCC* ambayo kama sio uzembe basi jengo kuu la kusafirishia abiria lingekuwa nalo limemalizika pamoja na zile barabara tano za Pemba zingekuwa mbali sana.

Kwa hivyo tunaitaka serikali kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa miradi hiyo ili kuleta maendeleo ya haraka. Lakini pia kamati yangu inashauri katika sekta hii ya klasta ya kwanza bado kamati yangu haijaridhika na kwa kuwa hadi leo tumeshindwa kujenga hoja za kupata fedha au wawekezaji wa kujenga bandari kubwa ya kiuchumi ya Mpiga Duri. Hapa ndio maana nikasema serikali tunataka sasa ianze mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba inatafuta fedha kwa njia yoyote ya halali ili kuweza kujenga bandari yetu ya Mpiga Duri ambayo tunategmea ndio itakuwa daraja ya maendeleo.

Mhe. Spika, hili tunaomba Mhe. Waziri aje atwambie ni wapi alipokwama hadi leo mradi mkubwa kama huu ulioasisiwa tangu awamu ya tano ya serikali hii hadi leo umetushinda. Ushauri wangu naomba hivi sasa kwa wale wawekezaji wanaokuja kwa nia ya kutusaidia tuwapo mradi mmoja tu mkubwa wa ujenzi wa bandari ya Mpiga Duri halafu tuangalie kama hawatoweza kutusaidia.

Mhe. Spika, serikali yetu kupitia Mhe. Waziri au tumeshindwa kutafuta mbia wa ujenzi wa bandari hiyo kwa njia ya P.P.P ili kuweza kujenga mradi huo ambao kukamilika kwake kutafungua lango la uchumi wa Zanzibar na bidhaa za viwanda na kuweza kutoa ajira nyingi. Pia nawaomba sana wachumi wetu

na wataalamu wa mipango wa SMZ waanze kushughulikia uekezaji wa sekta ya ujenzi kupitia miradi ya *Real Estate* kama nilivyoeleza hapo mwanzo.

Mhe. Spika, Klasta ya pili ni Huduma za Ustawi wa Jamii. Klasta hii ina miradi mingi karibu miradi 33, program 11 ambayo ilikabidhiwa 117.17 sawa 35% ya bajeti ya maendeleo 2012/2013 kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha zilizotolewa ni karibu 43% na SMZ lakini vile vile na wahisani karibu 42%.

Mhe. Spika, katika sekta hii tunashukuru sana serikali kwa kuweza kuboresha huduma za afya, huduma za afya na zaidi kwa utaratibu aliokuja nao sasa hivi wa kuweza kutoa zile *kits* katika hospitali hizi za kanda au hospitali za wilaya zetu.

Mhe. Spika, huduma za afya zinazidi kuimarika lakini bado inabidi tuongeze nguvu hasa kwenye sekta ya elimu kuanzia upatikanaji wa vitabu vya skuli za msingi, viti na meza zake na kumaliza majengo ya zamani, lakini vile vile na kuimarisha au kuanzisha majengo mapya, pamoja na kuweka vifaa vyote pamoja na vile vya maabara sio tu lakini inabidi Wizara ya Elimu ibadilishe mitaala yake, na kipaumbele kwa sasa kiwe kwa skuli za ufundi stadi ili kuandaa mafundi na wataalamu kwani mpango wetu tuliokuwa nao hivi sasa tunaandaa vibarua wengi na sio wafanyakazi.

Kwa hivyo kuimarisha mitaala ya elimu ya Vyuo vya Ufundi tunaweza kuimarisha na kuweza kutoa mafundi, lakini vile vile hata kama wakija wawekezaji kama hatujaimarisha hii sekta ya ufundi tunaweza tukakosa wataalam na ajira zote za kitaalam zitachukuliwa na wageni. Kwa hivyo matokeo yake vijana wataendelea kulalamika kama kazi hawapati na zinachukuliwa na wageni. Kwa hivyo kuimarisha vyuo vya ufundi na kuanzisha mitaala maalum ya somo la *Information Technology* kwani tumegundua katika ziara yetu nchini China taaluma ya *Information Technology* imetoa ajira nyingi sana ya moja kwa moja kwa vijana na bila kutegemea kuajriwa katika Serikali au kuajiriwa na makampuni. Vijana wengi wamekuwa wakijitegemea wenyewe kwa kutumia taaluma ya *Information Technology*. Mhe. Spika, ndio maana hivi sasa bidhaa nyingi tumekuwa tukizipata katika nchi za Afrika kutoka China na kuna baadhi yao basi vingi vinatengenezwa katika viwanda ambavyo viko majumbani.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza pia kwamba Zanzibar kuna dalili za upatikanaji wa nishati na madini kama vile *gypsum*, pamoja na gesi na mafuta na umeme wa upepo, basi ni vyema tukawaandaa vijana wetu katika fani hizo zote pamoja na kuwa tayari tumeshachelewa lakini waswahili wanasema kawia ufike. Kwa hivyo itakapokuja bajeti ya Wizara ya Elimu Mhe. Spika,

tunaomba kwamba wajitahidi kujikita zaidi katika programu za kusomesha elimu za ufundi na utaalam katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, tatizo jengine ni suala la maji. Maji ni miongoni mwa huduma muhimu kwa maisha ya kila siku na kwa viumbe wote wakiwemo wanadamu, mimea pamoja na wanyama. Serikali imekuwa ikihangaika kwa wahisani na marafiki mbali mbali kuomba misaada na fedha nyingi na fedha nyingi zimeshatumika hasa katika mkoa wa Mjini/Magharibi, ingawa Waziri mdio mwenye dhamana ya maji amesema mkoa huu unapata maji kwa asilimia 80 jambo ambalo mimi sikubaliani nalo. Bado suala la maji ni tatizo sugu na inaonesha bado hayana mipango endelevu ya Serikali kuweza kukamilisha suala hili. Serikali ya Japan iliweza kujenga mradi wa maji mkoa wa Mjini/Magharibi na tuliahidiwa baada ya kumaliza mradi tatizo la maji lingeweza kumalizika.

Baadae tukaambiwa miundo mbinu ya paipu imekuwa ni ya zamani na maji mengi yanapotea. Tulitegemea awamu iliyofuata tungeliona ubadilshaji wa paipu na kuweka laini mpya, lakini matokeo yake bado tunaambiwa kuwa mradi mwengine umetengewa fedha nyingi na tunategemea kuziidhinisha zaidi ya karibu 55 bilioni kwa uchimbaji wa visima vyengine, je lile suala la miundombinu ya kusambazia maji ikiwemo paipu na mabomba umeishia wapi. Lakini pia mwaka 2011 aliyekuwa Waziri wa Maji aliomba fedha na kuahidi angelichimba visima vyengine karibu 56 lakini hatukuona visima hivyo bado tatizo liko pale pale.

Kama alivyoeleza Mhe. Waziri na kuomba klasta hii imetekeleza program sita na miradi 26 katika ya bajeti ya maendeleo Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imejitahidi katika klasta ya pili. Mhe. Spika, katika suala zima la suala la miradi ya maji kama nilivyosema huduma za jamii afya tunaridhika lakini bado kwenye sekta ya afya waziri anayehusika aje atupe taarifa ya kutosha.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza katika klasta ya tatu ya utawala bora ametekeleza programu nyingi lakini vile vile serikali imejitahidi kuimarisha utawala bora na katika suala la utawala bora ndio unaoimarisha amani na utulivu. Kwa hivyo ninaishauri kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 tuelekeze zaidi nguvu zetu katika kuboresha daftari la kudumu la kupiga kura na kuhakikisha kila anayeishi Zanzibar awe na kitambulisho aidha cha Mzanzibari au Mtanzania ili kuweza kulinda na kudhibiti usalama wa nchi yetu. Pia kupitia Tume ya Uchaguzi waandae program maalum ya mafunzo ya elimu ya uraia ili wananchi wetu wajue haki zao na umuhimu wa kufuata sheria za nchi, ili kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani hasa kuelekea kipindi kijacho ambacho nchi yetu itapita katika kipindi kigumu cha

uboreshaji wa daftari la kudumu, Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, Bunge la Katiba la SMT, kura ya maoni ya katiba mpya ya SMT na hatimae uchaguzi mkuu wa 2015.

Kwa hivyo ndani ya miaka miwili na nusu ijayo nchi yetu itapita katika kipindi kigumu sana cha mabadiliko makubwa ya mfumo ya utawala wa nchi yetu pamoja na uchaguzi mkuu. Kwa hivyo bado tunaitaka SMZ kuendelea kutenga fedha nyingi kwenye klasta hii ya utawala bora ili kuhakikisha kwamba muda wote elimu inatolewa kupitia makongamano na kupitia vyombo vya habari mbali mbali ili wananchi waweze kuelewa na kufanya maamuzi sahihi wao wenyewe bila ya kubururwa na watu wengine.

UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE 2012/2013

Mhe. Spika,utekelezaji wa vipaumbele kwa mwaka uliopita SMZ iliweka vipaumbele vyake kuimarisha huduma ya afya ajira ya vijana, ustawi wa wazee, elimu ya lazima, kuimarisha uchumi na kuimarisha mashirikiano ya sekta binafsi na kwa pamoja Waziri kueleza kuwa maelezo zaidi yatatolewa na Mawaziri husika kwenye bajeti zao, na ninaamini huku katika sekta husika tutachangia vya kutosha na tutashauri vya kutosha lakini bado katika eneo la ajira kwa vijana inabidi Waziri uje kutupa maelezo utapokuja kusimama hapa, kwa sababu mwaka uliopita tulishauri Wizara yako ya Fedha na Uchumi kutenga fedha katika bajeti kuu ya serikali ili kuanzisha Benki ya Maendeleo ya akinamama pamoja na vijana kitu ambacho nadhani ndio pekee kitakachoweza kuwakomboa vijana na akinamama katika kukuza mitaji yao na kuimarisha biashara zao ndogo ndogo kupitia mikopo na misaada mbali mbali.

Lakini humu kwenye mipango yenu Serikali tusitegemee kupitia mifuko inayokopesha vijana na akinamama kuwa utawatoa kwani hata wenzetu Bara walitumia mifuko ili kutoa mikopo kwa akinamama na vijana hawakufika pahala pazuri. Lakini leo baada ya kuanzisha Benki ya Akinamama imeweza kuwahudumia akinamama wengi na wameanzisha biashara kubwa na wengine wanamiliki maduka makubwa ya nguo na viwanda vya kusaga na kukoboa mazao na wengine wanasafiri nje ya mipaka ya nchi kuimarisha biashara zao. Kwa hivyo bado tunaishauri Serikali yetu kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana na akinamama, hii itakuwa mkombozi wa kuweza kuwakomboa vijana wetu katika kuimarisha katika biashara zao.

Mhe. Spika, sensa ya watu ya idadi ya makaazi Zanzibar kama alivyoeleza Mhe. Waziri tumefika 1,303,569 na T.bara 44,928,923. Kwa hivyo sasa Watanzania tupo zaidi ya 46 mil. na sehemu kubwa hao ni vijana na akinamama. Kwa hivyo iko haja ya kuwa na mipango madhubuti na endelevu

ya kuwashughulikia mahitaji yao ili waweze kujitegemea kwani hivi karibuni hata nchi za ulaya kumejitokeza vuguvugu kubwa la maandamano ya vijana hasa katika nchi za Ugiriki na nchi zilizopakana nazo kwa ajili ya vijana kudai ajira ndani serikali yao na ukosefu mkubwa wa ajira sasa hivi duniani. Kwa hivyo tukiweza kuanzisha hizi benki na sisi itaweza kutupunguzia tatizo hili.

VIPAUMBELE 2013/2014

Mhe. Spika, Serikali vile vile imeweka vipaumbele katika miradi ya maji kama nilivyoeleza imetengewa bilioni 55.4, Elimu 32.8, Afya 23.1, Ajira 1.1. Kwa mgawanyo huo katika fungu la maendeleo la bilioni 305.4 ambao ni sawa na asilimia 100% ya bajeti yote ya maendeleo vipaumbele vimetengewa 113.3 bilioni. Kwa hivyo inaonesha dhahiri kweli ni bajeti ya huduma ya jamii. Kamati yangu inaishauri Serikali tusiweke vipaumbele kwa maneno tu bali tutekekeze kwa vitendo pamoja kwamba tunaridhia kupitisha fungu hili la miradi ya maendeleo, lakini bado hatujaridhika na utekelezaji wa miradi ya maji hasa kama nilivyoeleza hasa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ambapo Serikali kama nilivyoeleza mwanzo kwamba inadai karibu 80% kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi maji yanapatikana.

Mhe. Spika, utekelezaji wa dira ya 2020 na Mkuza 2 pamoja na Programu tano

(a) Mageuzi ya Kiuchumi – umelenga kuinua utalii, biashara, viwanda na kilimo katika sekta hii. Kamati yangu inashauri kwamba kukamilika kwa *master plan* ya maeneo huru ya kiuchumi ya Fumba na Micheweni na kuiwekea miundombinu ili kuweza kuwavutia hao wawekezaji, kwani nchi yetu haina ardhi kubwa ya kutosha na ni uwekezaji pekee hasa katika sekta ya viwanda ndio itakayoweza kuleta mageuzi ya kiuchumi hapa Zanzibar.

(b) Mageuzi ya Serikali – Utawala Bora, Uwajibikaji, utoaji wa huduma bora na kupambana na rushwa, eneo hili bado linahitaji mkazo mkubwa kwani bado vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma vinaendelea na bado jitihada za Serikali kupambana na jambo hilo haziridhishi.

(c) Rasilimali Watu – katika eneo hili pamoja na jitihada ya Serikali kuboresha huduma za Afya na Elimu, nadhani kwa sasa iko haja ya kuweka kipaumbele kwa elimu na kuandaa mtaala mpya ambao utawandaa wanafunzi wetu kuwa wajasiriamali mara tu baada ya kumaliza skuli kwani mfumo tuliokuwa nao unaandaa vibarua zaidi kuliko wafanyakazi na katika eneo hili iko haja kuimarisha na kuviongeza vyuo vya amali pamoja na kusomesha walimu wa kutosha ili kuandaa wanafunzi kujitegemea baada ya kumaliza skuli. Lakini kama nilivyoeleza hapo mwanzo kuandaa mitaala somo la

"Information Tecnology" ambalo litaweza kutoa ajira kama nilivyoeleza mwanzo.

(d) Mabadiliko ya Tabia ya Nchi – Serikali bado iendelee kuweka mkazo katika kuhifadhi mazingira kwani maeneo mengi hivi sasa Zanzibar kuna uharibifu mkubwa wa mazingira lakini pia kuna miradi mingi ya maendeleo ambayo inafanywa na wahisani, miradi ambayo iko chini ya serikali lakini inafanywa bila ya kufanyiwa tathimi ya mazingira jambo ambalo linachangia uharibifu mkubwa wa mazingira.

(e) Visaidizi vya kuongeza ujuzi na kuendeleza sekta binafsi – eneo hili bado halijafanyiwa kazi ya kutosha kwani Serikali imeandaa sera ya PPP lakini bado ushirikishwaji wa sekta binafsi sijauona ushirikishwaji wake kiasi kikubwa katika sekta hii. Kwa hivyo tunamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha ajaribu kuwa karibu na wafanyabiashara na ninaomba Waziri wa Fedha katika hii ziara ambayo amealikwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naamini na yeye ataambatana nae basi ni vizuri akawashirikishana wafanyabiashara ili wakakutane na wafanyabiashara wenzao wakubwa ambao wanaweza wakaja kusaidia katika kushirikiana na uwekezaji katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Bajeti ya mwaka 2013- 2014 ya bilioni 658.5 ambapo 333.7 mapato ya ndani – 338.7 misaada na mikopo. Mapato halisi ni 616.6 bilioni kwa hiyo nakisi ya 41.9 inabidi wananchi kuichangia kwa hiyo Serikali kutokana na kutokuwa na vianzio vipya imebidi kuongeza kodi mbali mbali ili kuweza kujazia hilo pengo, hali hii itaendelea kuwapa mzigo wananchi wetu kwani kipato wanachokipata ni kidogo, kwa hiyo ni lazima tuandae mikakati mipya ya kutafuta vianzio vipya vya mapato ili kupunguza kuwakamua wananchi.

Mhe. Spika, Serikali imetenga bilioni 17.5 kwa ajili ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi pamoja na kuandaa ajira mpya kwa mwaka ujao wa fedha wa 2013/14. Mhe. Spika, hapa kwanza nataka nitoe shukurani zangu za dhati, kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza ahadi yake ya kuwaajiri vijana zaidi ya 2000 katika mwaka uliopita, wananchi wengi wamefurahi na kutokana na kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha hapa fedha nyengine zilizotengwa naamini kuna ajira ambazo zitaweza vile vile kujitokeza katika mwaka ujao. Kwa hivyo tunawaomba vijana wetu wasome sana kwa sababu ya sheria ya utumishi wa umma sasa hivi bila ya elimu basi huna ajira.

Mhe. Spika, Waziri amekuja na mapendekezo ya kupandisha kodi mbali mbali ili kuongeza mapato, ametoa mfano wa marekebisho mbalimbali ya Sheria ya *VAT* na amekiri kwamba kuna baadhi ya watendaji wachache

wanaendelea kudanganya kwa kutaja kima kidogo cha kutozea kodi kwa mahoteli jambo ambalo limekuwa sugu katika kupunguza mapato ya Serikali, sasa hapa mimi bado ninashauri Serikali iwe tayari kutekeza malengo yake vyenginevyo tutaendelea kubadilisha Sheria zote lakini kama bado watu hawajakubali kubadilika na kuwacha udokozi wa mali ya umma na rushwa basi tutaendelea na hali ile ile kwani tunazo sheria nyingi nzuri lakini muhali unaongoza kwenye sheria kuliko kufuata sheria zenyewe kwa kutoa visingizio kwamba sote ni wamoja lakini waswahili wanasema ”Mchelea mwana hakulia basi atalia yeye”.

Mhe. Spika, pia katika marekebisho ya sheria ya misamaha ya kodi iliyokuwa ikitolewa kwa baadhi ya taasisi kutoka 100% - 80% tunaomba kwa upande wa misaada au kwa upande ya misamaha tunayoipata kupitia Kamati zetu za maendeleo za majimbo iendelee kupatiwa misamaha ya asilimia 100% kwani miradi hii hatufanyi kazi kwa biashara lakini tunafanya kazi kwa huduma za jamii. Na hapa Mhe. Spika, nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kwa kuweza kutoa msamaha kwa vifaa ambavyo wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuweza kutusaidia vifaa vya hospitali na hatukuweza kutoa hata shilingi, tunaamini hatukutoa fedha lakini tumechangia vile vile katika kuboresha huduma za jamii. Mhe. Waziri wa Fedha nakushukuru kwa hilo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Spika, Serikali katika kuweka viwango vya kodi ya *VAT* kwa baadhi ya mahoteli inabidi *ZIPA* pamoja na *ZRB* ifanye kazi ya ziada kuzikagua hoteli zote za kitalii na kuona ujenzi wao hasa zinazomilikiwa na wageni kama zinakidhi vigezo vya uwekezaji, uwekezaji kwa wageni kwani kumekuwa na baadhi ya wawekezaji kwenye mahoteli wanachukua maeneo makubwa lakini ujenzi wao haulingani na matakwa ya sheria jambo ambalo wanajenga vibanda vingi badala ya kujenga majengo ya ghorofa ambayo yatachukua sehemu ndogo lakini yenye vyumba vingi.

Mhe. Spika, tunaishukuru Serikali kwa kupunguza ushuru wa stempu kwa bidhaa za mchele na unga wa ngano kutoka 3% hadi 2%, hii itasaidia kupunguza mfumko wa bei. Hapa tunaomba wafanyabishara kuthamini mchango wa Serikali huu kwani hiyo pia waliosamehewa pia ni kodi ya wananchi. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaomba sana wafanyabiashara wetu wajaribu kuangalia punguzo wanalolipata na wao kuwapunguzia makali katika bei hasa wananchi wanapokwenda kununua bidhaa.

Mhe. Spika, suala la magendo ya mafuta bado linakuwa suala sugu lakini bado mimi ninaamini hii ni biashara ambayo inahusisha sio watu wadogo watu wakubwa katika magendo haya, mara nyingi wanafanya katika meli

ambazo zinapitia baharini hasa kutokea Mombasa. Kwa hivyo Mhe. Spika, tuna vyombo vingi vya ulinzi na usalama, baharini na nchi kavu lakini inashangaza bado kuna watu waliopewa dhamana ya kusimamia masuala haya lakini bado tatizo la magendo ya mafuta linakuwa liko pale pale.

Mhe. Spika, tunashukuru jitihada za Mhe. Waziri la kupambana magendo haya tumeweza kumsikia kukamata mapipa ya mafuta lakini vile vile na kuweza kuyafilisi. Mhe. Spika, tunaomba Mhe. Waziri aendelee na mkakati wake huu kwa sababu kama ulivyosema kwamba tukiendelea kuoneana haya na kusema kwamba sisi ni Wazanzibari ni wamoja basi hatuwezi kufika mahala.

Mhe. Spika,Waziri pia amezungumzia katika zoezi la kuondoa tatizo la magendo na upungufu wa mara kwa mara wa mafuta kwa kuruhusu utaratibu wa mungizaji mmoja tu *(single importer)* kama ilivyokuwa kabla.

Mhe. Spika, hapa ndio kwenye tatizo letu la watu wa Zanzibar, hatufanyi mambo kwa utafiti na hatuna mipango endelevu ya kiuchumi kwa Baraza lako tukufu tulizungumza sana wakati tulipobadilisha sheria ya kuondoa mmilikaji mmoja wa mafuta wa Kampuni ya *ECOTEC* na alipoeleza athari zake kuruhusu kila mtu alete mafuta ndio matokezeo yake ndio tunayaona hivi sasa magendo yamekuwa mengi ya mafuta na kodi ya Serikali inapotea sana. Lakini leo tunarudi kule kule naomba tuzitafute, ninamuomba sana Mhe. Waziri, kampuni zenye uwezo wa kazi hii na kwa masharti maalum kwamba wao wayalete tu mafuta nchini yasiruhusiwe kuuzwa reja reja katika vituo vyao, kama ilivyo hivi kwamba kuna watu wanaleta mafuta na vile vile na wao wanauza reja reja ili kuweka usawa katika biashara.

Mhe. Spika, katika uimarishaji wa vianzio vya mapato serikali imeandaa utaratiba wa kutathimini ada za ardhi lakini pia ni muhimu kuangalia wawekezaji waliochukua maeneo makubwa lakini hayalingani na uwekezaji wao wakati umefika kuwataka wawekezaji hasa wa mahoteli kujenga majengo ya ghorofa ili kuchukua maeneo madogo, lakini leo ardhi yetu imejaa maeneo mahoteli lakini bado idadi ya vyumba ni ndogo sana ambapo kama Zanzibar itakuwa na mkutano mkubwa basi wageni watakosa mahali pa kukaa. Nadhani wakati umefika kuangalia *value for money* na tuende zaidi *(area per cash*) eneo hili wachumi wetu kama mtalifanyia kazi basi ardhi yetu itaongezeka kuendela juu badala ya kutawanyika. Mhe. Spika, na mapato vile vile yatangezeka maradufu.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti muda umechukua mkubwa sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Namalizia Mhe. Spika, hivi sasa tunahitaji majengo yenye ghorofa 30 hadi 50 kutokana na maumbile ya visiwa vyetu, mimi nasema kwa pamoja tukishirikiana haya yote yanawezekana. Nadhani tuutumie utajiri wa ardhi yetu ndogo kwa mambo makubwa kwani visiwa vyetu vinajiuza vyenyewe kwa uzuri wake.

Mhe. Spika, kama ulivyoelezea kabla ya kumalizia hotuba yangu hii nitaomba nichukue kama dadika 3 Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi kwa maeneo yafutayo.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka huu tunategemea ongezeko la mabadiliko hasa kupitia kodi mbali mbali lakini bado Mhe. Waziri hajatueleza mapato mengine ambayo ni mapato ya muungano.

Mhe. Spika, bado kuna eneo hili bado halijafutwa katika Katiba katika eneo la gesi, sasa hivi kuna vitalu vya gesi ambavyo vimeanza kukodishwa sisi Zanzibar bado Mhe. Waziri hajatuambia tunapata nini, lakini vile vile katika eneo jengine Mhe. Spika, kumetangazwa kadi za simu ambayo hata katika bajeti ya mwaka jana nilieleza, wenzetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuna ada katika *airtime* itaongezwa ambayo inategemewa kuongeza mapato makubwa ambapo na sisi Wazanzibari vile vile tunatumia hiyo *airtime*, bado eneo hili sijui Mhe. Waziri atatueleza nini. Sasa nilikuwa nichambue kodi moja moja katika maeneo ya anga na sehemu nyengine lakini kwa kuwa Mhe. Waziri, yale mapato ambayo yamo ndani ya Jamhuri ya Muungano ambayo Zanzibar tunastahili kupata aje anieleze kwa nini mapato haya hayakuingizwa katika bajeti hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo nataka niseme kwamba nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe waipitie hotuba hii na waichambue na waishauri vizuri Serikali yetu, lakini kikubwa zaidi tuishauri kuanzisha vianzio vipya vya mapato ili bajeti ya mwakani ije kupunguza hii kodi ya kuwakamua wananchi. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi ya leo hii kuwa ni mtu wa kwanza kutia baraka katika bajeti hii kubwa ya Waziri wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango na Maendeleo ya Zanzibar ambayo Mhe. Waziri Omar Yussuf nimshukuru sana, Makatibu, Manaibu Makatibu na watendaji wake na wataalamu. lakini zaidi nitoe shukurani za pekee kwa mwalimu wangu wa jana ambaye ni Dr. Jidawi alizidi kunipa ushauri ili kuweza kuchakachua zaidi ile ripoti yake aliyotuletea.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchambua kitabu hiki, nianze kuingia na ukurasa wa pili hasa pale inaposemekana kuwa kifungu kinachoeleza kuhusu kuwa leo tunakutana tena kuzungumzia mipango muhimu ya maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar na tunashukuru kwa Mwenyezi Mungu kutokana na hali hii kutupa uhai lakini kuna kifungu ambacho kinajieleza hivi, nasema namuomba atujaalie hekma katika kuendesha kikao hichi muhimu na tumalize kikao tukiwa tunatumia vyema kwa busara wananchi wenzetu tunaowakilisha majimboni mwetu.

Mhe. Spika, hapa leo tunapitisha bajeti na bajeti hii kuu ina mambo mengi sana na hasa tukieleza masuala ya uchumi. Mimi nakubaliana nae kuwa uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia kama inavyoeleza kitabu, hilo mimi sina tatizo nalo, tunalikubali kwa nguvu zote. Na sababu ninazo Mhe. Spika, za kuonesha ni kiasi gani uchumi wetu umekua kwa hatua kubwa sana.

Mhe. Spika, mwanzo mimi nilikuwa napata shida ya kufahamu ya kuambiwa uchumi wetu umekua, nilikuwa sijui unakuwa vipi, ingekuwa na mifano ya kukua kwa binadamu tu kwa kila siku umri unakuwa nilikuwa nikifikiria hivyo. Lakini kukua uchumi wetu katika maendeleo ambayo tunayaletewa katika kisiwa chetu cha Zanzibar siku hadi siku au mwaka hadi mwaka, nimekiri na hasa katika sehemu chache ambazo tofauti.

Mhe. Spika, tulikuwa na malaria mengi, sasa imepungua ni moja katika sera ya uchumi, Mhe. Spika, tulikuwa na barabara zetu mbovu sana na sasa hivi barabara zetu ni nzuri *quality*. Mhe. Spika, ulikuwa ukitaka kwenda sehemu nyengine sharti uzunguke sehemu nyengine ili ufike, lakini leo Mhe. Spika, unakata *shortcut* tu unafika sehemu ambayo unayoikusudia bila ya usumbufu na unakwenda kwa wakati. Mhe. Spika, hayo ni moja katika maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, jengine sasa hivi juzi tu Waziri anatuambia kwamba ana uwezo wa kuajiri watu, ni moja katika eneo la kuonesha kwamba sasa uchumi wetu umekua kwa sababu mara nyingi sana bajeti nyingi tumezipitisha sijasikia kifua mbele Mhe. Waziri kusema sasa anaajiri watu, lakini leo anatusomea kitabu chake kuwa ana uwezo wa kuajiri watu, ana uwezo wa kuwaongeza watu mishahara, ana uwezo kulipa watu fedha za kiinua mgongo kwa waliostaafu. Ameyasema hayo na sisi ni mashahidi nimuombee Mungu tu ayatekeleze kama alivyoyaeleza katika kitabu chake hiki na inshaallah Mwenyezi Mungu atampa kauli thabiti hiyo ya kuweza kutekeleza kwa kupitia kwa watu wake.

Mhe. Spika, sasa kwa kuendeleza zaidi na kuthibitisha na kuonesha dhahiri kwa makusudi kuwa ni kweli mambo haya ya kweli na hasa alivyozungumzia

masuala ya kuwa tuna asilimia sasa hivi ya viwanda, hilo sina tatizo nalo. Mheshimiwa katika *research* yangu nimejaribu kuangalia mambo ya viwanda ambavyo vinatuingizia mapato zaidi ya kutosha, kama viwanda vya kokoto, tumeangalia sana sasa hivi vimekuwa viwanda hivyo vingi na tukisema leo tuvifunge basi angalia uchumi wetu utakavyokwenda chini kabisa. Lakini hili naomba sana Mhe. Waziri azidi kuleta mashine za kisasa ili wananchi baadae mwaka wa kesho bajeti nyengine iwe na matumaini mazuri zaidi.

Mhe. Spika, masuala mengine ambayo nimeyagundua uchimbaji wa mchanga, lakini ninachoomba watu wanaochimba mchanga ninawaomba sana tujali na mazingira tuwaelimisha watu wetu vizuri wakisha kuchimba mchanga wao waweze kupanda miti ambayo italeta rutba ili kuleta ardhi ile kuja juu zaidi kwa haraka sana.

Mhe. Spika, naomba kumshauri Waziri wangu na kuweza kumsaidia kwa sababu binadamu yeyote kila mtu ana fikra zake na mawazo yake, utaangalia kitabu hiki kimekuwa na wataalamu chungu mzima, jana tumepewa semina na maprofesa wengine madokta wengi tu, lakini sasa kuna mambo ambayo hata na sisi ambao si maprofesa kuna mambo ambayo tunayaona yatakayomsaidia Mheshimiwa wetu Waziri mpendwa kabisa ili aweze kutuletea uchumi zaidi katika bajeti ya kesho. Nakuja katika sehemu ya utalii.

Mhe. Spika, nakuja katike sehemu ya utalii bado hatujasema kama hiyo ni mkombozi wa uchumi wa Zanzibar hatujatamka neno hilo. Mapato bado yanavuja hatujaweza kuyadhibiti mpaka sasa hivi. Watalii wanamiminika katika kisiwa cha Zanzibar lakini idadi ambayo iliyokuwa *cream* kabisa kuweza kuipata sisi tukaweza tukajua pato letu likoje tunakuwa tunashindwa kupata, lakini ukenda kwenye mahoteli wanakwambia kuna watu *full up* ambapo 300 wameingia au 500 wameingia lakini ukenda kwenye mapato yanakuwa kidogo sana ni jambo moja ambalo linasikitisha na sasa hivi utalii umeshamiri na kuna njia moja ambayo ninamwambia Mhe. Waziri hasa katika masuala haya, hebu tujaribu kidogo tuangalie hii kodi kidogo ya utalii kwa sababu sasa hivi kuna *challenge* wenzetu wa Kenya wako juu, Uganda, Zimbabwe wako juu ile nayo *visa* au *payment* ya kuingia pale inawekwa *standard* kidogo na sisi tuangalie mazingira hayo ni bora tupate kidogo kidogo lakini kiwe kingi kuliko kupata kingi tukakosa *market* hapa Zanzibar na hali halisi kama unavyoijua, kisiwa hiki ni tajiri tena sana tu si kisiwa ambacho cha kuwa masikini kama tutakuwa tumesimamia vizuri.

Mhe. Spika, kwa kuendelea sasa hivi ipo haja nchi yetu ya kuongeza mapato kwa kupitia njia ya viwanda vikubwa, uwezo huo upo na inawekezana. Zanzibar sasa hivi wakati wowote Mhe. Waziri, wewe utakuwa ni shahidi tukawa na chelezo chetu cha Zanzibar ambacho chenye *standard* badala ya

kupeleka Kenya, sasa tukawa na chelezo chetu hapa Zanzibar. Nikushukuru sana Mhe. Waziri ulijitahidi sana katika bajeti iliyopita lakini mpaka leo bado wale watu hawajapa *go ahead* ya kuweza kufanikisha suala lile, ninaomba sana tia mguu wako tena ili kiwezekane kile ili kuweza kufanikisha uchumi wetu kukua. Mhe. Spika, yote hayo katika kitabu chako hakipo sasa mimi ninakupa, hilo moja ambalo tutaweza kusaidia uchumi wetu.

Mhe. Spika, chelezo hicho kwa sababu sasa hivi kama unavyojua tu tunacho chelezo hapa lakini hakiko *standard* cha bandari, kipo chelezo lakini tokea wakati huo mimi sijazaliwa na sasa hivi vyelezo vya kisasa vinatakiwa viwe *standard* na viweze nchi zetu za majirani na wao waweze kuja kuekeza kupandisha boti kwa kufanyiwa matengenezo madogo madogo, lakini vile vile niseme sasa hivi Zanzibar pamoja na kutamka milango wazi wakaja kuekeza lakini kauli zetu Mhe. Spika, hazina ukweli, nasema sababu gani.

Mhe. Spika, kwa mfano sasa hivi kwa kweli Mhe. Waziri anajitahidi sana lakini labda kuna mambo yanatukwaza sisi watu wa Baraza tumsaidieni, na ndio maana tukawa tunafanya semina. Semina inakuelemisha na kuelimishwa, sisi juzi tumeelimishwa lakini tumeelimisha, japo wengine wanakwambia ah! Mshimba porojo, sijui hivi kumbe porojo ile kwa sababu unai-*challenge paper* yake na ukii-*challenge* mtu *paper* yake kila jina utapewa. Namsitiri Katibu mmoja alisema neno hilo, lakini ah! mimi hicho ni chakula changu, kwangu mimi ni mbolea tu.

Mhe. Spika, tuna mradi ambao siku zote huwa tunausema mradi wa umeme wa takataka, kampuni yake inaitwa Seprona. Mhe. Spika, nilisema sana, usingoje ukasifiwa lakini wewe lazima ujisifu mwenyewe hilo tuliseme, kwa sababu utaposema jambo zuri binadamu wenzako hawalifurahikii. Mhe. Spika, nimekwenda Marekani kuangalia mradi huu (*Makofi*).

Mhe. Spika, wenzentu wa Marekani hakuna asiyejua wao ndio baba wa ulimwengu, hata wakaukubali mradi huu wa takataka kuleta umeme na wakautumia Pentagon. Mheshimiwa mradi wa umeme wa takataka unatumiwa kwenye Pentagon, nani asiyejua kwamba Pentagon ni sehemu ambayo ni ya siri na muhimu sana umeme wake unatakiwa. Lakini jitihada za Mhe. Waziri atanielezea kafikia wapi hata leo mradi usiweze kufanya kazi yake, atanieleza Mheshimiwa Waziri wa Majenzi hayupo hapa, kitu gani kilichokwama. Lakini zaidi ya yeye kwamba yeye ni msimamizi mkuu wa miradi mikuu atanieleza tunakwenda wapi jamani, tungelikuwa tuna mabilioni ya fedha sasa hivi hapa, tunajinasibu hapa kabisa. sasa hizi ndio kasoro ya Serikali tunaomba tuwaambie ili iweze kutusaidia katika masuala haya.

Mheshimiwa mradi huo namuomba sana Mheshimiwa Waziri aje anieleze aniambie kwamba sasa wakati wowote mradi huu Zanzibar utaanza kazi yake. Na kuwaokoa wananchi kupata bei kubwa ya umeme ambayo tunakwenda nayo faida moja hiyo, lakini faida ya pili takataka zitaondoka katika kisiwa chetu hiki, uchafu wote utaondoka, maradhi yatapungua ukiwekwa mradi huu, naomba sana Mhe. Waziri aje anipe utamu wa maneno kuhusu mradi huu umefikia wapi. lakini vile vile anionyeshe jitihada ya Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi jinsi gani ya kuwapelekea wananchi maendeleo yao.

Mhe. Spika, katika suala la kilimo, naweza kusema kwamba hivi sasa wakati wowote Mheshimiwa watu wa Kitope watu wa Kilombero watafaidika katika mpunga wa kumwagilia maji. Mhe. Spika, *project* hiyo niliisema sana hapa, kwa hivyo nashukuru sana mradi huo umeshaanza wakati wowote visima vitachimbwa na maendeleo yataweza kupatikana, ni moja katika kukua katika kitabu hiki cha mheshimiwa wangu alivyoeleza.

Mhe. Spika, suala la mafuta. Tulipokuwa katika Kamati yangu ya Mawasiliano na Uchukuzi tuliandaa *committee* nzuri tu lakini tulikosa fedha za kuweza kufanikisha lengo lile, tulikuchukulia *example* kama harambee ya ya kuokoa zao karafuu, lakini sisi tulikosa fedha, naomba sana Mhe. Waziri, Kamati ile kama itafika kule Pemba na tumeshafanya mahesabu ya mafuta naomba sana mheshimiwa peleka hesabu ile ili uokoe mabilioni ya magendo ya mafuta. Mheshimiwa toa mali upate mali ukisema umeng'ang'ania tu mali hupati kitu utazunguka kila siku hapa.

Mhe. Spika, naomba niende katika sheria ya *ZIPA*. Mhe. Spika, naifurahia sana sheria hii ya *ZIPA*. Mhe. Spika, *ZIPA* wapewe fursa kubwa ndio wataweza kutuletea utajiri hivi sasa, wacha *ZRB*, *ZRB* ni *final* tunasema wao wamemaliza, lakini kuna sheria zinanikwaza *for example* leo hoteli ya *VENTA* wallahi cha kusikitisha pale ukenda utafikiria kama *half London*, lakini leo katizame utasema kama msitu wa Serengeti, hakuna kilichokuwepo laiti ingelikuwa *ZIPA* wanayo sheria Mhe. Spika, hoteli ile wala isingefilisika kiasi kile wananchi wetu wangepata kuendesha huduma zao kama walivyokuwa wakipeleka pale wakiuza vitu, lakini mpaka leo fedha zao walizokuwa wakiuza vitu hawajalipwa wanahangaika wanapelekwa Mahakamani, hoteli ile sasa hivi msitu mtupu, watu wameshaiba vitu, kwa sababu nini sheria ya *ZIPA* bado mmeibana, mpeni kijana yule Mkurugenzi afanye kazi vizuri, tusimuingilie wala tusimbane, tumpe uhuru wa kuangalia miradi ambayo itaweza kuondoa umasikini Zanzibar tumpe fursa afanye hivyo. Mhe. Spika, naomba sheria hiyo iangaliwe.

Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri angalie uwezekano wa kodi ambazo sio nyingi *please*; kodi hizi zilikuwa nyingi sana zinashindwa hata wale wafanyabiashara, kuna siku wameongeza bei kutokana na kodi zimekuwa nyingi jamani hebu wekeni mfumo mzima wa kodi moja lakini iwe na mapato mazuri, hilo moja tunaomba sana tusaidiwe lakini kodi zikiwa nyingi kunakuwa na matatizo yake umasikini unakuwa upo pale pale.

Mhe. Spika, kwa kuendelea katika kitabu hiki. Mhe. Spika, tutizame pato la mlaji la mtu wa chini, kwa hesabu yangu ya haraka haraka tu ninaona kwa hisabu hii ya kitabu chake ukurasa wa 9, kuna pato la mtu binafsi. Mheshimiwa 2700 mimi ninaona ongezeko hili kwa wastani mimi naona Mhe. Waziri uliangalie vizuri huko mbele utajua zaidi siweze kulichambua sana kwa sababu sijajua mshahara wake ukoje sasa hivi, lakini hali halisi haikidhi haja. Mimi naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri aweze kuliangalia kwa ubunifu kabisa ili suala hili liweze kuleta tija na liweze kuwasaidia wananchi kuondokana na umasikini ambao tuliokusudia.

Mhe. Spika, naomba niende katika fedha za wahisani, ukurasa wa 15. Mhe. Spika, fedha za wahisani utakuta wanasema kuwa kuna mapungufu, mimi najiuliza aidha hawa wahisani wanatufanyia *fix* kutuletea fedha kidogo au hizi fedha zinapokuja watendaji wetu wanachakachua. Mimi Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea kufanyika na mapungufu kama hivi, naomba ili uweze kuniambia niweze kufaidika vizuri nizidi kuvipamba moto.

Mhe. Spika, tuende kwenye ukurasa wa 17 namalizia mbio mbio kwenye programu zetu. Mhe. Spika, tunakuwa na programu nyingi lakini katika programu hizi hebu naomba uniambie katika programu ambazo zilizokuwa zina-*playing* sasa hivi ni ngapi? Naomba sana uniambie programu moja, mbili, tatu zipo hizi au hivi. Mhe. Spika, tunakuwa na miradi mingi, kipindi kilichopita tulikuwa na miradi 84 lakini sasa tunachukuwa miradi mingi halafu umalizaji wake unakuwa ni mdogo sana sana.

Mhe. spika, ninaomba sana bora tuwe na usimamizi wa miradi kidogo lakini tufike pahali mradi ule uwe wa moja kwa moja isije kuwa kila siku tunatoa miradi mingi, lakini hatimae inakuwa miradi ile tunakuwa hatuimalizi tunaiacha njiani. Ninaomba sana Mhe. Spika, hilo aliangalie tena tuna miradi tele mengine mipya tuna programu 35 na miradi 75. Naomba sana hapa ili kwa kuwa sasa hivi inavyoonesha Mhe. Waziri ana lengo zuri sana lakini inakuwa miradi inazidi na inapungua, hajanieleza ni ipi miradi mengine ambayo tayari katika programu hizo ambazo za nyuma, hebu naomba sana mheshimiwa tueleze vizuri sana katika programu zako faida zake zikoje katika mlivyoanzisha hizi programu hizi za utekelezaji na miradi ambayo mingapi ambayo tayari imeshafanyika.

Mhe. Spika, kutokana na kama nilivyosema jana Doctor Jidawi kwa kutoa *presentation* yake hii, nilisema sana jana na niliwaambia Waheshimiwa wenzangu kasoro zimo nakubaliana nazo, lakini na sisi tuchangie sehemu ambazo ndogo sana ili tuweze kupitisha kwa mujibu wa sheria na taratibu zetu, tusinune waheshimiwa kwa sababu humu mna vitu ambavyo vya kitaalamu vimefafanuliwa, ameeleza vizuri sana Mhe. Spika, hakuna mtu ambaye anachukia ripoti hii kama mwenzangu alivyosema kabisa, huu ndio ukweli tuseme ulivyo.

Mhe. Spika, ametumaliza Dr. Jidawi, Katibu ametueleza, Mama Amina katueleza, lakini Mama Amina aliyoyaeleza rasmi kutokana na wajibu wake kwenye taaluma yake; Katibu wetu naye ametueleza vizuri lakini na Dr. Jidawi vile vile ametueleza vizuri.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Spika, kuwa Wajumbe wenzangu sikupigini kampeni lakini naomba sana bajeti hii tuiunge mkono kwa asilimia mia moja kama mimi ninavyoiunga mkono pamoja na wananchi wa Jimbo la Kitoke, kwa sababu wao kwenye programu watafaidika na kuondoa umasikini kwa bajeti hii.

Nikushukuru sana Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Makatibu wake, Manaibu na Watendani wake wakuu ahsanteni sana kwa bajeti hii iliyokuwa haina kasoro, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ataibariki na itapita. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii sote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa pumzi na afya ya kuweza kufika katika hili Baraza lako tukufu tulilokuwepo hapa, ambapo sisi sote tuliopo hapa katika bajeti hii tupo kwa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hotuba ya waziri naipongeza kwa dhati kabisa kwa hali utulivu, busara, hekma na usikivu pamoja na watendaji wake wote ambao wameelezea bajeti nzima na vitu ambavyo vimekosekana humu ndani ambavyo sisi tunatakiwa kuisaidia Zanzibar na kuwasaidia hawa watendaji wetu akiwemo kaka yangu Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwafikiria wananchi wa Zanzibar hasa katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kusamehe *zero percentage* mchele, unga wa ngano, tende na sukari asilimia kumi na mbili (12%). Matumaini yetu sisi wafanyabiashara tutakuwa waadilifu katika kuwapunguzia maisha wananchi

kwa bei hii ambayo serikali imetupa upendeleo sisi wafanyabiashara kwa kusamehe kodi hii. Imefanywa hivi kwa sababu iwalinde walaji ili Mwezi wetu Mtukufu huu wa Ramadhan na naomba nikiwemo na mimi Mohamedraza wafanyabiashara tuwe na huruma hasa katika mwezi huu kutokana na msamaha ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa rasmi.

Mhe. Spika, nimeingia Barazani nashukuru Alhamdulillah tuna mashirikiano na katika semina, lakini narudia tena kusema humu ndani sote naamini kila mtu amekamata msahafu kwa dini yake. Nataka nikuhakikishie Mhe. Spika, mbele ya Baraza hili tukufu toka nimeingia kwenye semina na Baraza hili mimi sizungumzi jambo ambalo sina *document* na sizungumzi jambo la kubuni. Sasa Mheshimiwa nataka niweke wazi katika rikodi yangu kwamba wakati wowote nikihitajika kutoa nyaraka au *document* yoyote, kipindi chote ninazo na hata kipindi hicho nilichokuwa nje ya uwakilishi ninazo.

Mhe. Spika, rekodi yetu inaonesha katika ukurasa wa 14 ukitizama suala la deni la wenzetu Tanzania Bara kuna wafanyakazi wa SMT wanaofanya kazi Zanzibar na malipo ambayo wenzetu watulipe Serikali ya Tanzania Bara *pay as you earn.* Mhe. Spika, mwezi wa Februari ambazo wenzetu wamekusanya kwa niaba yetu wanaita Serikali ya Muungano mimi naita Serikali ya Bara, wamekusanya 1.7 *program* 75 billion mwezi wa Februari. Mwezi wa Machi wamekusanya 1.75 billion na mwezi wa April wamekusanya 1.75 billion. Total ni 5.25 billion.

Mhe. Spika, kinachonisikitisha sana hapa ndio maana nikasema nchi mbili huru zimeungana, Rais wa Muungano, Rais wa Zanzibar ni Marais ambao wako sawa sawa kimuungano na kinchi. Kwa hivyo, nataka kusema Mhe. Spika, hizi pesa wenzetu wamekusanya kwa niaba yetu, walitakiwa watulipe kwa sababu wameshazikusanya, sasa sioni tatizo Mhe. Spika, wenzetu kwa sababu ya uaminifu tumehamia Zanzibar pesa zetu hatujalipwa hizi na tunaingia kwenye Bajeti, 5.5 billion ambazo zingesaidia mambo mengi ya kuweza kuondoa matatizo mengi sana. Sasa mimi nafikiri tusitumie siasa sana kwa sababu hizi ni pesa zetu Zanzibar wala hatufanyiwi hisani, mtu kapokea tunakwenda ukitaka kuchukua wanasema wamezitumia.

Sasa Mhe. Spika, tutafanya kazi kwa maslahi ya wananchi kwa sababu sisi ndio tuna uchungu na nchi. Kwa kweli jambo hili Mhe. Spika, na jambo hili limekuja mwaka jana na ukienda kwenye ripoti yangu nilizungumza haya haya. Sasa Mhe. Spika, mimi naona kwamba, *where is the problem, where is to find the solution and what is next*. Sasa mimi nafikiri *solution* ya hapa kama kuna uwezekano wana kamati, mimi mshamba lakini sikuzaliwa shamba tu, sifahamu mambo sijui kanuni zinasemaje kama tataruhusiwa wanakamati

kama watano mimi niko tayari twendeni Dodoma tukamsikilize waziri atwambie hizi pesa zetu ziko wapi, kwa sababu kishazipokea hamna suala la hisani wala hawatupi msaada, wala hatuombi ni pesa zetu.

Sasa Mhe. Spika, mbali na haya kuna misaada ya kibajeti ambayo kwenye kitabu hiki hiki ukurasa wa 16 na 15 kwenye msaada wa kibajeti mwezi wa Februari, Machi, Aprili inakaribia asilimia 17 hatukupewa wameshazipokea wenzetu. Mimi nafikiri katika mazingira tuliyonayo hii nchi na mimi naipongeza Wizara ya Fedha bajeti hii ambayo makisio yake wenzetu wa Bara hamna msaada wao humu, tunaendesha nchi yetu huru hii bajeti haioneshi kwamba wenzetu Bara au Serikali ya Muungano inatusaidia kutupa sadaka, ni mapitio ya sehemu ile na bajeti hii tunaendesha yetu wenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika mazingira kama haya tuna matatizo mengi, hapa Muungano tunalia kwa sababu ya umasikini lakini kuna pesa hizi na zinaendelea, kuna mwezi wa Juni, sasa angalia kichekesho hawa wenzetu Bara wamekuja kutulipa pesa za mwezi wa Mei, Februari, Machi, Aprili hamna sijui zisharuka hizo, maana utalipa vipi mwezi Mei wakati una deni la Februari hadi Aprili. Sasa Mhe. Spika, mimi naomba sana kwamba sote tumekuja hapa kwa maslahi ya wananchi lakini sioni sababu ya hizi pesa kubadika na kama kuna Waziri Mkuu tumtafute, kuna Rais tumtafute tujue hizi pesa zetu tuna matatizo, tatizo letu njaa, Mhe. Spika, tumeingia humu kwa niaba ya wananchi hilo Mhe. Spika.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika hali nzima ya kiutendaji kwenye mambo ya Kimuungano naomba ninukuu tu kwamba, Gazeti la Habari Leo la tarehe 13 Machi, 2013. Gazeti la Serikali la Tanzania naomba ninukuu:

> "Katibu Mkuu Fedha Ramadhan kushoto na Mwakilishi wa Benki ya *ADB* nchini, Tunis, anasaini mkataba wa kuipatia Zanzibar bilioni 34".

Mhe. Spika, Afisa kutoka Bara anasaini kwa niaba ya nchi yetu ina maana yule Katibu Mkuu Fedha hayupo, Naibu Katibu Mkuu Fedha hayupo. Sasa Mhe. Spika, tumekuwa kama tunatoka Mkoa wa Arusha, hivyo Katibu Mkuu wa Tanzania Bara au Tanganyika anasaini mkataba wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, angalau tungelidanganya kungekuwa na kiini macho, angalau angelichukuliwa Katibu Mkuu Fedha Wazanzibari wangewekwa nyuma tu, hili gazeti Mhe. Spika, Gazeti la Habari Leo.

Saa Mhe. Spika, msaada tunapata sisi basi hatuna mwakilishi wa Zanzibar, ndio niliposema mimi wakati ule, samahani sana, miaka 20 iliyopita cheti cha ndoa tutachukua. Lakini isitoshe hapa Mhe. Spika, tunazungumza sisi tuko

kwa niaba ya wananchi. Gazeti hili la Habari Leo, Gazeti la Serikali maana nisijenikachukua magazeti ya mitaani mkasema wapinzani.

Gazeti la Habari Leo hili la tarehe 15 Aprili, 2013 siku ya Jumatatu, Stanbic yachukua mkopo kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania US$ 600 milioni. Kwenye bajeti sijaona humu mkopo huo hili hapa gazeti la Serikali. Waziri wa Fedha anasema kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huu mkopo na Waziri wa Fedha wa Bara tunaita wa Muungano yeye anasema pesa hizi mwisho Chumbe. Sasa hofu yangu mimi Mhe. Spika, tusije tukabambikizwa madeni haya wakati Wazanzibari hatukuchukua hili. Sasa Mhe. Waziri atusaidie kutupa ufafanuzi, je vipi mkopo huo.

Lakini pia Zanzibar tunapotaka kukopa tunalipa wenyewe tunaambiwa tulipe sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inataka kukopa inalipa ya Muungano mimi sielewi, ikiwa sisi Serikali ya Mapinduzi tunakopa hii Serikali ya Muungano wanasema inalipwa na Serikali ya Muungano, ipi? Ndio maana nikasema hivi leo tupo Baraza la Wawakilishi na kule Bunge linajadili, ninachotaka kusema Mhe. Spika, narejea miaka 20 iliyopita nilisema Tanganyika imejificha ndani ya Muungano ndio huu hapa sasa hivi.

Mhe. Spika, hakuna mtu asiyetaka umoja, hakuna mtu asiyetaka Muungano, hakuna mtu asiyetaka mashirikiano, lakini mashirikiano iwe ni kujadiliana, kuvumiliana na kuheshimiana.

Mhe. Spika, mambo mengi tungeliweza kuyatatua matatizo ya wananchi, leo barabara zetu za ndani Unguja na Pemba gari la punda halipiti na pesa zetu hizi hapa zipo, zimepokelewa hatuna hata senti. Sasa mimi nasema tunayo *solution* tutafute wasaidizi kwa niaba ya wananchi tulitizame vipi tutaweza kulitatua na mimi nafikiri sasa hivi kuanzia kesho tuwaombe ndugu zetu wa *ZRB* wazipokee hizi pesa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar *pay as you earn.*

Mhe. Spika, kwa kweli katika mazingira kama haya na siku zote mimi nilikuwa nazungumza hata wenzetu China wao wametoa karibu Shilingi 54 bilioni kusaidia bajeti ya Tanzania hii hapa. Waziri wa Fedha anazungumza kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 27 Machi, 2013.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba katika hali kama hii tumekuwa na *trust*, ina maana hapa hakuna suala la kuaminiana tena. Kwa hivyo, mimi ninavyotaka kuzungumza mbele ya Mhe. Waziri taratibu sifahamu, lakini nafikiri tufike pahala nchi huru zimeungana mbili, Rais wa Zanziba na Rais

wa Jamhuri ya Muungano tuko sawa sawa katika Muungano hakuna mkubwa wala mdogo. Sasa tuzungumzeni maslahi ya wananchi.

Mhe. Spika sote hapa, mimi nilikuwa huku shimoni nilianza na gari la punda, nikaja baiskeli, nikaja honda, nikaja gari la *Land Cruiser* sasa lazima tuwafikirie na wale wenzetu walikotoka. Serikali inajaribu kufanya na ishafanya mambo mengi, kuna sehemu kuna kilimo na tunasema mapinduzi yetu ni kilimo gari la punda haliendi hao wakulima watavusha vipi mazao yao kufika barabarani mpaka wafike marikiti, tujaribu kufikiria maslahi ya nchi kuliko kuweka udini, udini, udini. Mhe. Spika, huu udini ndio unaotufikisha nchi hapa tulipofika. Kwa hivyo, ninachoomba Mhe. Spika, katika mazingira kama haya na kitabu hiki lazima kama kuna suala litafutiwe ufumbuzi.

Mambo haya mimi sijaanza leo Mhe. Spika, miaka 15 iliyopita kuna kitabu nimetungiwa kule Bara akina Raza watakimbia au watabaki? Hili hapa gazeti. Mhe. Spika, naomba kunukuu jambo dogo tu, linasema hivi:

> "Akina Raza watakimbia au watabaki, mambo mengi aliyokuwa akiyasema bila woga na amekuwa akiitetea Zanzibar kwa nguvu zake zote"

Mhe. Spika, mimi nina uchungu wa Zanzibar, hii ni nchi yetu sote, Zanzibar mimi nchi yangu, mimi siwezi kuwa na marafiki kadri mnavyonijua, tena hao waliokuja ni CCM vile vile wananambia kwamba akina Raza watakimbia au watabaki? Gazeti hili tena Mhe. Spika, tunatafuta nini hapa, tunazungumza suala la nchi. Wenzetu waliotangulia Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliweka nchi ipo, kaja Mzee Aboud Jumbe kaondoka nchi ipo, kaja Marehemu Mzee Idrisa Abdul wakil Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema kaondoka nchi ipo, kaja Mzee Ali Hassan Mwinyi kaondoka nchi ipo, kaja Komandoo, Dr. Salmin Amour Juma kaondoka nchi ipo, kaja Dr. Amani Abeid Karume kaondoka nchi ipo na leo tunae Dr. Ali Mohammed Shein Mwenyezi Mungu amjaalie ampe afya ataondoka nchi ipo. Sasa lazima tufike pahala Mheshimiwa tuwe na uchungu na nchi.

Mhe. Spika, ndani ya kiti changu mimi nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini, lakini sio maana yake kuwa kiti cha Uzini nitaendelea, nitaondoka atakuja na mwenzangu vile vile, lazima tuache alama kwa Wazanzibari, kwa ndugu zetu, kwa maslahi ya nchi ili tujenge nyumba iliyokuwa na ubora na nyumba iliyokuwa na ubora ni kuzungumza maneno ya wazi, lakini tukikaa tukianza kupangiwa *menu*, matumbo haya yameshafanya vidonda, hatuwezi kuwa watu sita wakatuamulia. Leo anakuja ofisa anazuwia pesa tena afisa wa kawaida hii nchi hawa wizara waziri atafanyaje, sana atawapigia simu tu, waziri atatoka afanye nini, Katibu Mkuu atafanya nini, hii

nchi mtu mmoja Ofisa Mwandamizi anazuwia pesa ambazo sisi hawatufanyii hisani wala bajeti hii hawatufanyii hisani ni pesa zetu ni *pay as you earn*.

Sasa Mhe. Spika, mimi naomba busara, hekma, usikivu, tumekuja hapa na nashukuru sana kwa maslahi ya nchi tuendeleeni kupendana ili tuone matatizo ya wananchi ambayo ndio yaliyotuleta hapa. Hii bajeti inazungumza Wazanzibari wa Zanzibar tuondokane kuliko kuanza na lawama hakuna haja ya kupeana maneno. Mimi narejea tena, kama Mhe. Spika, narejea tena wito wangu *Wallahi* kama sisi watendaji viongozi leo nafsi zetu tukiweka pamoja Zanzibar hakuna umasikini kabisa. Kwa sababu tunazungumza mambo ambayo unazungumza na wenzako nyuma anajiambia, anacheka anakuamkia shikamoo nyuma anajiambia hatufiki Mhe. Spika. Kwa hivyo, mimi busara zangu ninachoomba hakuna mtu asiyependa umoja, hakuna mtu asiyependa utaratibu, lakini tuangalie Zanzibar tumetoa nchi huru, tumepoteza mambo yote. Lakini haiwezekani mtu mmoja akasimama akatufanyia anavyotaka tena ofisa halafu anaachiliwa mtu anakuja tu kweli inatia uchungu Mhe. Spika, anapokea msaada kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo Katibu Mkuu Fedha, Waziri wa Fedha halafu tunaambiwa kuna Waziri wa Muungano kule lakini hayumo kwenye Muungano, basi wangelimdanganya wakamchukua Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano, Samia Suluhu Hassan) au Naibu Waziri wa Fedha akamdanganya tu akakaa nyuma tukaonekana na sisi Zanzibar, wewe ni Katibu Mkuu tu wa Fedha, yeye kaona kama yuko Arusha pale kumbe hajui kama hii nchi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninachoomba busara, lakini vile vile naomba Mhe. Spika, wafanyabiashara sisi tujitahidi kubadilika katika kulipa kodi ziweze kusaidia haya maendeleo kwa jumla. Kwa kweli kuna vianzio vingi vinahitajika na viko vingi vinaweza kusaidia kupata fedha. Nasema naipongeza *TRA*, *ZRB* na sehemu nyengine zile za ukusanyaji pesa lakini mashirikiano, elimu, kuelewana ni jambo muhimu. Kwa hivyo, ninaamini bado yapo mambo madogo madogo, zipo kodi nafikiri tukikaa kwa pamoja kodi zetu za ndani tunaweza kuziongoza.

Mhe. Spika, nchi yoyote haitokuwa na tabu kama itaweza kujiendesha yenyewe na kodi za ndani. Kwa kweli hiyo ni moja katika fursa ambayo huko Mwenyezi Mungu atujalie tufike, lakini tukiendelea kuwa tegemezi za wahisani bado tutaendelea kuwa na kipindi kigumu sana katika kujiamulia mambo yetu yenyewe.

Mhe. Spika, nimalizie hapo kwa kuona kwamba nashukuru haya yote yamezungumzwa na nitaendelea kushirikiana na Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar, nitaendelea kushirikiana na Baraza la Wawakilishi na wenzangu, lakini narejea kwamba katika suala la Muungano lazima tuheshimiane,

tuvumiliane, tujadiliane, hivi kesho tunataka pesa zetu ili tuwapelekee wakulima wetu. Hii pesa naomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama zitakuja kesho na lazima zije hakuna sababu Waheshimiwa, kama kuna uwezekano mimi sijui utaratibu wa Baraza kwa sababu ushamba sikuzaliwa shamba tukafahamu mambo, kama kuna utaratibu wa kuweza sisi tukatoka kwa niaba ya serikali au kwa niaba ya Baraza hili tukajenga hoja hizi pesa zitakuja kesho na pesa hizi zikija tushatoka na bajeti, naomba pesa hizi zitumike kwa barabara za Unguja na Pemba mbali madawa.

Naomba pesa hizi zisije zikatumika barabara za mitaani zinachomwa moto na wendawazimu hawa kwa sababu kuna barabara hizi zinachomwa moto mitaani ziachwe Mhe. Spika, pesa hizi zikatumike kwa wanakijiji ambako sisi ndiko tulikotoka sisi sote humu, tulikuwa huko nje kabla hatujapanda *Land Cruiser* tukawa tunapiga kelele sana wananchi wee, wananchi, serikali wee, serikali wee, leo tumevaa suti tunasahau na Mwenyezi Mungu hataki tufike huko. Kwa hivyo, ninachoomba hizi pesa zikipatikana mimi naomba hili hata nikitumwa mimi na vielelezo naweza kwenda kuzichukua ikiwa Baraza la Wawakilishi litaniruhusu, kwa gharama zangu na kama nitapata wenzangu nichukue hatuwezi tena kuvumiliana tu kwa mambo kama hayo. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache kwa ajili ya ujenzi wa nchi yetu. Lakini kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu anayeendelea kutuwezesha kufika katika maeneo haya muhimu ya kujadili mambo ya nchi yetu tukiwa wazima na uhai.

Lakini pia nataka niitumie fursa hii Mhe. Spika, kama walivyotangulia kusema wenzangu kutoa pole kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye ameondokewa na kipenzi chake, kaka yake Inshaallah Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi. Na sitokuwa nimetenda haki kama sitokipongeza Chama changu cha *CUF* Mhe. Spika, kwa kupata ushindi si wa kishindo lakini ni ushindi wa halali, ushindi mkubwa sana. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Mbunge Ndugu Yussuf na namuombea heri na mafanikio katika kazi zake za Ubunge.

Baada ya dibaji hiyo Mhe. Spika, naomba sasa niingie moja kwa moja katika kuchangia hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa nane wa kitabu cha Mhe. Waziri, katika ukurasa wa nane kumeelezewa namna uchumi ulivyokua, uchumi wetu umekua ni jambo la kutia moyo sana na umekua kwa asilimia saba ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka uliopita. Tumeelezwa kwamba pato la taifa limefikia shilingi 1,354 bilioni hiyo sawa sawa na

trilioni moja na bilioni mita tatu na hamsini na nne. Sasa kwa hivyo basi, pato la mtu binafsi kwa sababu mafunzo tulioyapata ni kwamba maana hata mimi nilikuwa najiuliza wanafanyafanyaje hata wakajua pato la mtu binafsi linakuwa vipi, lakini kumbe wanachukua pato la taifa halafu wanaligawa kwa idadi ya watu walioko nchini, hapo unapata kima kile cha pato la taifa mwananchi mmoja mmoja atapata shilingi ngapi kwa mwaka. Kwa *formula* hiyo Mzanzibari kwa pato hili la Trilioni 1.3 basi kwa mwaka Mzanzibari kila mmoja atapata shilingi milioni moja na elfu tatu kwa mwaka.

Sasa ukizigawa hizo kwa siku 360, kwa hivyo kila siku Mzanzibari atakuwa anapata shilingi 2,786. Hapa ndio kwenye kipimo cha kuweza kupima umasikini wetu, maana yake shilingi 2,786 nikiwanazo mimi mfukoni mwangu nikiamka nazo basi naweza kujiuliza masuala mengi kama nitatakiwa nitumie hizo hizo mpaka usiku, kwa sababu hazinitoshi hata kwa chai ya asubuhi sikwambii chakula cha mchana au ikitokea kesi kichwa kinauma niende nikapate panadoli na *unit* angalau mbili tatu za umeme yaani hizi hazinitoshi Mhe. Spika, hata kwa chai ya asubuhi. Sasa hiki ni kiwango cha umasikini, mimi nilikuwa nadhani na nafikiri watendaji hili wamekiri kwamba kwa kweli hali yetu haijawa nzuri ni mbaya sana.

Halafu Mhe. Spika, hili pato la taifa sasa baya zaidi ukienda kwenye mambo yaliyosababisha mpaka tukawa na *calculation* hii ya pato la taifa kuna mambo matatu yamewekwa hapa, ukisoma ukurasa wa tisa utayakutia. Kwanza ni ongezeko la ukuzaji rasilimali kwa asilimia 41 na hii ndio kubwa, ukuzaji rasilimali umeongezeka kwa asilimia 41.3 ambayo ndio imechangia hili pato la taifa. Sasa ukuzaji wa rasilimali kilichoelezwa humu ni uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa nyumba za kuishi na nyumba za kibiashara, zana za usafirishaji na ujenzi vijijini.

Sasa Mhe. Spika, mimi hoja yangu iko hapa na kwa hoja hii nitakayoitoa sasa nakusudia kusema hili pato la shilingi 2,786 kumbe sio pato halisi. Si pato halisi kwa sababu haya mambo yaliyosababisha *calculation* hii ni mambo ambayo hayawagusi masikini wa Mungu moja kwa moja. Mhe. Spika, masikini wa Mungu hawajengi, majengo haya tunayoyaona yanaimarika ni majengo ya makundi ya watu maalum katika jamii hii ambao si wengi. Sasa mimi nilikuwa nadhani sijui wachumi watasemaje, lakini mimi nilikuwa nadhani tusifanye *calculation* za *average* namna hii hata kama formula yenu ndio inavyosema. Mimi nilikuwa nataka tuwagawe watu kimakundi masikini wa Mungu wamekua vipi na pato lao liko vipi, watu wa katikati wako hivi, watu wa *high rate* wako hivi.

Kwa sababu ukifanya *average* hii 2,786 ukiuchukua kwa jumla kumbe haiwafikii wananchi moja kwa moja, kuna masikini wa Mungu hapa hata

shilingi mia tano hawapati. Sasa mimi nadhani watupe *statistic* za kuonesha hili kundi la masikini wa Mwenyezi Mungu katika hizi 2,786 wao mnawapa ngapi, hizi pengine za matajiri. Mhe. Spika, wafanyabishara, watu walioko serikalini pengine mimi najua kuna watu humu humu wana nyumba sita mpaka nane na hizo idadi za nyumba zinazojengwa huko ndio mtakazokopeshwa nyinyi. Hivyo, mimi nakusudia kusema hili si pato halisi la Mzanzibari tutafuteni *formula* nyengine, kuna watu masikini wa Mwenyezi Mungu wanapata kiasi gani yule masikini aliyekuwa hana uwezo wa kujenga.

Mhe.Spika, jambo jengine ambalo nakusudia kusema ni kuhusu bajeti ya Serikali. Sasa tumeambiwa bajeti ya Serikali mwaka huu inakusudia kutumia shilingi 658.5 bilioni, hiyo ukifunua ukurasa wa 38 mpaka 39 ndio kuna maelezo haya. Mapato ya ndani kati ya hizo ni milioni 333.7, wahisani ni milioni 277.9. Sasa ukiyachanganya mapato ya ndani na yale ya wahisani na haya unayojumuisha mpaka misaada ya kibajeti sijui na misamaha ya kodi kwa kujumla unapata shilini bilioni mia 616.6. Sasa kwa kuwa hiyo haijafika kuna makisio hapa ya bilioni 41.9 ndivyo alivyotwambia Mhe. Waziri.

Sasa ili kuziba pengo tatizo langu liko hapa Mhe. Spika, ili kuziba pengo la nakisi 41 bilioni kwa mwaka huu. Mhe.Waziri anakusudia kurekebisha sheria 11 za kodi. Sasa Mhe. Spika, ikiwa *point* yangu ya kwanza ina maana kwamba kipato cha mtu binafsi kiko hapa ambayo mimi nilisema nisihadithie hii itapungua halafu mtu huyo unampandishia kodi sheria 11 unazibadilisha, huko si kummaliza jamani?

Mhe. Spika, mimi nadhani katika hili simlaumu sana Mhe. Waziri kupandisha hizi kodi kwa sababu anataka kukidhi mahitaji ya bajeti yake. Tumesomeshwa pale kwamba vizuri zaidi sio kuongeza bei za bidhaa, leo pakacha moja la machungwa umeliuza shilingi 2000 bajeti yangu ya leo ipo, kesho bajeti yangu imeongezeka pakacha lile lile la machungwa pengine mna machungwa 30 yamo mle, yale yale leo nayauza elfu 3000 badala ya 2000. Utaratibu huu si mzuri, kwa sababu kuna kundi la watu linadhalilika sana na anayelipa kodi si mfanyabiashara bwana, anayelipa kodi ni mnyonge masikini ya Mwenyezi Mungu hohe hahe.

Mhe. Spika, sasa leo ukimuongezea Mhe. Mohamedraza Hassanali kodi halipi yeye ana biashara yake na kwa vyote vile atakayeumia ni yule mwananchi. Kwa hivyo, na yeye ataongeza bei ya bidhaa yake kwa sababu kodi imeongezwa atakayeumia ni yule mwananchi. Sasa mwananchi tunamsaidia vipi. Mimi ushauri wangu Mhe. Spika, nadhani Serikali sasa ijikite katika kuongeza uzalishaji baada ya kung'ang'ania kodi zile zile, tupanue wigo wa uzalishaji ili na kodi ziwe zinajaza hii mifuko sio tunapenya pale pale kila siku. Tumeambiwa humu sijui ukurasa wa ngapi nimesahau lakini leseni ya

njia ile utaratibu uliowekwa ni shilingi 35 kila lita ya petroli au dizeli atakayonunua mtu. Nilijaribu kuifanyia *calculation* hiyo Mhe. Spika, tena nilifanya *calculation* kwa mtu atakayetumia lita kumi tu za petroli na siku nimesahau ile. Lakini niliifanya kwa mwaka sasa ile nimezingatia mtu huyu atakayetumia lita kumi kwa mwaka bei ile ya kuongeza shilingi 35 atakuwa analipa laki moja na ishirini na sita elfu kwa mwaka.

Mhe. Spika, ili kutoka shilingi 36 elfu na huyo ni mtu ambaye anatumia lita kumi lakini fikiria ni watu wangapi wanatumia lita ishirini, hamsini kwa siku, tutamfanya mtu sasa alipe zaidi ya laki mbili na nusu kwa mwaka baada ya leseni ya shilingi elfu hamsini au sitini. Ukifanya hivyo maana yake nini? maana yake hiyo yule mteja anayehudumiwa na gari lile na yeye lazima alipe zaidi kwa sababu na yeye anafanyabiashara kama daladala lazima alipe na hawezi kwenda kwa hasara. Kwa hivyo, matokeo yake mzigo unakwenda kule kule kwa wananchi.

Mhe. Spika, mimi nafikiria kwamba hatujakuwa na uamuzi mzuri. Mimi nilikuwa nadhani tuna wachumi wazuri kweli kweli Zanzibar. Mhe. Spika, hebu tukae kitako wachumi tutafuteni njia zitakazotusaidia kuongeza mapato yasiokuwa haya ya kuongeza kodi kila siku. Nadhani njia nzuri ni kupanua wigo wa kodi sio kuongeza kodi kila siku.

Mhe. Spika, kifungu cha 333 cha Katiba ya Zanzibar cha *section one* uwezo au ruhusa ya kutoza kodi inatoka katika Baraza hili. Mhe. Spika, mimi naomba sana nimshauri Mhe. Waziri hiki kiwango cha shilingi 35 kwa lita ya petroli akipunguze hilo namuomba sana. Kwa sababu kikibakia hivi hivi kitazidi kuwaelemea wananachi na sisi hapa tupo kwa ajili ya kutetea wananchi, tupo kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi. Kwa hivyo, tutafute ufumbuzi mwengine lakini hizi pesa shilingi 35 zipunguzwe.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ajira na hapa nataka nimnukuu Mhe.Rais wa Zanzibar siku aliyepokuja kulihutubia Baraza kwa mara ya kwanza, alisema katika mambo ambayo alisema moja ni kuajiri watu na akasema ataajiri watu kwa asilimia nimeisahau. Lakini kwa kifupi alisema mle miongoni mwa kero kubwa za jamii hii ni ajira na akajitahidi kusema kwamba atatoa ajira. Sasa ajira mimi nilizigawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni zile ajira anazopata mtu akawa analipwa mshahara anafanya kazi ya watu akawa analipwa mshahara. Kundi la pili ni ajira ambazo mtu mwenyewe binafsi anatafuta biashara ya kufanya ambayo itampatia kipato chake cha kuweza kukidhi mahitaji yake.

Mhe. Spika, katika makundi yote mawili haya kuna matatizo hii ajira ya kuajiriwa halafu ukalipwa mshahara imekabiliwa na mambo mengi, lakini

mimi nataja mawili. Moja hatuna usawa katika kupewa ajira na hili limesemwa sana hapa asubuhi na Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma akajitahidi sana kupapatua lakini bado na mimi nasisitiza hakuna usawa katika kutoa ajira.

Mhe. Spika, nchi hii ni ya Wazanzibari wote mimi nilikuwa nadhani tumejipangia mipango mizuri sheria, sera, Katiba na Kanuni zetu *wallahi* ukizisoma huwezi kuziona dosari yoyote. Lakini kidogo kuna matatizo, sasa naomba sana kuwe na usawa katika ajira.

Mhe. Spika, tusipewe ajira kwa ubaguzi si wa eneo mtu analotoka wala chama anachotoka wala jinsia. Mimi nadhani katika hili tuwe makini kabisa kwa sababu ni kero kubwa wananchi wanayo na wananchi wote wanahitaji hilo. Mhe. Spika, tumelalamikiwa Mhe. Waziri aliwahi kusema hapa hakuna kesi iliyopelekwa kwake, lakini sisi Wawakilishi wa wananchi tunalalamikiwa sana kwamba mtu akienda kuomba ajira anaambiwa maneno hata kuyasema hapa siwezi naona aibu hasa. Kwa kweli si vizuri yanayofanywa.

Mhe. Spika, halafu kuna hizi ajira hasa za muungano Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi ni ajira ambazo watu wetu Wazanzibari wana haki ya kuzipata. Mhe. Spika, zimeelemewa na wimbi la ufisadi. Kuna utaratibu sijui ni wa Kikatiba au ni utamaduni tumejiwekea, lakini ajira kwa mfano za Polisi, Jeshi basi zinagaiwa kimkoa. Kwa mfano unaweza kuambiwa hizi zitakwenda kwenye Mikoa ya Zanzibar kama ni asilimia 5 au 4 ili mradi hizi zinakwenda kwenye Mikoa ya Zanzibar na zikifika hapa Zanzibar zinagaiwa kwenye Mikoa mitano hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mfano ukiambiwa kama Mkoa wa Mjini/Magharibi nafasi yao ni watu 50 basi wale watu 50 wawe wa Mjini/Magharibi. Lakini leo zinakuja ajira watu wanajitokeza masikini ya Mungu wanakwenda kufanya *interview* kinachotokea wakubwa wale wa vyombo hivi wanapenyeza ndugu zao ukija ukitizama Mhe. Spika, kama nafasi 50 zimebaki 10 tu ambazo wanapata Wazanzibari, nyengine zinaondoka na wenyewe hii si haki. Kama ni haki yetu watu wa Mjini/Magharibi nafasi 50 maana yake zote 50 ziwe za Mjini/Magharibi. Sasa hili linafanyika na linasababisha manung'uniko mengi ukija kwenye Polisi yako hivyo hivyo na kwenye vikosi vyetu wenyewe wako vile vile. Mimi nadhani Serikali ijitahidi sana kurekebisha. Mhe. Spika, amani inakuja kwa kufuata sheria ukianza kupinda sheria ni chazo cha kuvunja amani katika nchi. Vizuri zaidi wananchi wenyewe wawe radhi na uongozi ulioko madarakani uwe unawatendea haki kwa mujibu wa sheria tuliojipangia hili la msingi sana.

Jambo jengine ambalo linawakabili wafanyabiashara waajiriwa hawa wanaopokea mshahara. Mhe.Spika, hasa kwenye *private sector,* mahoteli ya kitalii kuna vikundi vya ulinzi siku hizi kuna makampuni ya *Zantel* na mengineyo yote yanaajiri watu. Kwanza tunawapongeza kwa kutuwekea ajira za namna hiyo wanatusaidia. Lakini sasa kinachotokea zile sheria za kazi hazifuatwi mle mikataba anaweza kuajiriwa mtu miaka mitatu hajafungishwa mikataba halafu akifukuzwa ndio kishafukuzwa hakuna haki yake yoyote kwa sababu hakuna mkataba. Hivi karibuni *Zantel* walifanya kitu hicho hicho, kuna watu kwenye sekta ya ulinzi waliachishwa kazi.

Kwa hivyo, kwa kuwa hakuna mkataba rasmi hata malipo yao ya kiinua mgongo wamelipwa kwa watakavyo tu si kwa mujibu wa sheria za kazi. Sasa hili nimeliona humu kwenye kitabu lakini nilikuwa nasisitiza kwa kweli sekta binafsi Serikali iwe inafuatilia kwa karibu kweli kweli wanawadhalilisha vijana wetu katika upeo mkubwa. Kama kima cha chini Mhe. Spika, cha mshahara ni shilingi lakini moja na nusu kuna watu wanalipwa shilingi sabini elfu tu hivi sasa katika *sector* ya *private* unamkata mtu mshahara mpaka inakuwa balaa hana mkataba wala hana chochote unamdhalilisha na yeye mwenyewe anahisi, lakini maisha magumu tu ndio yanayomsukuma kule. Sasa nilikuwa naomba hili suala lifuatiliwe kwa ukaribu sana maana yake watu wetu wanadhalilishwa.

Jambo jengine ambalo muhimu Mhe. Spika, na kwa sababu muda wako umeshakwenda sana nataka liwe la mwisho. Mhe. Spika, ajira hizi za Serikali za *private sector* kwa kweli zinachukua watu kidogo sana ajira ambazo zingetusaidia sana kuwaajiri watu wengi ni ajira hizi za mtu mwenyewe kujitafutia sehemu kama ni mkulima au mvuvi mfanyabiashara mchuuzi wa samaki, hizi Mhe. Spika, ndio ajira zinazoweza kuwasaidia watu wetu kwa wingi sana na mimi nilikuwa napenda sana takwimu zetu zituoneshe hivyo, tuna watu wangapi Zanzibar ambao wana uwezo wa kufanyakazi, kati ya hao walioajiriwa Serikalini ni wangapi walioajiriwa sekta binafsi ni wangapi na waliojiajiri wenyewe ni wangapi. Halafu tupate kupima tunaweza kupunguza kiasi gani kuwapeleka watu kwenye ajira ya Serikali au vyenginevyo. Lakini tusiiache hivi hivi maana mpango lazima uwe na *statistic.*

Mhe. Spika, sasa hili kundi kubwa sana lakini tatizo la kundi hili kwanza Mhe. Spika, linakabiliwa na kero watu wanajiajiri wenyewe. Kwa upande mwengine Serikali inawafanyia sivyo, amesema leo asubuhi hapa Mhe. Subeit Khamis Faki pale Darajani imekuwa balaa sijui kwa nini na hili tatizo ni la muda mrefu sana Mhe. Spika. Hivi kwa nini Serikali haiandai mazingira itakayowafanya wale wafanyabiashara wawe wanakaa pahali pazuri ambapo hapaleti kero kwa watu wengine, lakini na wao wanaweza kupata riski zao pale. Kila siku tufukuzane kwa mabunduki pale si uzuri. Maana wewe ukipita

Darajani sasa hivi wanakusimamisha watu zaidi ya kumi wanakuzungumzia kwamba jana tumefukuzwa hivi na hivi, ukija kwa Mhe. Waziri huku anakwambia kuwa wamevunja sheria. Hebu tengenezeni mazingira wale watu wasivunje sheria na wapate pahali pa kukaa wafanye biashara zao wenzetu duniani ndivyo wanavyofanya.

Lakini nilikuwa nadhani Serikali ina kazi kubwa ya kufanya Mhe. Spika, kupanga mipango ambayo itazalisha hizi ajira na tuna vianzio vizuri vya hizi ajira kwa mfano tuna ardhi yetu nzuri ya kilimo. tatizo letu kilimo chetu si cha uhakika, kilimo ambacho mkulima analima vile alivyozowea halimi kitaalamu. Jana tulipokuwa kwenye semina mtaalamu mmoja alitwambia Zanzibar kwa jumla tunalazimika kuagiza mchele kutoka nje kwa sababu tukilima wenyewe hapa inakuwa ghali zaidi kuliko ule wa kuagiza nje, maana huko wanakozalisha wao wanazalisha mchele mwingi kwa bei nafuu kuliko tunaolima sisi. Hapa pana nini wataalamu watwambie tunakosa nini sisi ardhi tunayo, Serikali tunayo watu wa kulima wapo, kitu gani, nafikiri tutafute wataalamu wa kilimo hapa watwambie tumekosea wapi, ukienda kwenye uvuvi nako hivyo hivyo.

Sasa haya ndio mambo ya kushughulikia na yenyewe yangesaidia sana kuinua uchumi kwa sababu uchumi unainuliwa na watu hawa wenye ajira ndio wanaoinua uchumi. Sasa hebu tujipangeni mipango mizuri wasitupe nambari tu hapa kila siku nambari nzuri ukisema wewe unaweza kucheka humu. Lakini tunataka matendo, rai na mikakati itakayotukwamua hapa tulipo Mhe. Spika.

Awamu ile ya pili ya Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi kulikuwa na Vyuo vya Kilimo Pemba na kilikuwa kinaendelea vizuri na kulikuwa na Chuo cha mambo ya uvuvi Lumumba, lakini kulikuwa na Chuo cha Karume kinafundisha Ufundi, Chuo cha Mikunguni kinafundisha ufundi. Hizi ni sekta muhimu sana ambazo kama zitaimarishwa bahati mbaya Chuo cha Kilimo kimekufa tena nasikia wamefungua chengine Kizimbani hapa, Chuo cha Uvuvi sijui kama kipo hapa. Sasa hivi ni vyuo vya kuimarishwa kweli na kuna haja sasa Mhe. Spika, huu mtaala wetu wa elimu ubadilishwe watu wanasoma afya tu, kuna madigirii kibao na miaka kumi ijayo kutakuwa na madigirii hapa hata la kufanya hatuna. Lakini madigirii hayana ajira hayazalishi chochote hebu tuelekeze utaalamu wetu tutoe elimu itakayomfanya mtu apate mbinu ya kujiari mwenyewe hii ingetusaidia sana na ajira zipo kwenye kilimo kwenye uvuvi.

Lakini jambo jengine ambalo linatukwaza mtu siku nyengine ana elimu lakini mtaji hana Serikali ijipange kuwapatia watu mitaji mtu akitaka kuvua apatiwe mtaji utakaosaidia kuvua akijikita kwenye kilimo apatiwe mtaji kwa sababu

kulima ni gharama hawezi kulima mtu bila ya pesa na ukimpatia mtu pesa atalima kwa faida. Kwa hivyo, ni jambo jengine ambalo ni mihumu.

Mhe. Spika, baaada ya kusema hayo nadhani mimi nimeshamaliza yote sina tatizo naunga mkono bajeti hii ahsante sana.

Mhe. Mansoor Yussuf Himidi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pili nikupongeze wewe Spika wetu kwa namna unavyoendesha shughuli hizi nakuombea afya njema, maisha marefu kwa Mwenyezi Mungu na *inshaalla* Mwenyezi Mungu atakuepusha na mitihani iliyo migumu na akujaalie kila la kheri.

Mhe. Spika, niendelee kwa kumpongeza Mhe. Waziri ndugu yetu Omar Yussuf Mzee kwa maandalizi na uwasilishaji wake wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali, sote tuna imani na matumaini makubwa juu ya uendeshaji wake, heshima yake kwa wenziwe sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa nchi hii na yeye tunamuombea kila la kheri na mafanikio katika usimamizi na utelezaji wa bajeti hii ya Serikali tukielewa kwamba dhamira ni njema pale panapo wajibu wetu tutafanya kumsaidia yeye kuwa na mafanikio makubwa zaidi.

Mhe. Spika, nilihitaji muda mwingi zaidi lakini muda uliobaki kuelekea saa saba ni mchache, kwa hivyo nitagusia maeneo matatu, alioyagusia Mhe. Waziri. Awalan kwa maana la mwanzo la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Pili Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na tatu suala la marekebisho ya kodi na nitakuwa na maswali na rai au ushauri.

Mhe. Spika, nikianza la mwanzo ni Mapinduzi yetu Matukufu ya Januari 12 ya mwaka 1964. Mhe. Waziri amezungumzia umuhimu wa kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi hayo mwakani Mwenyezi Mungu akituweka hai. Jambo hili mimi limenipa faraja kubwa sana na napongeza umakini na utayari wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kujipanga vizuri katika kuadhimisha Mapinduzi haya ni jambo la faraja na heshima kubwa kwetu sisi Wazanzibari na wale waliokuwa waumini wa Mapinduzi hayo kama mimi ni faraja na heshima kubwa zaidi.

Mhe. Spika, hapa nina ushauri au rai kwa Mhe. Waziri nataka nikukumbushe kwamba Mapinduzi hayo yalikuwa na malengo yake na sababu za kuwepo kwake tukiyazingatia hayo basi ni wajibu wa Serikali na sisi viongozi wa wananchi humu ndani kuandaa mazingira yatakayokuwa muafaka kuadhimisha maadhimisho hayo ya miaka 50. Tukikumbuka kwanza kwamba Mapinduzi yamekuja kwa kutafuta mamlaka kamili ya Wazanzibari, kwa

maana ya Wazanzibari kujitawala wao wenyewe. Uhuru uliokamilika baada ya kumuondosha mkoloni.

Pili yaliokuwa muhimu na ya msingi zaidi ni usawa wa Wazanzibari wenyewe, kuondosha ukabila, ubaguzi, kuoneana na Wazanzibari wote kuwa wamoja bila ya kujali Mzanzibari huyu katoka wapi, ana rangi gani, ana dini gani, ana msimamo gani au ana itikadi gani ya siasa na mtizamo wake na sote Wazanzibari kuwa sawa mbele ya sheria ya nchi yetu. Tukiyachukua hayo sasa ni wajibu wa Serikali na namshauri Mhe. Waziri Serikali iandae mazingira ya Wazanzibari wote kuelekea kwenye maadhimisho hayo tukiwa na furaha na wamoja na tusihofie wale miongoni mwetu wenye madukuduku yao, na ningeshauri wakati umefika pia kuandaa mahojiano na makongamano ya wazi ya kuwauliza wananchi wa nchi hii nini maana ya Mapinduzi. Kwao wao nini faida ya Mapinduzi hayo, wapi tumefika, wapi kasoro ziliopo na vipi tunafanya ama kwenda mbele zaidi. Kwangu mimi Mapinduzi haya ni aina ya pekee na mafanikio yake pia ni pekee. Kwa maana Mapinduzi yaliyofikia miaka 50 nadhani ni ya Cuba, China na Korea ya Kaskazini.

Lakini mimi naamini mafanikio yaliyopatikana na Mapinduzi ya Zanzibar ni ya aina ya pekee, kwa maana nchi zote hizo nilizozitaja uhuru, fursa za watu sio sawa na huko. Vyama vingi vimeshamiri kwetu, uhuru wa mtu mmoja mmoja na wa vikundi umeshamiri kwetu, heshima ya mtu mbele ya sheria imeshamiri kwetu, ni tofauti na nchi nyengine hizo nilizozitaja. Japokuwa Wachina wanapiga hatua kubwa kwenye masuala ya kiuchumi, Wacuba nao na wao wana mafanikio yao. Lakini kwa jumla mimi naamini Mapinduzi ya Zanzibar yamekuwa na mafanikio makubwa zaidi.

Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunayasakafia mafanikio haya ili tuweze kusonga mbele kwa manufaa ya watu wetu. Tusiwahofie wale ambao pengine hawakubaliani nayo mia juu ya mia. Lakini naamini wanaokubaliana nayo wako wengi zaidi. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali kuhakikisha kwamba mazingira ya kuelekea Januari 12, Mwenyezi Mungu akituweka hai mwakani ni ya umoja, ni ya mshikamamo na kila Mzanzibari kujihisi na yeye pia ana haki na ni sehemu ya Mapinduzi yake, yasije yakawa sasa ni ya kundi fulani na wengine wote wakawa sio, huo ni wajibu wa serikali.

Nakuomba sana ndugu yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, nyinyi Mawaziri na serikali kwa jumla mfanye kazi hiyo ili tuelekee huko na muelekeo mpya wa namna ya kuyalea na kuyaendeleza Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, kuhusu Muungano, Mhe. Waziri ameyagusia humu. Hapa nina swali lakini nianze kwa kusema kwamba kila mmoja wetu na hasa baada ya

kuzungumza kwa kuyazungumzia Mapinduzi yetu, ni sawa na mwenziwe. Mapinduzi yale kwa lugha ya moja kwa moja au ya mtaani ndio yaliyotupa jeuri na kibri cha kufika hapa tulipofika leo. Tukielekea kwenye Muungano huu, mimi naamini ulipoasisiwa na kwa mawazo yangu mimi hadi hii leo una umuhimu wake na mimi ni muumini wa Muungano huu, lakini kwangu mimi ni Muungano wa aina gani ndio muhimu.

Kwangu mimi kuwa na Muungano ulio wa heshima, ulio sawa, ulio wa haki ndio msingi na kwa fursa hii iliyojitokeza ni wajibu na haki ya kila mmoja wetu kuwa na fursa ya kueleza namna anavyoona Muungano huo uwe na hatima yake.

Mhe. Spika, mimi nikiwa mjumbe wa Baraza hili lako tukufu, tangu mwanzo wa Baraza hili linaanza sikupata kuficha hisia zangu juu ya namna ninavyoona mimi Muungano unapaswa uwe na mimi nina muelekeo wa *confederation* kwa maana Muungano wa mkataba, ndio hisia zangu mimi. Hisia zangu mimi ni zangu mimi mmoja peke yangu, sina uwezo wa kumlazimisha mwengine yeyote humu ndani na sina haki ya kufanya hivyo na wala sina ugomvi na mwengine na mawazo yake.

Ikiwa kuna mtu anahisi serikali mbili ndio zinafaa basi ni haki yake, kama kuna wengine wanahisi serikali tatu ndio zinawafaa ni haki yao na ikiwa wengine wanahisi mbili kuelekea moja ni haki yao. Kuna watu humu humu wanasema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Zanzibar isiwepo hasa aa!! wapo, tena wengine wakubwa na wazito. Lakini sitokubali kwa njia yoyote ile mtu kunilazimisha mimi kwa yale ninayoyaona. Bado ninaendelea kuwa na msimamo wa Muungano wa Mkataba.

Lakini bwana Warioba ametuletea rasimu ya serikali tatu. Nashukuru hajafukuzwa kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala na wenziwe hawajatimuliwa kwenye nchi hii, maana kuna watu wakali humu. Lakini ile rasimu mimi sijaikataa, kwa sababu ikiwa ni mtu mwenye akili nina wajibu wa kuipitia, kuipima, kuifahamu na eneo ninalokubaliana nalo sawa na nisilokubaliana nalo sawa tutasema na tutaendelea kusema na hatutosita kusema.

Mhe. Spika, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Raza, tena alianza kusema kama alivyosema yeye mwenyewe sio mara yake ya mwanzo hii, ameanza kusema miaka 20 nyuma na wengi tumeyashuhudia aliyokuwa akiyasema Mhe. Raza, ninaungana naye. Nchi zilizoungana ni Zanzibar na Tanganyika kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ugomvi uko wapi. Hili jambo halitaki ugomvi, panahitaji busara.

Mhe. Spika, inasikitisha kwa juhudi kubwa tunayochukua kuleta umoja miongoni mwa wananchi wa nchi hii, ukawaona viongozi wanachochea hisia potofu za wananchi. Matusi gunia zima, mtu mzima anasema mpaka anatoka mapovu, kwa nini? Kwa sababu kuna mtu hakubaliani na mawazo yake, msingi wake unajiuliza kulikoni. Yeye anataka serikali mbili mimi sitaki. Narudia tena mimi sitaki, ugomvi uko wapi.

Kwa hivyo, mawazo huwezi kuyatia mnyororo, mawazo huwezi kuyapiga nyundo au mawe yamo kichwani mwangu na hatuwezi kujenga nchi imara yenye umoja kama malengo ya Mapinduzi yanavyotuambia, ikiwa hata kwa mawazo kutofautiana imekuwa ni tatizo na kosa la jinai ndani ya nchi. Ni lazima tufike pahala na tuelewe kwamba sote hatuwezi kukubaliana, lakini misingi ya nchi iliyoachwa na Mapinduzi matukufu ndio ya sisi kusimamia na kufuata.

Mhe. Spika, mtu yeyote yule na hasa viongozi, nimeshawahi kusema na ninasema tena. Kiongozi anapoanza kuwapachika wenziwe majina. Leo hii baada ya miaka 50 ya Mapinduzi yetu kusimama na bendera ya Zanzibar kujivunia na kusimama na kupepea, anahofia Sultan kurudi ndani ya nchi. Bwana Karume kasimamisha Jamhuri, na ndani ya Jamhuri watu huchaguana.

Tujiulize Mhe. Spika, Sultan gani asiyekuwa na akili akaacha utajiri akaja hapa kwa maskini. Hao waliokuwa wanatutawala, walipokuwa wanatutawala walikuwa wakilala chini ya Ngamia, leo nenda kwenye nchi zao, wametuwacha nyuma miaka miaka 200. Sasa atoke kule kuja kufanya nini hapa. Ana mafuta, ana viwanda, ana gesi na majumba yanakwenda juu, anajenga pwani, anajenga chini ya ardhi. Sisi ghorofa saba hatujafika, tujiamini sisi wenyewe kwamba Mapinduzi yameshafika na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu yataendelea. Muhimu kufuata misingi yake, malengo yake na dhamira yake njema, hatuwezi kupotea. Tufuate dhamira njema, tufuate misingi yake hatuwezi kupotea.

Lakini leo hii vielelezo vya watu ni watu wenye matusi gunia, haya ni mawazo ya watu, watu wanakusanya mawazo. Kwa hivyo, demokrasia ni wengi wape. Sasa iweje leo Mhe. Spika, narudia tena, kwamba Wazanzibari wanataka kulazimishwa kuwa na kikomo cha fikra zao, hilo haliwezekani abadani, hatuwezi kukubali. Mtawaita watu majina mpaka lini? Mtawatukania wazee wao mpaka lini? Kama wewe Mzanzibari na sisi ni Wazanzibari, haki yako na yangu sawa sawa, ilimradi mimi sivunji sheria ya nchi hii, ndio misingi na hayo ndio Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na ndio muelekeo sahihi wa Mapinduzi haya. Rasimu ipo, Mabaraza ya Katiba yanakuja, kila mtu ana haki ya kueleza kile alichokuwanacho. Tuna haki ya kuwashawishi watu kwa misingi ya hoja, sio porojo, sio matusi na kwa dunia hii nani

atakusikiliza kwanza Mhe. Spika. Ukienda na matusi watu wanaondoka, ukienda na hoja, busara, hekima watu watakaa watakusikiliza na kupima.

Sasa tunawaambia jamani Muungano ni wetu sote, bado tunauamini, nasema tena bado tunauamini, tunaelewa umuhimu wake. Lakini kwetu sisi wengine aina ya Muungano ndio muhimu na tunaamini pakiwa na fursa ya wanadamu kuweza kutoa mawazo yao au maoni yao, tutapata mambo ya maana na ya msingi kuendeleza Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar. Naamini utakuwa na faida na tija kubwa zaidi kwa pande zote mbili, kushinda tukatishana tishana, kasoro zikafutikwa futikwa, ndio maana mpaka hii leo tunazizungumza hizo kero, mpaka hii leo watu wazima humu ndani wanatoa magazeti ya miaka 20 iliyopita, mfano wa magazeti ya leo. Kwa sababu mfumo tuliokuwanao haukidhi mahitaji kwa pande zote mbili hizi, ni mwelekeo mpya wa kileo na ambao utaweza kuongeza nguvu ya mahusiano baina ya pande hizi mbili, bila ya kuambizana sijui mwisho Chumbe, mwisho wapi na wapi.

Hapana Mhe. Spika, tunaweza kuwa na Muungano tukawa tunaheshimiana na tukapiga hatua kubwa zaidi na hilo ndio lengo, tunafika miaka 50 ya Mapinduzi, miaka 50 ya Muungano, wapi tumetoka, wapi tulipo na wapi tunataka kwenda. Lakini sasa ikiwa kuna watu wazima humu wengine akili zao zina walakini, basi tutakuja kuangukia pabaya na wakitarajia kwamba kwa kuwapiga piga watu maneno, vitisho hapa na pale, kumwita mtu hizbu, sultan huyo hataki Muungano, watu wataacha kusema wamekosea, tena wamekosea sana na tena tutazidi kusema.

Mhe. Spika, nikiwacha Muungano nakwenda kwenye masuala ya marekebisho ya kodi. Lakini nilikuwa nina swali kwenye sehemu ya Muungano. Mhe. Waziri amezungumzia Muungano, kwenye kipengele 32 ukurasa wa 22. Swali langu ni kwamba Mhe. Waziri amejiandaa vipi au serikali yetu imejiandaa vipi. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Raza kwamba mabadiliko yapo na yanakuja. Je, serikali yetu imejiandaa vipi. Kwa hisia ziliopo, pamoja na maneno ya Jaji Warioba, maana yake mimi sikumsikia lakini nimewasikia wengi na kama nimekosea Mhe. Waziri nitakuomba unisahihishe kwamba Wazanzibari wengi waliotoa maoni walitaka Muungano wa mkataba, sijamsikia mimi nimeambiwa na watu waliomsikia na akasema walikuwa na hoja za msingi, lakini ili kwenda kwenye mkataba inabidi uvunjwe Muungano kwanza, kwa hivyo wamekuja na wazo la serikali tatu. Sasa hilo linaonesha kwamba wengi wa Wazanzibari tayari wanataka mabadiliko.

Je, serikali yetu imejiandaa vipi. Japokuwa maneno haya ya Jaji Warioba mimi binafsi sikukubaliana nayo, kwamba kuwa na mkataba uvunjwe

Muungano. Hapana, nimeona ametafuta sababu. Lakini sio neno, ndio utaratibu tunaokwenda nao na kama nilivyosema hata hii rasimu aliyokuja nayo, tutakuwa wapumbavu tukiikataa. Ni lazima tuipitie tuifahamu, tupime na tuishauri tume na humo tutatofautiana. Lakini hatimaye ni ile misingi imeshasakafiwa na Mapinduzi ndio sisi tuzingatie, umoja wetu, usawa wetu, haki na fursa na ustawi wa Wazanzibari, hayo yote ndio ya msingi. Ustawi wa watu wa Wanzibar na ustawi wa watu wa Tanganyika, kuunganisha nguvu za pande hizi mbili kuwa na kitu kimoja kilichokuwa imara, lakini kwa kuelewana vyema.

Kwa hivyo, swali langu ni hilo Mhe. Waziri, nimalizie kwenye masuala ya kodi. Mhe. Waziri nilivyofahamu mimi hukuwa na kodi mpya kwenye sekta ya utalii, lakini umefanya marekebisho ya kodi hizo. Kwanza kwa hilo tunakupongeza sana umeona mbali, umepima vizuri na umekuwa na hekima kubwa, tunakushukuru. Kwa sababu baada ya athari tuliyoipata kwenye uchumi wa dunia, sekta ya utalii ambayo tunaitegemea imeathirika sana hapa kwetu na bado haijakaa sawa itachukua muda mwingi zaidi au miaka mingi sana kukaa sawa.

Kwa hivyo, kwa kipindi hiki kuiongezea kodi sekta hiyo serikali kwa kweli itakuwa inafanya kosa kubwa, lakini nashukuru serikali yetu hilo wameliona na badala ya kuongeza wamefanya marekebisho. Lakini bado nina swali la kumuuliza Mhe. Waziri, hii *logic* ya kufanya marekebisho hayo imetokana na misingi ipi au viashiria vipi, naomba anisaidie maelezo yake.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri alizungumzia misamaha ya kodi. Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba kwa uzoefu wangu mimi binafsi na wawekezaji wengine ambao nazungumza nao, wanaridhika sana na utaratibu uliopo wa misamaha ya kodi, utaratibu unavyofuatwa na muda ambao wanapata huduma hiyo. Lakini nikirudia suala lile lile langu la mwanzo kwamba *FDI* imekauka duniani, hata misaada ambayo tunaipata kwa washiriki wa maendeleo nayo imepotea. Sasa tukiondosha vivutio hivi taathira yake kwa uchumi wetu, sio leo. Kwa sababu unaweza ukazuwia kitu leo na ukakosa leo, lakini taathira yake ikaendelea kwa miaka 10,15 au 20. Je serikali yetu imefikiri vizuri. Tumefikiaje kwenye maamuzi hayo, tulifanya maamuzi ya kina kuelewa kwamba je, uwekezaji umeongezeka kwenye sekta ya utalii au umepungua, *interest* imeongezeka au imepungua.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa hilo. Ninakubaliana naye kwamba kazi kubwa imefanywa na kazi yetu ya kusambaza miundombinu, maji, barabara, umeme na huduma nyengine muhimu nazo imesaidia sana kupunguza mzigo kwa wawekezaji, kila pahali zinapitika, sehemu nyingi sana nchi yetu umeme uko karibu. Kuna tatizo la maji, lakini sivyo lilivyokuwa,

kwa hayo tunaipongeza serikali nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri, lakini namuomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri anisaidie kwa maswali yangu hayo matatu. Nina amini kwa yeye atatuweka pazuri, lakini tunamuomba atupe viashiria, atupe sababu ya serikali kufanya hivyo, ili sisi turidhike. Kama hatujaridhika tutaendelea kuzungumza naye na kumuhoji, ili tufikie pahali ambapo maamuzi ambayo tunayafanya humu ndani kwa kuisaidia serikali yetu yanakua yenye maslahi kwa nchi yetu, leo, kesho, keshokutwa na miaka kumi au kumi na tano ijayo.

Mhe. Spika, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuendelea kusisitiza umuhimu kwenye sekta ya kilimo, naamini inahitajika na naipongeza serikali kwa hayo.

Nikimalizia kwa mara nyengine tena Mhe. Spika, Muungano ni wetu sote na tunautaka, tunauheshimu na tunauhitaji, tukiwa viongozi wa watu nilishawahi kusema ndani ya Baraza hili hili, tunawajibu kuwa wa kweli kwa watu, tuna wajibu wa kuwaambia umuhimu wa Muungano huu watu wa nchi hii na tutakuwa watu wa ajabu leo tukizungumzia kuwa Muungano huu hauna faida kwa watu wa visiwa hivi. Lakini pia tutakuwa na watu wa ajabu zaidi tukiwazuwia na kuwashurutisha watu wa nchi hii na kuwaondoshea fursa yao ya kujitutumua, ya kujieleza na kuamua ni aina gani ya Muungano wanaouhitaji. Hiyo ni kazi ya wananchi, viongozi tuna wajibu wa kuwaonesha njia watu watakuwa na mawazo tofauti, kutofautiana kwa wanadamu ni jambo la kawaida, ndivyo alivyotuumba Mwenyezi Mungu. Ninawasihi sana viongozi wenzangu wa kisiasa watulizane, tuwe watu wa kuwaonesha wananchi njia, sio wakuchochea hisia potofu. Tuwaeleze yale tunayoamini kwa kuwaheshimu wenzetu, tena wote, ikiwa hapa tunajua sehemu mbili tu za siasa, basi nazungumzia CCM na CUF wote watumie busara na hekima katika kuwafika wananchi. Tusichochee fikra potofu kwa vyama vyote hivyo, kwa sababu wote wana makosa.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, naamini kwamba bajeti yetu ni ndefu tutakuwa na nafasi tosha ya kuuzungumza Muungano kwa kina sana na kutumia vipaza sauti hivi hivi kuwaelimisha wananchi juu ya kasoro, faida na muelekeo.

Lakini la mwisho kabisa nilipata taarifa kwa wenzangu hapa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad amefiwa na kaka yake. Nakuomba uniruhusu nitumie fursa hii kumpa pole yeye na familia yake, *Inshaallah* marehemu Mwenyezi Mungu atamlaza mahala pema, na familia yake Mwenyezi Mungu atawajaalia subira. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mansoor Yussuf kwa mchango wako huo. Muda uliobaki hautoshi kumkaribisha Mhe. Mjumbe mwengine kuchangia. Wajumbe ambao ninao katika orodha yangu ni Wajumbe wawili ambao nategemea watakuwa wa mwanzo kuchangia jioni. Nao ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Kwa hivyo, tuwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na wengine wote kufika kwa wakati ili kuendeleza mjadala huu wa bajeti ya serikali.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe, naakhirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:55 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaanza kuchangia Mhe. Spika aliacha majina ya watu wawili, kwa hivyo ninaomba au ninashauri kila mwenye nia ya kuchangia basi angeleta jina kabisa wanaotaka kesho na wale wanaotaka leo, ili tuweze kuweka utaratibu mzuri wa kuchangia na hivi sasa bado tunayo majina ya watu wawili.

Kwa hivyo, tukianza jioni hii kuchangia wa mwanzo ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadaye atafuatia Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwanza kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Suhuhanahu Wataala* aliyeniwezesha kusimama hapa na kuniazima pumzi zake hizi nikaweza kupumua na huu sio ujanja wangu wala uwezo wangu au akili yangu wala maarifa yangu, isipokuwa hii ni neema yake Mwenyezi Mungu na tunatakiwa kushukuru na kusema maneno *Alhamdulillah*.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sijakufanyia haki kama sikukupongeza wewe kwa kunipa fursa hii ya kuwa mtu wa mwanzo jioni hii. Vile vile nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa bajeti yake hii aliyotuletea. Pia nataka niwapongeze wakusanyaji wakuu wa fedha kwa upande wa Zanzibar akiwemo Kamishna Alhajji Abdi wa *ZRB*, nataka nimpongeze kwa dhati kabisa kutokana na utulivu wake, utendaji wake wa kazi pamoja na uadilifu wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Kamishna wa *TRA* Alhajji Mcha kwa utulivu wake pamoja na utendaji wake wa kazi.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imenikosesha usingizi pamoja na kupata kitanda kizuri Pwani Mchangani, lakini bajeti hii sijaona kama imemlenga mwananchi nasema kweli, isipokuwa imemkamua mwananchi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nianze na ukurasa wa 25 kuhusu hali ya uchumi wa Zanzibar kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba uchumi umekua kwa asilimia 7.5 kutoka asilimia 7 mwaka 2012, kuongezeka kwake uzalishaji wa ndani ikiwemo sekta ya viwanda na kilimo. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwamba kiuchumi viwanda hivi viko wapi na hapa tumebakia na magofu tu hivi sasa. *(Makofi)*

Kwa mfano, tulikuwa na Kiwanda cha Viatu hakipo, Kiwanda cha Sukari watu wananyang'anyiana mwenye uzio, mwenye kuni mwenye mua hakipo, Kiwanda cha Maziwa pia hakipo, Kiwanda cha Dawa hakipo, Kiwanda cha *COTEX* kiko wapi, Kiwanda cha Magodoro kule Karakana kiko wapi? Sasa hapa nadhani Mhe. Waziri angeelezea zaidi kuhusu viwanda ili wananchi wetu wakapata ajira na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora alisema hivi asubuhi alisema kwamba kuna wananchi karibu laki moja wamekosa ajira. Mhe. Naibu Spika, leo kuna fedha hizo hizo tunataka kununua meli basi nadhani tuangalie huu ununuzi wa meli na fedha hizi kama tungezitia kwenye sehemu ya sekta ya uvuvi tungefikia wapi, bila ya shaka nchi ingekuwa imepiga hatua.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba kuchangia eneo moja muhimu la wananchi wa Zanzibar kuhusu marekebisho ya sheria ya viwango vya kodi ambapo sheria 11 ambazo mwananchi hawezi kwenda kulala bila ya kukutana nazo zote, yaani akiamka akatokea upande huu atakutana nayo na akitokea upande wa pili atakutana nayo ukurasa wa 39 huo. Mhe. Naibu Spika, hapa ndipo mwananchi atakapokuja kuumia na hasa tukiangalia tunaelekea katika mfungo wa Ramadhani keshokutwa Mwenyezi Mungu akituweka hai. Kwa kweli kodi hizi zimekuwa kubwa na sijui mwananchi atafaidika vipi kutokana na kodi hizi. Vile vile kuhusu utekelezaji wa *program* ya kilimo Zanzibar, kuvuta uwekezaji wa kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo vidogo nchini, kuimarisha uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje atusaidie maelezo zaidi, kwa sababu sheria hizi zimekuja majuzi tu sio muda mrefu. Kwa mfano tukiangalia Sheria ya *VAT* Nam. 4

mwaka 1998, Sheria ya Ada za Bandari ni juzi tu tayari zimeongezeka tena, tutawaambia vipi wananchi wetu sisi huko tunakotoka.

Pia Sheria ya Kodi ya Mafuta ni juzi tu mwaka 2001 na leo tunakuja kuweka sheria nyengine hapa, hivi mwananchi atafaidika vipi hapa. Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Usafiri wa Barabara Nam. 2003 ni juzi tu sheria hii imeletwa. Kwa kweli sheria hizi zinawaumiza sana wananchi wetu, kwani kodi hizi ni zile huduma ambazo mwananchi zinamgusa kwa kila siku. *(Makofi).*

Hata hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kuiongezea serikali misamaha ya kodi na hivi ni vichochoro na watu wakapita kwa njia za *shortcut* na hapa amejitahidi sana Mhe. Waziri na hivyo naomba nimpongeze kwa dhati kabisa kwenye ukurasa wa 41.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kipaumbele cha bajeti mwaka huu ni pamoja na Sekta ya Maji, Afya, Elimu na *Program* za Ajira. Lakini hapa Wallahi Mhe. Naibu Spika, hapa ni mtihani mtupu hasa kwa Wizara ya Afya, nafikiri hatujawa *serious* kutaka kuwatumikia wananchi wetu. Kwa mfano, mwaka jana bajeti ya serikali kwa Wizara ya Afya haina tofauti na ile ya mwaka huu atapona mtu kweli, maana hata ukikaa ukipiga hesabu kwamba msamaha wa wazazi kwa Hospitali ya Mnazi Moja kwa siku ni karibu wazazi 50, hivi shilingi 40,000 x 50 = 2,000,000 sijagusa Pemba wala Makunduchi na hata Kivunge bado. Katika hali hii kweli afya ni kipaumbele au vipi au imekuwa ni wimbo wa taifa tu na watu wanalalamika kwamba maisha magumu. *(Makofi).*

Vile vile chakula wagonjwa ambao wako hospitali hawapati. Kwa kweli bajeti hii inamuumiza mwananchi na hii bajeti ya Wizara ya Afya ni ndogo na kuna kila sababu ya kuongezwa. Mhe. Naibu Spika, wakati wa kupitisha vifungu hapa kama sijapata jawabu ya kuongeza bajeti hii basi naomba uniruhusu nitoke nje na nitakuwa sijawafanyia haki Wizara ya Afya, itakuwa kama hadith ya Uganda wabunge walivyogoma hawakupitisha bajeti mpaka Wizara ya Afya ikaongezwe fedha. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, ukizingatia zaidi wachangiaji wetu wakubwa hivi sasa wameshaanza kututoroka au kutuponyoka ikiwemo *UNICEF*. Jambo la kusikitisha zaidi hapa tunazungumza kitu wala hatuna hakika nacho wakati huo nilikuwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kabla sijapata uhamisho 2.1 ni kiwango ambacho ni sawa na mwaka jana kupitia Mfuko Maalum wa *Basic Fund*, ambapo Serikali ya Zanzibar ilitakiwa kuchangia shilingi milioni 150 badala yake ilichangia shilingi milioni 30 tu, sawa na asilimia 20, wakati *DANIDA* walitakiwa kuchangia

shilingi bilioni 1.1 na wao walichangia shilingi milioni 500 sawa na asilimia 45.

Vile vile *UNICEF* walitakiwa kuchangia shilingi milioni 160 hawakutoa hata shilingi moja, pia walitakiwa kuchangia shilingi milioni 27,300 na wala hawakutoa hata kidogo. Kwa kweli maneno haya Mhe. Naibu Spika, si maneno yangu isipokuwa haya ni maneno ya Wizara ya Afya kuhusu mpango wa kipindi cha Oktoba na Disemba mwaka jana.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 45 kuhusu kuimarisha utaratibu wa utozaji kodi ya mafuta. Serikali imesema itafanya upembuzi yakinifu juu ya uwezekano na utaratibu bora wa kuwa na muingizaji mmoja tu wa mafuta (*single importer*).

Kwa kweli utaratibu huu Mhe. Naibu Spika ni ukiritimba tena wala haikubaliki na huu ni ubaguzi wa hali ya juu, kwa sababu biashara ni huru na mtu anayo haki ya kutumia uhuru wake na leo au kesho Mhe. Waziri anatuambia muingizaji mafuta awe mmoja na baadaye atatwambia muingizaji wa sukari awe mmoja, uhalali uko wapi na hapa mimi na-*declare my interest*. Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hii kesho kutwa anaweza kuja kutuambia hata mwenye kuweka meza marikiti awe ni mmoja tu. Kwa hivyo, hivi hatuwezi kwenda na huu ni uhuru. *(Makofi).*

Kwa mfano, kuna Kampuni ya *ZAT* imefanya kazi miaka mingapi na hivi sasa imekuwa ni mpizani wake mwengine. Sasa kila mtu anakula na wala huwezi kumpangia mtu leo ale wali au pilau, ni wali ule ule isipokuwa mapishi tu ndio yamebadilika. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie maelezo kama kuna njia imesafishwa ili aweze kupita mtu atueleze na hapa tunawekeza na sisi wengine tayari tumeshakopa mpaka fedha kutoka *PBZ* kwa ajili ya kununua meli kwa ajili ya biashara ya mafuta. *(Makofi).*

Sasa wakati atakapopewa mtu mmoja na hawa wawekezaji wengine wote wataondolewa na nafikiri hakuna hata Mzanzibari mmoja. Kwa mfano, *GAPCO* kutoka India, *Zanzibar Petroleum* kutoka Mombasa na wangapi hapa walikuwa na viwanda wameviondosha kwa kuangalia maslahi kutafuta njia ya biashara ya vichochoro, ili watu wapite. Vile vile ilikuwepo Kampuni ya *ECO-TEC* na mwisho wake iliondoka. Kwa hivyo, huu sio utaratibu mzuri, kwa sababu hii ni nchi na kila mtu anayo haki yake ya kufanya biashara na wala huwezi kumpangia mtu afanye hivi na vile na kwa maana hiyo tusitafute njia za mkato na wala hatuwezi kwenda hivyo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sitounga mkono bajeti hii mpaka nitakapopata maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika bajeti hii ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ambayo imewasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwanza nimshukuru kwa kutuletea bajeti hii mbele ya Baraza lako tukufu ambayo ni kazi au majukumu ambayo tumepewa na wenzetu wananchi wengi waliotuchagua huku nje. Vile vile kwanza nichukue fursa hii kuwaombea malazi mema wale wote walitangulia mbele ya haki na wale waliofikwa na misiba basi kwa kipindi hichi kigumu cha msiba Mwenyezi Mungu awape subira.

Mhe. Naibu Spika, nikienda moja kwa moja kwa ujumla bajeti hii ya mwaka huu yenye ongezeko kubwa kutoka shilingi bilioni 648.9 mpaka shilingi bilioni 658.5. Kwa kweli hii ni ishara ya maendeleo ambayo nchi yetu inapiga hatua licha ya changamoto tulizonazo. Pia nimefarajika na jina na madhumuni ya bajeti kuitwa bajeti ya huduma kwa jamii ya Zanzibar. Hali hii ni ishara tosha kwamba serikali imedhamiria kuleta mabadiliko ya kijamii Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo sasa niende kwenye mchango mzima wa bajeti sehemu ya 41 mpaka 42 ukurasa wa 28, ambapo umeelezea wazi juu ya umuhimu wa kuendelea na vipaumbele ili kuleta ufanisi. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni kama kuimarisha ajira kwa vijana. Kwa kweli ajira kwa vijana bado ni changamoto ambazo tunazo na lazima serikali ijidhatiti kwa kuwapatia ajira vijana wetu hawa.

Jambo la kuisaidia serikali ni kuanzisha elimu au vituo tofauti vya kuwakusanya watoto wetu ili kuwapa elimu mbadala. Kwa kweli vijana wetu hivi sasa ni wengi ambao wapo majiani huko na kutokana kuwa hawana kazi, basi huamua kufanya mambo mbali mbali ambayo yanayohatarisha maisha yao na pia huleta athari kubwa kwa wanajamii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande huu niseme kwamba ni lazima serikali ianze kuwatafutia maeneo tofauti na kuwakusanya kwa ajili ya kuwapa elimu, ili kuweza kujiendeleza kwa kufanya mambo mbali mbali ambayo yatakuwa ni endelevu kwao na hata kama hawakupata ajira nchini, basi wakati mambo haya ni ya amali wawe wanaweza kuajiriwa sehemu nyengine katika ulimwengu huu. Kwa mfano, Zanzibar tumo katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki basi na sisi tunayo haki ya kutafuta kazi sehemu mbali mbali. Kwa

hivyo, wajibu wetu ni kwamba vyuo hivi viwe vinatambulika ili wakati watakapotoka kwenda nje kwa ajili ya kutafuta kazi basi vile vyuo viwe vinatambulika.

Mhe. Naibu Spika, nimeona vipaumbele vyengine ni huduma za afya. Kwa hivyo, ni kuona namna gani huduma hizi za afya na hasa kwenye kupunguza vifo vya watoto kati ya umri wa mwaka 1 mpaka 5 ni kwa mujibu wa bajeti, basi mara nyingi kutathmini kwake ni kuona kwamba ni kiasi gani tumepunguza vifo vya watoto pamoja na mama wajawazito. Kwa maana hiyo, zitakapokuja wizara moja moja hapa nafikiri zitatufafanulia ni namna gani vifo vya mama na watoto vimepungua na hapo tutapata kutathmini ni namna gani vipaumbele hivi vya afya kwamba vimepiga hatua gani.

Vile vile kipaumbele ambacho ni tatizo kubwa katika Zanzibar yetu hii kwa ujumla ni tatizo la maji safi na salama. Mhe. Naibu Spika, ingawaje kuna fedha nyingi ambazo zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya maji. Kwa kweli tatizo la maji bado lipo na tunaiomba serikali na hasa pale jimboni kwangu tatizo hili la maji lipo. Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara husika kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba zile bajeti ambazo zimetajwa za maendeleo basi miradi ile iwe endelevu na kwa kila mwaka tunaona tunapitisha miradi mbali mbali ya maji safi na salama, lakini bado tatizo limetukabili pale pale. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba kama tutafanya kazi vizuri na kuondoa changamoto zile, basi nina hakika baada ya muda tutakuwa tunatizama mambo mengine ambayo nchi yetu itakuwa ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuwasilishiwa bajeti hii kwa upande huu wa maendeleo na kutuonesha vipaumbele vya bajeti hii. Pia naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa kupiga hatua kwenye kuimarisha mapato na kugundua na kukubali tatizo la udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wawekezaji. Pendekezo langu kwa serikali kwa vile imegundua udanganyifu huu, basi isimame kidete kwa ajili ya kuziba ufa badala ya kuendelea kupandisha kodi hasa katika masuala ya mafuta. Kwa kweli upandishaji wa kodi katika sehemu hizi ni kuwabebesha mzigo wananchi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa tuangalie mwelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2013/2014 inaashiria kuwa mfumko wa bei unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 7.9 mwaka 2013. Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe pendekezo kwa serikali kuendelea na *program* ya kilimo kwa kuwekeza kwenye *program* hii. Kwa mfano, wenzetu Bara hivi sasa wamefikia hata kuwaza kuwa na Benki ya Kilimo, basi na sisi ni vyema kujikita katika kuwawezesha wakulima na wafugaji ili matajario yetu yafanikiwe.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii nasema kwa mujibu wa Mhe. Waziri alivyotuwasilishia hapa na kwa mujibu wa mafunzo niliyopata tokea juzi, basi yananipa moyo na ninaweza kusema kwamba bajeti hii ni kweli ni bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli, hapa wananchi wetu watakuwa wanajiuliza na kusema kwamba pato la mwananchi binafsi limekua kwa asilimia ambayo imetajwa na Mhe. Waziri, kwanza lile pato la nchi ambalo ni kwa mujibu wa mafunzo niliyopata ni pato litokanalo na uzalishaji pamoja na matumizi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi kidogo kuhusu hili pato la taifa bado kwa wananchi wetu inakuwa ni tatizo. Kwa mfano, ukisema kwamba pato la mwananchi wa chini kabisa ni shilingi 960,000 kwa mwaka. *(Makofi).*

Kwa maana hivyo, hapa ni bado tunahisi kwamba kwa mujibu wa tathmnini hivi ni kitu vinathamini kwamba pato la taifa ni uzalishaji pamoja na zile nguvu na mtu mwenyewe binafsi na kodi kama nimefahamu. Lakini ukitathmini kwa mtu mmoja mmoja inakuwa ni kama ni ndoto tu, kwa sababu unamtathmini mtu mmoja mmoja kwamba kile kitu unamtathminia na wala hakiendi kwake yeye na hili ni tatizo ambalo tunalifikiria kwamba bado tunahitaji utaalamu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naona bado kumtathminia mtu *verbal* inakuwa bado haijaingia hasa kweli ile fedha inayotathminiwa hapa lakini kwa mwananchi mwenyewe hajafikia lengo lile pale. Mhe. Naibu Spika, niseme kwa ufupi kwamba bajeti hii ni nzuri lakini bado kutakuwa na changamoto ambazo kama kutakuwa na bajeti imepitishwa, basi ni vizuri zile fedha zipatikane kwa mapema kwa sababu ukizichelewesha fedha zile na yale uliyoyakusudia inakuwa vile vile ni tatizo.

Naomba niseme kwamba kama fedha zile zitakuja mwishoni kwenye miradi ile basi kwa kweli miradi inakuwa haifanikiwi vizuri na zile fedha pia mikataba yake inakuwa haiendani vizuri na inakuwa ya haraka haraka ya kuondoshwa njiani na kila siku tunakuwa nyuma na yale tuliyoyakusudia malengo hasa inakuwa hatuyafikii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niseme bajeti hii kwa mujibu ilivyowasilishwa na Mhe. Waziri naunga mkono hotuba hii mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii jioni ya leo na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mpango

wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuchangia lolote lile na mimi ningeomba unipe muda angalau wa sekunde mbili tatu kwa ajili ya kutoa pole kwa familia ya Marehemu Diwani Mstaafu wa Kwanza wa Jimbo langu Assaa Kheri Simai ambaye alifariki jana na kuzikwa leo kijijini Makunduchi, Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra wafiwa wote na ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. (*Amin*).

Baada ya salamu hizo za pole sasa naomba nianze kuchangia kwa kumtakia heri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mazungumzo yanazidi hotuba ya Mhe. Mjumbe. Kwa hivyo, naomba tuisikilize hotuba ya mwenzetu. Mhe. Mjumbe, endelea kuchangia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, naomba kumtakia heri na Mwenyezi Mungu Inshaallah ampe maisha marefu katika kuliongoza taifa hili la Wazanzibari na kuwaletea maendeleo siku hadi siku. *(Makofi)*

Vile vile naomba pia kwa dhati ya nafsi yangu nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa namna alivyotuwasilishia Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mwenyezi Mungu ampe nguvu na uwezo katika kulitumikia taifa kwa wizara yake aliyopewa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye michango yangu ambayo ni kama miwili mitatu.

Kwanza kabisa naomba nichangie katika suala zima la mwenendo wa uchumi wa Zanzibar katika pato la taifa. Mhe. Naibu Spika, katika suala la pato la taifa na hapa tumeelezwa kwamba pato limekua kutoka asilimia 7.0 mwaka 2012 ambapo mwaka 2011 ilikuwa ni asilimia 6.7. Kwa kweli mimi naomba nipongeze kwa hatua ambayo wenzetu watendaji wanaendelea kujitahidi na kuweza kukuza hili pato la taifa.

Lakini ningeomba nisaidiwe kwa sababu ya moja ya vitu ambavyo tumeelezwa humu vilivyochangia ukuaji wa pato la taifa kwenye ukurasa wa 9 kuhusu sekta ya viwanda. Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri lakini bado sisi tunahisi kwamba sekta ya viwanda ambayo

imesaidia ukuaji wa pato la taifa basi ninamuomba Mhe. Waziri kuna baadhi ya maeneo kupitia yeye na wataalamu wake wa kada za uchumi wajaribu kuangalia katika namna gani watawaweza kuviboresha viwanda ambavyo vinakwenda na wakati na ambavyo vitaweza kuisaidia nchi hii katika ukuaji wa haraka wa pato la taifa.

Mhe. Spika, sisi tuna rasilimali pamoja na kwamba ni chache lakini Mwenyezi Mungu ametujaalia. Rasilimali hizi imani yangu kama wachumi watajipanga na kama wachumi watakaa vizuri kutumia elimu yao, basi tunawaweza kuwasaidia wananchi wa nchi hii katika ukuaji wa pato la taifa.

Mhe. Spika, narudia tena tuendelee kuiangalia karafuu, baada ya kuuzwa karafuu basi tuangalie namna ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha machumi ambayo yanatokana na zao la karafuu. Ukiachilia mbali katika suala zima la mafuta ya karafuu, lakini bado kuna haja ya kuangalia kitu gani tunaweza tukakitengeneza, viwanda vya aina gani tunaweza tukaviweka kupitia zao la karafuu ili wananchi wetu waweze kufaidika.

Mhe. Spika, zao la karafuu ni sehemu moja lakini tulikuwa na Kiwanda cha Sukari cha Mahonda ambapo alipewa mwekezaji. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja labda atusaidie kiwanda kile kimefikia hatua gani au serikali ina mpango gani katika kukichukua kiwanda kile kujirejeshea wenyewe kama mikataba imekwishwa au umeongezwa. Namna gani serikali inaona kama kuna haja ya kiwanda kile kukichukua ili kuweza kuwa na viwanda imara na viwanda vitakavyokuwa endelevu katika suala zima la kujenga uchumi wetu.

Pia tuangalie uwekaji wa viwanda vidogo vidogo kupitia maeneo yetu ya matunda. Tunazalisha matunda mengi kama machungwa, ndizi na matunda mengineyo. Sidhani kwamba moja kwa moja kama tunaweza kuanzisha viwanda vikubwa, basi tuangalie angalau viwanda vidogo vidogo vya ushindikaji ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu na hususan katika maeneo ya vijijini. Mhe. Spika, hali ya vijijini na hali ya mjini ni tofauti kabisa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika suala zima la sekta ya kilimo. Tumeelezwa Mhe. Spika, kwamba sekta ya kilimo imeshuka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2011 hadi asilimia 1.3. Mimi nahisi bado hatujawa makini na hicho ndicho kinachotupelekea kutokuwa na mfumo madhubuti katika kusaidia mapato yetu ya taifa. Mhe. Spika, hebu tujiulizeni kuna nini Zanzibar, kwa sababu kila kile ambacho tunakianzisha baada ya sisi kusonga mbele siku hadi siku, sisi tunarudi nyuma. Hata ukiangalia katika sekta ya viwanda ukiangalia miaka ya 35, 40 nyuma tulivyokuwa tofauti na sasa hivi. Tulikuwa tuna viwanda vingi, viwanda vya ngozi, viwanda vya viatu,

viwanda vya sukari, viwanda vya kutoa vifaranga nakadhalika. Sasa na katika suala la kilimo na wao tunaanza kurudi nyuma kidogo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri watu wote hususan kada ya uchumi naomba wajaribu kuangalia zaidi hasa watumie elimu zao katika kulisaidia taifa hili. Leo sifikirii katika suala zima la kilimo, nimetafuta kwenye vitabu humu sikuona, nimejaribu kuangalia katika kurasa zote katika suala la kilimo, labda tuambiwe kwamba nchi hii kwa mwaka uliopita au miaka miwili iliyopita basi tumezalisha muhogo tani 20 au tumezalisha ndizi au viazi vitamu tani 10. Ili tuone namna gani wapi tumepungua na namna gani wapi tuongeze jitihada ili tuendelee. Sasa wataalamu watusaidie katika suala zima la kuwa na *data* za kilimo na kuangalia tumefeli wapi na nini tufanye.

Mhe. Naibu Spika, huwa sipendi kutoa mifano lakini serikali inajitahidi kutupa elimu. Nimetoa mfano juu kwamba wenzetu walifanya utafiti mtu ambaye aliyekuwa akitoa nusu tani, unafanyiwa utafiti na kupata taaluma kwamba mtu yule baada ya kutoa nusu tani anakuja anatoa tani moja. Wamefanya utafiti baada ya kutumia eneo kubwa kwa kuzalisha mazao, sasa hivi wanatumia eneo dogo kwa kuzalisha mazao mengi. Sasa lakini hawa wenzetu sijui wanafanya utafiti wa aina gani, ripoti zenyewe hatuzielewi, kinacholimwa hatukijui. Hili nalizungumza kwa sababu ya tahadhari kubwa Mhe. Spika, kwamba serikali yetu ina nia njema na inatumia fedha nyingi sana kuwapa Wizara ya Kilimo.

Mimi nafikiri kwamba kama tutakuwa na mahesabu imani yangu bora zile fedha tunazoziingiza katika Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kulima basi bora wangelipewa wananchi huko vijijini wangelinufaika, kuliko kutumia fedha zile kwa ajili ya kupewa wakulima, kilimo chenyewe hakieleweki.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi kwa imani ya dhati ya nafsi yangu tunasema maeneo karibuni matatu ambayo tunakuwa tunayaweka kwa ajili ya ndugu zetu wa Wizara ya Kilimo, kuna sehemu ya mishahara, tunawapa kilimo, tunatafuta vitendea kazi siku hadi siku, tunawapa kilimo, pesa za wafadhili hata hazieleweki tunawapa kilimo, lakini kukusanya mapato yote ambayo wanapewa kilimo. Faida ya matumizi na tunachokipata kinakuwa tofauti.

Mimi nahisi kwamba itafika pahala kuna siku tutasema hizi fedha zote za wahisani, za mishahara ya Wizara ya Kilimo na pembejeo za mambo ya matrekta. Basi bora wakati wote wawe vijijini watulie kuliko kuwa tunazipeleka halafu hicho kilimo chenyewe hakionekani. Vyenginevyo itakapokuja bajeti ya kisekta hapa basi Mhe. Waziri labda atakuja kutwambia kwamba mpunga tani ngapi, wananchi wamefaidika vipi, muhogo tani ngapi, lazima tujijue wapi tunatoka na wapi tunakwenda Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika suala la ulipaji wa kodi. Mimi nishukuru sana jitihada za Mhe. Waziri, watu wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Tuna imani jitihada zake zimepelekea kutufikisha hapa tulipo kwamba serikali imekwenda haikupata kuyumba pamoja na mapungufu ya kibinadamu madogo madogo. Lakini tunaamini kwamba masuala ya mapato katika nchi yetu yameweza kuongezeka. Lakini bado nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na jitihada zake ambazo anazifanya, pamoja na nia yake njema ambayo kaieleza, mwaka jana wakati nachangia bajeti hii niliomba kwamba tuondokane na tabia ya kimazoea tuende katika nyanja za kileo.

Mhe. Naibu Spika, masuala ya utoaji wa fedha kwa njia za vikapu umepitwa na wakati, tutafute wataalamu wakulipia fedha katika vyombo vya benki. Bado suala hili katika baadhi ya taasisi tunakwenda nalo. Mtu anachukua kapu soko la Mwanakwerekwe anapanda kwenye gari anakwenda na kapu katika Baraza la Manispaa. Hii inachangia masuala ya mianya ya wizi, hakuna mtu ambaye atachukua kapu la pesa azione aziache kuzichukua. Mhe. Naibu Spika, nikuombe ufanye jitihada ya kutafuta njia ya kitaalamu ili kuweza kuona namna gani serikali yetu inalipa kodi kwa sababu ya kutumia njia ya vikapu mikononi.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili hili pia ningekuomba tujitahidi katika suala la kada ya uhasibu kuona kwamba watu hawa hawakai muda mrefu katika maeneo na hususan katika maeneo nyeti ya kukusanya mapato. Bado baadhi ya maeneo kuna wahasibu, kuna watu wa manunuzi kuna ma-*auditor* bado wanakuwa muda mrefu. Suala hili haliendi kwa haraka linakwenda kwa kusua sua, labda umzungumze mtu maalum. Ukipiga kelele kwamba mahali fulani kuna mtu fulani ndio utaambiwa kwamba anafanyiwa kazi. Lakini ule utaratibu wa kifedha bado haufanyiwi kazi ipasavyo katika kueleza kwamba wahasibu kama wahasibu wanakuwa na hali ya mzunguko kwa ule utaratibu wa kisheria ambao mmejiwekea. Hili bado lifanyiwe kazi ili liweze kusaidia serikali yetu iweze kukusanya mapato kwa nguvu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzi katika masuala mazima ya vipaumbele ambavyo nimevitaja. Nikushukuru na ninaimani wananchi wetu watafarijika na hili na ndilo tunalolihitaji. Katika mambo muhimu ambayo mwanadamu anayahitaji ni mambo matatu, mwanadamu anahitaji apate elimu, afya na apate mali kila siku. Lakini bado mimi najua kuna nia njema lakini mara nyingi tunasema katika Baraza hili kwamba baadhi ya viongozi wetu wana nia njema lakini baadhi ya viongozi wenzetu hawana nia njema na serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, itakapokuja bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati, kwenye Mamlaka ya Maji, mimi binafsi yangu kazi itakuwepo. Kwa sababu bado siridhiki kabisa na utendaji wao na laiti kama ingelikuwa inawezekana hizi 55.4 bilioni basi bora zingeliingizwa katika mfuko wa maendeleo wa Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo basi tungenufaika na tungeona kwamba pesa hizi zimeleta manufaa gani. Kwa sababu kama utafanya uchambuzi yakinifu katika majimbo, maeneo yote majimbo ya Mkoa wa Mjini/Magharibi, nazungumza kwa ushahidi kwamba maji yanapatikana kupitia visima vilivyochimbwa na Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge na sio maji yanayopatikana kutoka Mamlaka ya ZAWA.

Sasa hii ni jitihada ya Waheshimiwa, huu ndio uaminifu waliouonesha, sasa kama kuna mapesa bora tuwape Waheshimiwa wakachimbe visima katika maeneo yao, kuliko kupeleka sehemu watu wanatafuna. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tuna mradi mkubwa hapa wa maji, tukaambiwa Mkoa wa Mjini/Magharibi, maji ndani ya kipindi hichi kutakuwa hakuna tatizo tena. Mabilioni ya wafadhili yalitumika pale pesa za walipa kodi. Kila siku Mamlaka kazi yao kukopa, kazi yao kuchukua pesa serikalini, kinachoendelea hakuna. Hizi pesa waelewe pesa zinazotumika ni pesa za wananchi, pesa za watu wanyonge, walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri bado nakuomba sana pale ambapo tunapeleka fedha za serikali basi tuhakikishe tunawasimamia ipasavyo na kile tunachokilenga basi tuoneshe mafanikio. Vyenginevyo hali itakuwa tete na kwa ukweli tunawapa unyonge wananchi wetu. Tuna nia njema ya serikali. Nasema tena kwamba kuna watu wanajitahada ya kuisaidia serikali hii na ndio maana vinazidishwa viwango vya mapato na ndio maana mmezidisha kasi ya kuzidisha mapato katika masuala ya maendeleo. Lakini tuna haki ya kusema hayo maendeleo bado hawajawa tayari kuifanyia serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie haraka haraka na mambo kama mawili tu. Kwa bahati katika ukurasa wa 47 kifungu (h) (66) nimekieleza namna ambavyo kimelenga katika kusaidia kuongeza mapato ya taifa la nchi hii. Katika ukurasa huu lile toleo ambalo nahisi ni muafaka kwa magari yanapoingia nchini, basi husajiliwa bandarini. Ni vyema na sisi tunaliunga mkono.

Nataka nitoe indhari moja tu. Wafanyabiashara wetu mara nyingi wanakuwa wajanja na ujanja wao ni katika masuala mazima ya kutozwa kodi. Sasa umejitokeza mtindo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaoingiza magari, huingiza magari vipande vipande, huingiza magari ambayo yamechoka wakitoa pale nje yanakuwa *scrap*. Huu ni ujanja ambao unatumika ukifika

pale unaambiwa gari *scrap* lakini mtu kashusha gari mpya lakini watu wanatafuta njia ya kukwepa kulipa kodi.

Sasa kwa mujibu wa taratibu magari yote kabla ya kusajiliwa basi taasisi inayohusika na usajili ni taasisi ya Miundombinu. Hili sijui Mhe. Waziri umejipanga vipi, baina yake yeye na Wizara ya Miundombinu kuweka wataalamu bandarini katika kuangalia hali halisi ya magari ambayo yanaingia bandarini ili tusije tukawa huku tumeamua kuongeza kodi, lakini ikawa tunakuja kuwaletea maafa wananchi wetu. Maana mtu akiona gari yake imeshasajiliwa anatoka mbio lakini kumbe gari lile limekuja na dhamira nyengine, ubora halina, hatulijui hali yake likoje kwa afya ya wananchi wa nchi hii.

Nataka nikuombe kwa dhati kabisa katika suala hili na nia njema ambayo umeipanga Mhe. Waziri basi tuanze mapema kushirikiana na taasisi inayohusika kuona kwamba pale tunaweka kitengo, kwa kuwatumia wataalamu ili kuiangalia hali hii na kuangalia wale ambao wanaofanya ujanja katika suala zima la ukwepaji wa kodi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa msemo wa Kiswahili na wewe ni mwana Mapinduzi mara nyingi anampenda Shaban Robert. Mimi nasema ninde kwa wazee wa kiasili jinsi walivyokuwa wakitumia misemo ambayo ilikuwa ina maana na ina faida na tija kwa lile ambalo walilokuwa wanalizungumza. Wazee walikuwa wanasema kwamba 'Tukithubutu tunaweza"**,** kwamba kama tutakuwa tayari hakuna jambo ambalo linaweza kutushinda.

Mhe. Naibu Spika, msemo huu nautolea mfano katika taasisi ya serikali ambayo ilithubutu na ikaweza na kwa kweli taasisi hiyo yule kiongozi Mwenyezi Mungu ampe nguvu na ampe maisha marefu mahiri na ampe maisha marefu katika kuisaidia nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bandari mnamo mwezi wa 9 mwaka 2012, kulitokea mabadiliko ya Mkurugenzi. Lakini tuangalie ndio kule ninapomwambia Mhe. Waziri tusikae muda mrefu, hapa kahamishwa Mkurugenzi tu, lakini Mkurugenzi anayekuja na yeye kaamua kufanya *reshuffle* katika kada zake zote za ndani. Nini kimepatikana, kaangalie *data*, ndani ya miezi mitatu Shirika la Bandari limeweza kuongeza mapato yasiyopungua milioni mia moja, ndani ya miezi mitatu mpaka mwezi wa Septemba kuja Disemba kuondoka kwa Mkurugenzi na kuja mwengine. Sasa hii Mhe. Naibu Spika, utakwenda kuiangalia wenzangu wananinyooshea vidole vitatu kwamba sio mia moja ni milioni 300.

Hii ni taasisi moja lakini kuna taasisi nyengine ambazo kuna hawa wahasibu wanaokaa wanahisi kwamba hizo ndio wizara zao na ndio milki yao. Sasa kama hii tumeweza kupata kima kama hichi kwengine kuna kima gani. Mhe. Naibu Spika, nasema tena yule Mkurugenzi aliyokuwepo pale namuombea kila la kheri Inshallah kwa nia yake njema.

Mhe. Naibu Spika, ongezeko hili la milioni mia wenzangu wanasema mpaka mia tatu taasisi ile imeweza kuwasaidia wanyonge wa Mungu, wafanyakazi wa taasisi ile. wafanyakazi wa chini wa Shirika la Bandari kuongezwa mshahara asilimia 60 ndani ya kipindi hichi kifupi. Kwa sababu baada ya kukusanya wakajihisi wanaweza na vifaa vikapatikana na mambo yanakwenda mazuri na taasisi imeanza kubadilika, ukiachilia mbali na mikono ya wafadhili wetu kama ndugu yetu Bakharesa mambo ya bandarini *Alhamdulillah.*

Mhe. Naibu Spika, hii ndio hali halisi. Nasema tena Waziri ana nia njema, Waziri ana ukweli, Waziri ana nia ya kuisaidia serikali hii, lakini baadhi ya watu huko chini bado hawajawa tayari kubadilika. Sasa kwa ushirikiano wako na wetu sisi bado tutaendelea kupiga kelele kwa maslahi ya nchi hii na kwa maslahi ya taifa la Wazanzibari katika kumsaidia kazi Mhe. Rais wetu Dokta Ali Mohammed Shein ili kumpa wepesi katika kazi zake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo na mimi naunga mkono hotuba hii ya Makadirio ya Mapato iliyowasilishwa na Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani. Nashukuru sana kwa kunipa muda wako. Ahsante.(*Makofi*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunichagua jioni hii niweze kutoa mchango wangu mfupi sana ikiwezekana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani na kwa niaba ya Wazanzibari wenzangu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Fedha, kaka yangu Omar Yussuf Mzee, kuanzia Micheweni hadi Makunduchi hakuna asiyemjua juu ya umakini wake, ustaarabu wake na uwezo wake wa kuongoza kila anapowekwa kwenye serikali. Lakini unaweza ukawa kiongozi mzuri lakini ukashindwa kuongoza kwa sababu ya nyenzo. Nyenzo maana yake ni yale mambo ambayo unapangiwa kwa ajili ya kuongoza. Wazanzibari wanamjua kaka yangu huyu ni mzuri lakini nadhani tunamuangusha kwa sababu hana nyenzo za kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi napingana kata kata na wale wanaosema kwamba bajeti hii nzuri, kwa maslahi ya Wazanzibari. Kama mzuri Waziri naunga mkono kwamba waziri wetu mzuri mara mia na kwa busara aliyonayo siwezi

kuuliza swali hata moja. Lakini uzuri wake yeye hautokuwa uzuri wa bajeti hii kwa sababu yeye ni sehemu ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nathubutu kusema kwamba bajeti hii si nzuri na ina hatari kubwa kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar wanyonge. Nasema hayo kwa sababu nataka ni- *prove* maneno yangu.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana Mhe. Waziri alitutajia maeneo ya kipaumbele wazi wazi na akaelekeza jinsi ya kuyatekeleza. Bajeti yetu mara hii na kwa sababu makadirio hayakutekelezeka mara hii ameshindwa kuyataja na akasema kwamba ni yale yale mengine, kwa sababu mengine ni ya muda mrefu. Ni lugha tu ya kitaalamu lakini ameshindwa kutekeleza ya mwaka jana.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana ilikuwa moja kati ya kipaumbele ni maji. Bajeti ya maji iliyopita ilitumia zaidi ya bilioni 32, mara hii serikali imetenga bilioni 58. Kwa bilioni 32 hakuna maji zaidi ya wale Wawakilishi waliochimba na naamini kwa bilioni 58 hakuna maji zaidi ya wale waliochimba.

Mhe. Naibu Spika, tumsaidie Mhe. Waziri afanye kazi kwa kuwajibika, watendaji wa serikali ambao Mhe. Rais amewaamini kwamba nyinyi mchukue majukumu haya. Mhe. Naibu Spika, leo wataalamu wetu wameshindwa kuoanisha baina ya vipaumbele vya mwaka jana na mara hii, kitabu hiki kimetia maneno ya juu mno na huwezi kuchambua vipaumbele ambavyo serikali hii mwaka huu wamevitenga.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana Mhe. Waziri wamekiri kwamba haukuwa mzuri. Haukuwa mzuri kwa sababu ya mapungufu ya fedha za wahisani. Mimi naomba akija anijibishe ni kiasi gani ya fedha za GBS 4.5 ambazo hadi leo zimekwama Tanzania Bara kuingia hapa. Mhe. Waziri atwambie ni kiasi gani cha fedha ambazo zilizokwamba za GBS 4.5 ambazo zimeathiri bajeti yote ya maendeleo ya mwaka jana zimekwama Tanganyika au kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Waziri atwambie ni kiasi gani cha fedha chake yeye ambacho kimekwama hadi hii leo hakijapatikana na hicho ndicho ambacho kimeathiri bajeti yetu ya maendeleo kwa mwaka 2013. Ikiwa fedha imekwama Tanzania Bara itapatikanaje Italiy, Hong Kong, itapatikanaje Marekani.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kungekuwa na nia ya karibu ya kusaidiana eti mtandao tu ndio unaosababisha fedha ya maendeleo isingie Zanzibar,

mtandao tu. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri tumsaidie. Mimi niombe tu Mhe. Waziri wa Fedha aendelee kuwa muwazi si mtu mwenye utata husema kwa uwazi, jambo likimkaza na hana siri kwenye wajibu. Atwambie tatizo ni nini ili Wawakilishi hawa 82 ndio ambao watamlinda, asiogope aseme ukweli. Wazanzibari wanamtegemea kwamba yeye ni kioo, wako wengi mmoja ni mimi, sina mashaka nikiambiwa Mhe. Omar Yussuf Mzee kuwa Rais wa Zanzibar. Kwa hivyo asiogope kusema kwa kuwalinda wachache, atwambie tatizo ni nini.

Mhe. Naibu Spika, bajeti imeathirika si kwa sababu ya kwamba wahisani wamekataa ni kwa sababu mbili kubwa. Kwa sababu wahisani hawatuamini baadhi yetu ni wezi, lakini pili wenzetu Watanzania Bara suala la GBS limechelewa kuingia Zanzibar. Zote si sababu za msingi. Mhe. Waziri atwambie tatizo nini? Ili tumsaidie na ule ufanisi ambao mimi namuamini sana aweze kufikia.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii nikiri kwamba leo taifa limeongezeka, limefikia bilioni 252.3 ni sawa sawa na asilimia 68.6 ya pato la taifa. Maana asilimia karibu 20 ya pato la taifa ni deni la taifa. Ukigawa hili kwa takwimu za Wazanzibari, kila mtu ana mamilioni ya fedha ambayo anadaiwa.

Mhe. Naibu Spika, moja ambalo nimelizungumza na Mhe. Waziri kwamba hili ni la taifa ni la madeni ya kiinua mgongo. Nasema kwa sauti pana kwamba viinua mgongo ambavyo vinalipwa Zanzibar baadhi yake si sahihi. Kuna watu wanaingiza mkono wao na wanakula fedha za umma. Lakini haya tutayazungumza baadae tukifika Wizara ya Fedha na Wizara ya Utumishi kwamba kuna watu wanakula fedha ya umma kwa kisingizio cha kiinua mgongo. Serikali inawajua na kama hawawajui wakubali tuwambie na wachukue hatua haraka. Deni hili limeongezeka kwa sababu kuna watu wachache wanatumia hilo kama ni mtaji wao.

Mhe. Naibu Spika, namuamini Mhe. Waziri kwamba yupo tayari sisi kumsaidia lakini tukimsaidia akubali wale walioharibu fedha ya umma basi awachukulie hatua. Kuna watu wamefoji nyaraka za viinua mgongo feki, leo matakwa ya watu fulani yamekuwa ni deni kwa mtu wa Muwambe na Makunduchi, ni hatari kubwa. Hii ni hatari kwamba leo serikali tumewaamini watu wafanye kazi kumbe wanatula, wamegeuka makabaila, wameweka mrija wananyonya mali za wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, deni hilo la Taifa la kiinua mgongo si sahihi limesababishwa na watu wachache ambao wana nia mbaya na serikali hii kwa ajili ya kudhoofisha maendeleo ya nchi hii. Mhe. Waziri amesema madeni yenye kuendelea na anasema hapa kwamba deni la ndani ni bilioni 44.3 la

nnje ni bilioni 208.8 na deni la viinua mgongo ni bilioni 5.1 ambalo mimi nasema kwamba deni hili limesababishwa na watu wachache kwa maslahi yao. Serikali mimi niwaombe Wawakilishi wenzangu mwaka huu wakubali kubadilisha watu, hatuwezi kila siku kuona watu wanakula fedha hakuna hatua. Mtoto wangu mimi akiwa mwizi mara ya kwanza nikimvumilia, mara ya pili nikimvumilia, maana yake nimemtuma. Mimi nashauri kwamba serikali ichukue na iiwajibishe wale wote ambao wamezoea kula mali za umma kwa misingi ambayo si sahihi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye maeneo ya viwanda. Mimi nakataa tena kwamba dunia ya leo karne ya 21 ya sayansi na teknolojia boflo, kidani, hivyo vyote si viwanda. Dunia ya leo karne ya 21, huwezi kujigambia kwamba una kiwanda cha boflo, herini, kidani, kokoto na mchanga kuwa ni viwanda kwa kweli kama ni viwanda ni aibu. Mzee Jumbe na Mzee Karume wameondoka hapa madarakani wakiacha viwanda zaidi ya vinane, wataalamu wetu wameshindwa kuviendeleza viwanda vinane tena leo wanatwambia kiwanda ni cha kokoto. Hivi ndivyo ilivyo kwa viwanda vya sukari, kiwanda cha nguo, *COTEX* nakadhalika, vilikuwepo hapa na vimeuliwa. Mimi mategemeo yangu kwamba wataalamu wetu wangevihuisha viwanda vile tungesonga mbele, lakini vimeuliwa leo Wazanzibari wanadanganywa wanaambiwa eti boflo pale Amani ni kiwanda.

Mimi sikubaliana na hilo na nitakataa mwisho wa nguvu zangu kwamba bekari ya kutengeneza boflo, si kiwanda. Nadhani Mhe. Waziri angetwambia kwa nini wataalamu wake wameshindwa angalau kukiendeleza kiwanda kimoja. Leo ni mwaka wa tano huu Mahonda watu wanagombana, wengine wanahamu ya miwa, wengine waya, wengine magari, ugomvi tu baada ya kukaa wakawaendeleza wenzetu wale wa Mahonda, wakazalisha sukari kwa maslahi ya Zanzibar, watu wanagombana tu. Baada ya kwisha wanaambiwa kubalini kokoto, mchanga, boflo, chapati, vyote ni viwanda. Hivyo si viwanda.

Mhe. Naibu Spika, hii leo mimi niko mwaka wa saba na nusu, nimekuwa nikisikia kwamba Pemba sehemu ya Micheweni ndio maeneo huru ni maeneo ya kiuchumi. Lakini Mhe. Waziri atwambie wamewekeza nini Fumba, hakuna miundombinu, hakuna barabara, maji, umeme, eti ni maeneo huru ya kiuchumi nani fedha yake atakaeiwekeza Fumba wakati hakuna huduma ya miundombinu.

Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali isiwadanganye wananchi, ikubali kwamba haijaweza kuwahudumia wananchi na inavyozungumzwa hivyo ni maneno ya kudanganyana na ni maneno ya nadharia. Mimi niwaombe sana waheshimiwa wenzangu wakubali kwamba mapato yapo lakini hatujakuwa tayari kuyatafuta

mapato ya nchi. Ama *ZRB* wamekuwa wavivu mno na wamebakia ofisini kusubiri mtu aje alipe, ndugu yangu amesema hapa kwamba leo asubuhi mfanyabiashara aje pale na kapu yake alipe fedha. Lakini fedha hutafutwa kwa kuihangaikia, wenzetu hawa wamekuwa wakikaa ofisini na kusubiri mapato.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba aviangalie Mhe. Waziri viwango alivyovitaja vya mapato kwa haraka sana. Cha kwanza kuna kodi za huduma simu, kwa mfano kuna Kampuni ya Tigo makao makuu yake yapo Dar es Salaam wanalipa ile huduma ya usajili wa kampuni. Lakini ndani ya nchi hapa Zanzibar kila pahala kuna wakala wa huduma za simu za kutuma pesa, wale wanatuma pesa bure bila ya mapato kuingia serikalini. Serikali ingekuwa makini na inakusanya mapato hivi tunacheza na mapato. Lakini tumeshuhudia vile vile huduma za ushauri hapa kuna makampuni mengi ya ushauri *consultance companies* ziko nyingi tu. Lakini zaidi ya malipo ya usajili mahkamani au makampuni watwambie kwa nini hawachangii kodi za wananchi wa Zanzibar na badala yake serikali ikubali kuwanyonya wanyonge wa Muambe, Makunduchi na Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, jengine kodi ya ardhi ambayo Mhe. Waziri leo amesema tupendekeze, malipo ya kodi ya ardhi si sahihi. Mimi ninapendekeza kwamba kodi yoyote ya ardhi basi igaiwe mafungu matatu.

Fungu la kwanza wapewe wananchi husika, kwa mfano jana tulikuwa Matemwe kule watu wamejenga hoteli nzuri lakini wanatumia wenyewe hawana wanachokipata. Fungu la pili Mhe. Naibu Spika, serikali ichukue kodi ya ardhi kama ni mtu wa pili na fungu la tatu achukue muekezaji. Kwa nini Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hivi sasa wawekezaji wale wakiondoka wanatuachia magofu lakini fedha yote imekwenda kwao. Mimi nashauri kwamba kodi ya ardhi ibadilishwe mapato yale ya kodi ya ardhi 2013 iwe wananchi waweze kupata manufaa hayo.

Mhe. Naibu Spika, suala la mafuta, serikali inapendekeza kuwa na *single importer*, mimi nakataa vile vile, hatuwezi dunia ya leo kuwa na *single importer* na nina hakika huyo mtu serikali wanamjua wamemzulia huyu ndiye *single importer* hatuwezi kwenda hivyo. Wenzangu wamesema leo mnataka kubinafsisha mafuta, kesho mtafanya *single importer* ya madawa, keshokutwa wa sindano, keshokutwa maji ya kunywa hatimae kila kitu basi ni *importer*. Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hili tusilikubali kata kata hii ni hatari kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, leo tuna kampuni nne hapa. Kuna *GAPCO* tunaambiwa ya wahindi mimi hata siwajui, kuna kazi ya *petroleum*, kuna na Puma. Haya yote

ukikusanya kwamba tuwe mtu mmoja badala kuzalisha *monopoly* katika nchi jambo ambalo si sahihi katika dunia ya leo. Mimi ninawaomba wawakilishi wenzangu suala hili Mhe. Waziri atusamehe tuikatae kwa sababu lilikuwa mbele ya ukiritimba kwa maslahi ya Uzanzibari wetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo mimi nalikataa ni malipo ya leseni ya njia. Mhe. Naibu Spika, serikali imependekeza kwamba hivi sasa ili kudhibiti wale wasio leseni na wajanja, maana yake kila lita sasa hili posho liwe 35, nimefanya hesabu ndogo tu Mhe. Spika, kwamba mtu ambaye anatumia lita kumi kwa siku gari kama yangu kwa mwaka mmoja maana yake atalipia shs.126,000 kama ni *road licence.* Hivi leo mimi nalipia shs.60,000 ninazidishiwa mara mbili na nusu. Daladala Mhe. Naibu Spika, hivi sasa daladalani shs.70,000 daladala akipewa lita 60 kwa siku kwa maana yake kwa mwaka shs.378,000 unapandisha kodi ya daladala mara 4 maana yake nini? Maana yake abiria sasa badala ya shilingi 250 itakuwa shilingi 1000 Mzanzibari hiyo haiwezi. Mhe. Naibu Spika, vile vile hilo ninalikataa ni hatari kwa wananchi hasa wanafunzi wetu watashindwa kusoma kwa sababu mapato haya yatasababisha ongezeko la nauli kwa Wazanzibari wanyonge.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna gharama za jumla pia zimeongezeka kutoka asilimia 100 ya mwaka jana hadi asilimia 300, maana yake imepanda mara tatu bima yake. Sasa ikiwa gari moja kwa hiyo itakuwa shilingi laki nne na Bima yake laki tatu, maana yake laki saba hiyo ni gharama ya daladala moja kwa mwaka.

Maana yake nini? Maana yake milioni sita hii itasababisha kuongezeka kwa gharama za nauli kwa wananchi wetu, leo tujiulize nani Zanzibar ambaye hana wanafunzi wawili watatu kwenye nyumba yake. Utawezaje kutoa nauli shilingi elfu tatu kila siku kwa wanafunzi watatu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mimi ninamuamini na ninaamini kwamba ana nia safi lakini kodi hizi ni hatari sana kwa Wazanzibari, na tungekaa tukajipanga na wataalam wetu tukatafuta vyanzo vyengine vya mapato ili tuwasaidie Wazanzibari wetu. Lakini kodi hizi mbili za *road license* itagharamia sana itaendelea sana gharama za mafuta, na kwa hivyo gharama ya usafiri kwa Wazanzibari wetu zitakuwa ngumu na maisha yatakuwa magumu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba serikali haijakuwa tayari kutafuta mapato, kwa nini nikifuata tafsiri ndogo tu hapa kwamba kuna kampuni hii ambayo imefilisika ikaondoka, kuna hoteli *Venta Club, Venta Club* hadi inaondoka hapa ilikuwa na deni la dola laki tatu za *ZRB, ZRB* ipo ukimwacha akilimbikiza mpaka anafika dola laki tatu ni sawa sawa na milioni mia nne na amefilisika, ameondoka ametwachia mzigo. *ZRB* ipo, *TRA*, *Income Tax* walikuwa na deni la dola laki mbili sawa na milioni 500 na zaidi,

wameondoka kafilisika *TRA* ipo lakini *land lease* ambayo sisi ametuachia deni lake dola 170,000. *ZRB* ipo na jamaa ameondoka.

Mhe. Naibu Spika, jamaa huyu pia ameondoka na deni la dola laki nne na kumi za wananchi *suppliers* ambao walikuwa wakipeleka chakula na ameondoka, hii ni sawa sawa na milioni 700. Aliondoka ZRB ipo, serikali ipo jamaa yupo Italy. Mhe. Naibu Spika, ninasema tena ziko hoteli kama hizi nyingi tu ambazo huu ndio ujanja wao. Hivi sasa kuna hoteli inaitwa *All My Blue*, *My Blue* kuna hoteli inaitwa Baobao. Hivi sasa tayari wamebadilisha jina wanaita *Bein Hotel*. Ni ujanja wao kwamba akiona deni ni kubwa baada ya kuitwa baada ya kutambua sasa anaitwa Juma na nina hakika *ZRB* wanajua.

Baadae hoteli hii iko Nungwi alipoona ana deni ameamua abadilishe jina anaita *Bein Hotel* mnampa tena *lease*, mnampa tena msamaha wa kodi hasara kwa serikali. Sasa kama serikali haijui hivi ndio tunaambiwa wachukuwe hatua, kama hawachukui hatua maana yake ni *deal* ya watu fulani ndio maana yake. Unaambiwa jamaa huyu mwizi humkamati maana yake umemtuma. Nasema kwamba lazima tuchukue hatua, hatuwezi kuwanyonya wananchi wakati mapato hayapo, Mhe. Waziri ninakwambia kweli watu wanabadilisha majina kwa sababu ya maslahi yao akiona kwamba kuna mwanya anabadilisha jina, anakwambia maana yake hoteli imekufa, kwa hivyo tunaanza upya, hatimaye mapato yanapotea ovyo ovyo. Wewe kama Waziri wa Fedha kazi yako kutafuta fedha basi unaamua kuongeza kodi kwa wananchi wanyonge.

Mhe. Spika, mara zote Wawakilishi na Mhe. Mshimba amekuwa akisema kwamba kama wataalam wetu wameshindwa kazi watwambie tuwasaidie lakini lazima tuwasaidie ili wananchi wetu wasinyonywe kwa sababu ambazo hazina msingi wowote.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa kusema kwamba sehemu nyengine ambayo napendekeza kwamba tuangalie kodi ya mapato Zanzibar tusiongeze kodi, tukiangalia mjini petu hapa hasa maeneo ya Mbweni na maeneo ya kitajiri haya, watu wanakodisha kwa mwaka milioni sita kwa dola. Serikali ipo kimya haitozi kodi anasubiriwa mwenye daladala akenda na kurudi alipe kodi sielewi maana yake nini. Mwenye daladala ambaye pato lake ni shilingi elfu ishirini ndio Mhe. Omar anasema anatoa kodi, anayekodishwa nyumba kwa *dollars* anaambiwa kimya. Mhe. Naibu Spika, hatuko *serious* na bila shaka makato hayo kama tungekuwa tayari tungeyapata. Mimi nasema tu kwamba lazima mkubali ushauri wetu, mkae na sisi tuwaelekeze mkikataa maana yake itakuwa hatukusudii kupandisha mapato kwa maslahi ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba niwaombe Wazanzibari wakati ndio huu Katiba mpya imekuja, tujipange kutetea maslahi yetu ya Zanzibar kila penye upenyo wa kujitoa katika kuonewa tujitoe, kila penye upenyo wa kujinasua tuendelee kujinasua ili Wazanzibari tupate maslahi. Juzi Mhe. Naibu Spika, nilikuwa Uganda na niko tayari kutoa CD ambayo Rais Mseven alisema alitwambia neno moja kubwa, wenzangu tuliokuwa shirika wapo hapa, alitwambia mkifika Zanzibar kawambieni Wazanzibari kuna smzee mmoja amesema kupata mafuta sio kitu muhimu mafuta hayo utauza wapi, biashara itafanyika wapi angalau kupata mafuta si kitu muhimu uhusiano wa kimataifa. Na mimi naomba wazanzibari wajue kwamba mafuta si kitu muhimu uhusiano wa mataita, tuwe na uwezo wa ndani na nje ya nchi kwa maslahi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia angalau kidogo bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Fedha anayeshughulikia masuala ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza nimpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Maendeleo kwa hotuba yake aliyotuandalia na aliyoiwasilisha vizuri ni bajeti ambayo iko wazi haina utata.

Mhe. Naibu Spika, pia niwapongeze wenzake wanaomsaidia Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na Naibu Katibu Mkuu na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, pamoja na wote Wakurugenzi kwa kuweza kufanikisha bajeti hii ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii kwa ujumla ni nzuri kwa sababu imeeleza mambo mengi na kama tunavyojua kwamba bajeti ni mpango wa mapato na matumizi ya serikali. Kwa hivyo imeeleza namna mapato yalivyoweza kupatikana katika kipindi kilichopita lakini pia na matarajio ya kipindi hiki tunachokwenda nacho. Tatizo Mhe. Naibu Spika, nilichokiona kwamba mapato yameweza kupatikana kutoka katika taasisi za ukusanyaji wa mapato kwa zaidi ya asilimia 90. Lakini mapato yetu inavyoonekana yamezidiwa na matumizi, matumizi yetu yamekuwa makubwa kuliko mapato yetu. Kwa hivyo hiyo ni *challenge* kwa Wizara ya Fedha pamoja na sisi kwa ujumla, kwa sababu jambo hili si la mtu mmoja ni jambo letu kuhakikisha tunapata mapato ya kutosha ili yaendane na matumizi. Na kwa hili Mhe. Naibu Spika, tutakuwa kila wakati tunalaumiana kila mmoja anasema hivi huyu anasema hivi, huyu anasema muungano mbaya sijui hivi na hivi, yote yanatokana na

hii keki ndogo tuliyokuwa nayo. Kwa hivyo yatazuka mambo mengi katika hili.

Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri jana kwenye semina mtoa mada mmoja Dr. Jidawi alitupa kitu moja muhimu sana, alitwambia nyinyi Wawakilishi mnapojadili bajeti basi achane na hizi blaa blaa za vitabu za maneno, nendeni kwenye *datas* ndipo mtapoona mambo yalimo. Kwa hivyo niwaombe tuwache hizi blaa blaa hizi sijui serikali tatu, sijui serikali mbili, huku tukijadili bajeti ya serikali, twende kwenye *datas* tujadili bajeti kwa ajili ya wananchi ili tuone kwamba tunakwenda vipi, badala ya kuingiza blaa blaa hizi ambazo Mhe. Waziri ametuchomekea hizi, lengo tutoke huku kwenye bajeti basi tuanze kujadili mambo sijui ya muungano na mambo gani ambayo kwa sasa hivi hayawezi kutusaidia. Mambo haya yana wakati wake ukifika tutayajadili lakini sasa tujadili bajeti ya serikali, tuone serikali ina mipango gani, itakusanyaje, itatumiaje mambo haya mengine yatakuja kwa wakati wake.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mapato, Mhe. Waziri ametueleza kwamba katika bajeti ya mwaka 2012/2013 serikali ilikusudia au ilikadiria kukusanya mapato ya ndani ya shilingi bilioni 294.13 ambayo mapato haya yangetegemewa kukusanya na taasisi zetu za kodi ikiwemo *ZRB* ambayo ilitarajiwa kukusanya bilioni 146, *TRA* bilioni 106.73 na mapato yale yaliyokuwa yakikusanywa na mawizara ambayo yanakusanywa na Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na *PAYE* ambayo ni bilioni 21.4 ni ya wafanyakazi wetu wa Serikali ya Zanzibar ambayo kodi yao inakwenda Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akatueleza kwamba kwa muda wa miezi 9 kuanzia Julai mpaka Machi, serikali ilikusudia kukusanya bilioni 224 lakini makusanyo halisi yaliyokusanywa ni bilioni 201.24 ambayo ni asilimia 90 ya makusanyo yenyewe. Hapa Mhe. Naibu Spika, utaona kwamba kuna kasoro ya karibu bilioni 23. Mhe. Naibu Spika, *TRA* imekusanya bilioni 79.51 ambayo ni asilimia 99 ya makadirio katika kipindi hicho cha miezi 9.

Mhe. Naibu Spika, kwanza tuwapongeze sana wenzetu hawa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* kwa kuweza kufikisha kiwango hiki ambacho kimekadiriwa kwa muda huu wamefanya kazi nzuri na tunastahiki kuwapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, mapato haya yanayokusanywa na wenzetu wa *TRA* ni mapato yanayotumika hapa petu Zanzibar na wala haendi Tanzania Bara kama watu wanavyofikiria. Bado kuna watu wana dhana kwamba mapato ya *TRA* yanayokusanywa eti yanakusanywa yanakwenda kutumika Tanzania

Bara si kweli. Mapato haya yanayokusanywa na wenzetu wa *TRA* ni mapato yanayotumika hapa hapa kwetu visiwani Zanzibar.

Na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wanatusaidia kwa sababu masuala yote ya uendeshaji katika taasisi hii ikiwemo mishahara na mambo mengine yanalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo hiyo ni *advantage* moja kubwa ambayo sisi Wazanzibari tunaipata kwamba wakusanyaji pamoja na huduma zao zote zinatoka Bara, lakini mapato yanayokusanywa kwa ajili ya nchi yetu hii ya Zanzibar, kwa hivyo hiyo ni faraja kubwa, tunawapongeza sana *TRA*.

Lakini taasisi nyengine Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato *ZRB* ambayo kwa kipindi hicho imekusanya bilioni 109.48 ambayo ni asilimia 85 ya makadirio. Mhe. Naibu Spika, wenzetu hawa wamejitahidi, wamejitahidi kukusanya tunatakiwa tuthamini juhudi yao. Lakini kwa nini hawakufikia lengo, sisi Mhe. Naibu Spika, tungetegemea wenzetu hawa wa *ZRB* basi wenzetu hawa wa ZRB basi wafikie lengo na Mhe. Waziri alitakiwa atueleze kwenye hotuba yake ni kwa nini *ZRB* haikufikia lengo. Tuna-*appreciate* juhudi yao lakini atueleze kwa nini hawakufikia lengo na kwa sababu watakapotueleza sababu zilizowafanya wasifikie lengo, basi kwa pamoja tunaweza kutafuta njia ambayo itasaidia katika bajeti hii inayokuja basi kasoro zile tuweze kusaidiana nazo ili tuweze kuiondosha. Kwa hivyo Mhe. Waziri alitakiwa atueleze sababu za wenzetu wa *ZRB* kutokufikia lengo na badala yake kufikia asilimia 85 ya makadirio.

Eneo jengine Mhe. Naibu Spika, ni eneo la mapato haya ya *PAYE* ambayo yalikuwa yawe shilingi bilioni 21.4 na hadi kufikia mwezi wa Machi wenzetu, hawa wamekusanya jumla ya shilingi bilioni 12.3 ambayo ni asilimia 78. Kwa hivyo na hapa napo palikuwa panahitaji sababu za msingi za kutokufikia malengo.

Lakini pia Mhe. Waziri ametueleza matarajio, katika *speech* yake hii ametueleza matarajio sasa ya mwaka mzima ambapo matarajio ni mazuri. Kwa sababu mapato yote mpaka kufikia mwezi wa Juni yanatarajiwa kufikia bilioni 258.3 ambayo ni asilimia 94, kiwango hiki ni kikubwa sana cha ukusanyaji. Lakini kwa mapato yasiyokuwa na kodi wanatarajia kufikia bilioni 11.33 ambayo sawa na asilimia 57, hapa sasa pana matatizo. Mhe. Waziri na hapo tumetegemea atueleze kwa nini wenzetu hawa mapato yanayotokana na mawizara wafikie asilimia hii ya makadirio ili tuone kama kuna tofauti au kuna sababu zinazowapelekea kushindwa kukusanya kwa kiwango kile kinachotakiwa.

Lakini *TRA* pia itaongeza mpaka kufikia Juni inategemea kukusanya kwa asilimia 99 *excellent* na *ZRB* inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 148.6 ambayo sawa na asilimia 86, bado *ZRB* kunahitaji maelezo ya kina juu ya jambo hili na hii inategemea kukusanya bilioni 21.4 ambayo sawa na asilimia 100. Kwa hivyo wenzetu hawa wanaotoa pesa kutoka Bara kutuletea hizi za wafanyakazi, kwa mujibu wa maelezo yaliyokuwepo humu basi watatimiza asilimia 100 mpaka kufikia mwezi wa Juni, kwa hivyo hakuna haja ya kupiga kelele juu ya kodi hii na kwa sababu pesa inayokusanywa ya *PAYE* inakusanywa pale mwisho mshahara unapotolewa.

Kwa hivyo sasa hivi hakuna haja ya kupiga kelele kwamba wenzetu watueleze pesa hizi za *PAYE* zikoje wakati matarajio ni kukusanya kwa asilimia 100 ya makadirio haya. Kwa hivyo sisi tuwashukuru sana wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wamekuwa waadilifu na wakweli juu ya jambo hili na kwa sababu kodi hii tumeanza kuikusanya mwaka huu. Sasa kama kodi hii imekusanywa mwaka huu na itaweza kufikia kwa asilimia 100 basi tunahitaji pongezi na wala tusiweze kulalamika juu ya kodi hii. Hizi ni pongezi kubwa wenzetu wamejitahidi na wamethamini maelezo yetu, wamethamini juhudi zetu na wameweza kutusaidia na kiwango hiki cha fedha zimetusaidia sana katika kutekeleza bajeti zetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameeleza hatua za kuimarisha mapato ambapo si jambo baya na kwa sababu jinsi mapato ni madogo basi ni vyema akatafuta mbinu mbadala. Mhe. Waziri ametueleza kwamba serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya sheria ya viwango vya kodi na ada mbali mbali ambavyo anategemea kwamba marekebisho hayo ya sheria ya viwango mbali mbali ambavyo humu katika hotuba yake amevitaja vitaweza kumsaidia katika kutekeleza bajeti ambapo inategemea jumla ya shilingi bilioni 16 basi zinaweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho ya kodi tumeyaona na kwa ujumla marekebisho haya yatamgusa mwananchi moja kwa moja, lakini mimi sioni tatizo kubwa kwa sababu mjenga nchi ni mwananchi mwenyewe. Ni bora tujenge wenyewe nchi kwa mapato yetu kuliko kutegemea wahisani kutoka nje. Kwa hivyo kama tutakuwa na mipango kama hii ya kujibana wenyewe kwa ajili ya maendeleo yetu mimi sijaona kama ni jambo baya ni jambo zuri isipokuwa kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba mapato haya yanatumika vizuri. Mapato haya tunayoyakusanya ndiyo wanayotegemea wananchi wetu kutengenezea barabara, kupata madawa, watoto wetu kupata huduma za skuli na maendeleo mengi mengi. Kwa hivyo mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kubuni mbinu hii ya kujaribu kuongeza kodi kidogo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, si jambo baya.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo muhimu ya kuyaangalia. Haitokuwa vizuri Mhe. Waziri kuendelea kuwakamua wananchi wetu si jambo zuri, kwa sababu ng'ombe ukimkamua sana maziwa mwishowe hutoka damu. Kwa hivyo wataalamu wako wa uchumi wakae na waumize vichwa kuona kwamba wanatafuta vianzio vyengine vya kodi visivyowaumiza wananchi na uwezekano wa jambo hilo upo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mapato yanayotokana na mahoteli bado hayajakusanywa vizuri, kumekuwa na ujanja mkubwa mno katika maeneo ya mahotelini. Mhe. Hija kasema hapa, huu ni mfano mmoja tu lakini bado mapato yanayotokana na mahoteli, mapato yanayotokana na utalii hayajakusanywa ipasavyo, na hata leo Mhe. Waziri nikitaka unipe takwimu juu ya mapato yanayotokana na utalii naamini utashindwa ni mapato yaliyokuwa hayaeleweki. Utalii huu wa *packages* hausaidii nchi, wenzetu waliokuwa wakiutumia utalii huu wameshaachana nao kabisa kwa sababu fedha za watalii zinabakia nje, sisi tunabakia kukusanya makundi ya watalii hapa yasiyokuwa na manufaa yoyote. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie utalii wa *packages* wenzetu wameshaachana nao kabisa ni kwa sababu hauwezi kuleta maendeleo katika nchi, tunayo mahoteli mengi tu, jana tumekwenda kulala hotelini kule tumeona mahoteli, kuna mahoteli ya *five star* chungu mzima, lakini mapato yanayotokana na utalii kwa kweli si mapato ya kuridhisha katika kuendeleza uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Mhe. Waziri nilitegemea nalo ulieleze humu kwenye kitabu chako juu ya mpango wa kuimarisha mapato ni eneo la utoaji wa *visa* katika uwanja wa ndege, hili Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikilisema sana kwamba mapato katika uwanja wa ndege yanavuja sana, utaratibu unaotumika wa kugonga *stamp* ya *visa* watu wote wanatushangaa, wageni wanatushangaa kwamba bado tunaendelea na kuwa na utaratibu ambao kwa kweli haisaidii kunyanyua mapato ya nchi, hili tulikuwa tukilisema lakini kwenye *speech* yako Mhe. Waziri hili sijui umelisahau au bado halijawekewa mikakati hatuelewi liko katika *position* gani pale pana mapato mengi sana ya nchi yanapotea ovyo na inatokana na ule utaratibu unaotumika wa kukusanya mapato.

Eneo jengine Mhe. Naibu Spika, ni eneo la namna ya ukusanyaji wa kodi yenyewe unaokusanywa na *ZRB*, bado tunaendelea kukusanya kodi katika vianzio mbali mbali vya kodi kwa njia zile zile tulizozizowea za makadirio, hatukusanyi mapato kutokana na ule uhalisia wa kodi, bado tunaendelea kuwa na kodi za kukisia jambo ambalo wenzetu wameshaachana nalo. Sasa nataka nimtake Mhe. Waziri katika hili atakapofanya majumuisho aje atueleze Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inakusanya mapato yale ya risiti badala haya ya kukisia, eneo hili linapoteza fedha nyingi. Leo mtu anakwenda

dukani kununua bidhaa vitu vikubwa tu ananunua friji, TV, hapewi risiti au mfanyabiashara anamuuliza je unataka risiti, ukitaka risiti utalipa kiwango hiki, hutaki risiti utalipa kiwango hiki mambo haya mpaka lini. Kwa hivyo maeneo ya aina hii ni lazima yasimamiwe vizuri na kuhakikisha mapato ya nchi yanapatikana.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni eneo la kutafuta vianzio vipya, suala la uvuvi wa bahari kuu halijapewa kipaumbele na Serikali, uvuvi wa bahari kuu unaweza ukasaidia sana nchi kuitoa hapa ilipo na kwenda katika eneo jengine. Mifano tunayo kama nchi kama Srilanka ambayo sasa hivi ni nchi ambayo imepiga hatua kubwa sana ya uchumi kutokana na kuitumia bahari iliyowazunguka, lakini sisi bado rasilimali yetu ya bahari hatujaitumia vizuri. Maeneo ya uwekezaji, Fumba na Micheweni, maeneo haya kama tutayaimarisha tukaweka vivutio. Mimi naamini kwamba maeneo haya yataweza kutusaidia kuongeza uchumi na kuongeza mapato ya nchi, lakini bado inaonekana katika maeneo haya hatuyapi kipa umbele.

Mhe. Naibu Spika, katika maeneo ambayo ameyapendekeza Mhe. Waziri katika marekebisho ya sheria yake, maeneo hasa yanayowahusu wawekezaji, misamaha ya kodi yanahitaji kuangaliwa kwa umakini, kwa sababu yanaweza yakaleta athari kubwa, yeye Mhe. Waziri wa Fedha ni shahidi pamoja na Makamo wa Pili wa Rais ni shahidi tulipofanya ziara nchini Marekani, tukakutana na mama anayehusika na masuala ya uwekezaji wa nchini Marekani, jambo moja ambalo ametuuliza moja kubwa kwamba je nchi yenu imetoa nafuu gani kwa wawekezaji kwa wale wanaohitaji kuja kuwekeza *incentives* gani wametoa. Kwa sababu wawekezaji mara nyingi huwa wanaangalia katika maeneo mbali mbali na mara nyingi wanaelekea katika yale maeneo ambayo wao kwa hatua ya kwanza watapata nafuu. Kwa hivyo eneo hili linahitaji kuangaliwa tunaweza tukaongeza mapato lakini tukaweza kuwafukuza wawekezaji. Mimi Mhe. Naibu Spika, nimefikiria zaidi juu ya ukweli wa misamaha hii hapo ndipo penye tatizo, juu ya ukweli wa hawa wawekezaji wanaopewa hizi *grace period* ambazo tunazizungumza, kama tunaweza tukasimamia uzuri sheria ziliopo na zikafuatwa vizuri mimi nadhani kutakuwa hakuna matatizo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuna wawekezaji wana muda mrefu wamepewa ardhi lakini hawajapewa vibali vya uwekezaji, kuna mwekezaji mmoja amepewa ardhi anayo zaidi ya miaka 5 lakini anasubiri kibali kutoka *ZIPA* alikuwa kila wakati anaomba *grace period* anaongezwa muda unakwenda hajaanza kuwekeza hajaanza ujenzi anatusubiri. Kwa hivyo mambo mengine utayakuta ni matatizo si yetu sisi wenyewe hatuko *serious* katika hili, hatuko *serious* katika kusimamia masuala ya uwekezaji, mwekezaji anakuwa anakwenda anarudi kumekuwa na urasimu mkubwa juu ya masuala ya

uwekezaji. Linaloshangaza Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukienda sana kujifunza katika maeneo mbali mbali ya uwekezaji, wenzetu waliofanikiwa katika eneo hili la uwekezaji tulikuwa tukienda tukirudi, kumbe tunakwenda tukitembea tukirudi bure.

Mhe. Naibu Spika, tulipokwenda China ambapo wamepiga hatua kubwa sana ya uwekezaji, wenzetu wametueleza kwamba muekezaji anakuja kuomba siku moja anajibiwa siku ile ile, hakufanikiwa au amefanikiwa, siku moja tu anaomba anajibiwa lakini leo mwekezaji anakaa zaidi ya miaka 5 ana pesa zake anataka kuziekeza zaidi ya dola milioni 15, anataka kuwekeza hapa kwetu anataka kujenga hoteli miaka 5 anakwenda akirudi, hayo ni maeneo ambayo yatatusaidia sana katika ajira na masuala mengine, maeneo kama ya viwanda yanahitaji kupewa kipaumbele. Kwa hivyo Mhe. Waziri nadhani kuna haja ya kukaa na kutafakari na timu yako ya wataalamu kuona namna ya kuimarisha vianzio vipya badala ya kuendelea kuwakamua wananchi juu ya kutaka kuongeza mapato ya kuendesha nchi.

Mhe.Naibu Spika, la mwisho nisikumalizie muda wako ni haya maeneo ya vipa umbele. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa ametuonesha namna ya vipa umbele akatuambia vipa umbele vya mwaka huu ndio vile vile vipa umbele vya mwaka uliopita, ametaja maeneo ya sekta ya afya, elimu, ajira kwa vijana, kwa hivyo ametuambia kwamba maeneo haya yataendelea kwa muda mrefu kuwa ni vipa umbele katika bajeti zijazo.

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu huu tunaokwenda nao maeneo haya yataendelea kuwa vipa umbele milele na hayatofikia lengo, na kwa sababu kwanza hakuna vipaumbele vitatu vinne hamna kipa umbele kinakuwa kimoja, unapozungumzia kipa umbele, maana yake unakusudia kimoja lakini ukiona mtu anaweka vipa umbele vitatu, vinne, vinane hapo hakuna *improvement* yoyote na kweli ninakubaliana nae kuwa vitakuwa vipa umbele vya kudumu.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti iliyopita huku ambao tunaambiwa ni vipa umbele nimeangalia mchango wa Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo Wizara ya Afya ambapo ni kipa umbele moja kati ya kipa umbele, jumla ya shilingi bilioni mbili nukta saba zilitengwa ni kipa umbele hicho, lakini mpaka kufikia March fedha iliyopatikana milioni mia saba na ishirini ambayo ni asilimia ishirini na saba ya bajeti kipa umbele hicho.

Wizara ya Kazi, Uendeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika walitengewa fedha za maendeleo bilioni moja nukta moja nne sifuri, mpaka kufikia Machi pesa zilizopatikana ni milioni mia tatu na hamsini na nne ni asilimia thalathini na moja, kipaumbele hicho, huu ni mfano tu. Sasa tunaposema kipaumbele

tunakusudia nini kama tunakusudia ajira kwa vijana tulianzisha mradi kwa ajili ya Wizara ya Uwezeshaji tuwawezeshe vijana pamoja na kwamba ni kiwango kidogo hakiwezi kukidhi mahitaji ya vijana basi atleast hiki kiwango kipatikane, lakini leo unatoa asilimia thalathini na moja ya makadirio halafu unasema kipaumbele, Wizara ya Afya tunasema kipaumbele tunawapa pesa asilimia ishirini na saba halafu tunasema kipaumbele. Kwa hivyo mimi nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri kwamba vipaumbele hivi vitakuwa vya kudumu na havitamalizika kwa sababu hatuviingizii fedha, laiti kama ingelikuwa tunajua kwamba hivi ni vipaumbele basi bajeti yetu ingewapa *priority* tukajua kwamba hivi ni vipaumbele tuviwezeshe kupata pesa ili vimalize matatizo waliyokuwa nayo ili baadae tuweze kutafuta vipaumbele vyengine.

Mhe. Naibu Spika, muda wangu wa dakika thalathini umemalizika, kwa hivyo mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaiounga mkono sana bajeti hii na muda nilioutumia wote lakini katika eneo la matumizi kwamba wenzetu Serikali waangalie sana maeneo ya matumizi, kiwango cha fedha kilichokuwanacho kidogo lakini matumizi yetu yanaonekana yana ubabaishaji mwingi, fedha nyingi zinaliwa na wajanja hazitumiki kwa malengo yale yaliyokuwa yamekusudiwa. Kwa hivyo eneo hili Mhe. Waziri tuliangalia bado inaonekana kuna wafanyakazi hewa, bado kuna ujanja ambao unatumika kwa fedha zetu kidogo hizi tulizokuwa nazo hazitumii kwa uadilifu ujanja umekuwa mwingi na inapogundulika hakuna hatua zinazochukuliwa, hivyo niiombe Serikali kwamba pale ambapo ule ujanja utagundulika wizi au ubadhirifu unagundulika basi Serikali ichukue hatua kwa sababu fedha zetu hizi kidogo tunazozipata tukizitumia vizuri kwa uadilifu na uaminifu basi mabadiliko yataonekana na maendeleo yatapatikana inshallah. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi nikachangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba waja wake na kutufikisha hapa tukiwa na afya njema. Pia nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Maendeleo pamoja na watendaji wake kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake hii kwa umakini na umahiri mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze na ukurasa wa 10, aya ya 9 kifungu cha pili kinachoonesha kushuka kwa sekta ya kilimo katika uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili linatakiwa liangaliwe kwa mazingatio makubwa, ningeshauri Serikali kuandaa utaratibu maalum wa kusarifu mazao ya kilimo kwani ni muhimu sana kusarifu mazao ya kilimo na ni jambo ambalo linaweza kuongeza thamani ya mazao haraka. Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe mfano ndani ya jimbo langu la Ole pamoja na majimbo jirani ni maarufu sana kwa uzalishaji wa zao la embe. Mhe. Naibu Spika, lakini kwa bahati mbaya sana hazionekani juhudi za Serikali katika kusarifu zao hili angalau wale watu au wananchi wanaoishi ndani ya majimbo haya wakapata faida kubwa katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Zanzibar wanafika wakati au kikawaida wananunua *juice* ya embe kutoka nje ambapo kuwa hizo sehemu nyengine wanazonunua hakuna hata muembe mmoja sisi tuliokuwa na miembe mingi kuna maembe tani kwa tani zinazaliwa, zinapukutika na zinaoza au kuuzwa kwa bei ya kutupwa kabisa inasikitisha kweli Mhe. Naibu Spika, sasa ninaiomba Serikali katika hili iandae utaratibu mzuri angalau kuwawekea watu hawa kiwanda au wananchi wao hawa kuwawekea kiwanda kwa ajili ya kusarifu mazao haya ili kupunguza ule umasikini uliomo ndani ya maeneo yetu. Katika hili Serikali itakapoamua kutayarisha kijiwanda angalau kimoja kusarifu mazao haya basi nahakikisha kuwa vijana wetu wengi watapata ajira na lile suala la manung'uniko la kila siku vijana wanakosa ajira litapungua.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niulize suala hapa kwa sababu hatuwezi kusarifu hili zao la biashara la kilimo angalau watu wakapata faida, je vipi pato la wananchi wa Ole na majimbo ya jirani linaweza kukua wakati mazao haya husarifiwa wakapata angalau mazao yao kuuza kwa thamani, Mhe. Waziri naomba utakapokuja hapa unisaidie maelezo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, nataka niingie katika ukurasa wa 11 aya ya 16, bajeti imetaja kwamba mfumko wa bei umeshuka kuliko wa mwaka uliopita yaani mwaka jana. Katika hili wananchi walio wengi naona watashindwa kuielewa hii lugha ya kushuka huu mfumko wa bei.

Hivi kweli mfumko huu wa bei umekuwa na nafuu gani kwa bei za bidhaa za madukani, mfano katika kikao cha bajeti cha mwaka jana lita moja ya mafuta ya petroli ilikuwa kiasi gani na kikao hiki ni kiasi gani. Sasa Mhe. Naibu Spika, katika lugha hiyo kwamba bei imeshuka utawezaje kupunguza bei ya mafuta na kwa hivyo kupunguza bei ya usafiri na usafirishaji na uchukuzi ili wananchi wetu wakapata unafuu, kwa sababu ukisema kwamba mfumko wa bei umepungua lakini ukitizama bei za mafuta zinapanda, bei ya mafuta inapopanda na bei za magari watu wakisafiri na bei zinapanda, sasa wananchi wetu wa hali za chini ndio wanaoumia zaidi. Mhe. Naibu Spika, katika hili kwa nini mkulima wa Zanzibar na maeneo mengine akapata dhiki kubwa na

hapa panaonekana kama kuna mfumko wa bei umepungua, hili halioneshi usahihi wa kupungua bei.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 26 aya ya 38 kifungu kidogo cha 9 Mhe. Waziri amezungumzia matarajio ya ukuaji wa uchumi mwaka 2013/14 kuimarisha uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini. Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze sana Serikali katika eneo hili kwani kwa Zanzibar hapa ndipo kwenye mapato yetu makubwa. Sasa Mhe. Naibu Spika, suala langu liko hapa Serikali imejiandaa vipi na uvuvi wa bahari kuu, kuna maombi mangapi yaliyopitishwa yanayotaka kuekezwa kwenye eneo hili muhimu ili wananchi wetu tuone Serikali kweli imekusudia kuwekeza katika bahari hii kuu. Jengine katika ufugaji wa mazao ya baharini kuna fedha kiasi gani zilizowekezwa kwenye miundo mbinu ya ufugaji wa mazao ya baharini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la unafuu wa kodi ni jambo zuri na naipongeza sana Serikali kwa hatua hii, ila naomba kujua hatua hii ya unafuu wa kodi itakuwa na faida kwa nani kwa mlaji wa kawaida, kwa mfanyabiashara, sasa suala hili linatakiwa liangaliwe kwa umakini sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye suala jengine la muelekeo ya maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2012/13 Serikali imetoa kipaumbele katika maeneo muhimu ikiwemo kustawisha ustawi wa wazee, kuimarisha uchumi, sekta ya afya. Haya maeneo ni muhimu sana na ukiyaangalia katika kitabu utaona haya mambo tayari yameshakamilika lakini Mhe. Naibu Spika, kweli kuna changamoto nyingi katika kuekeza haya. Alizungumza sana Mhe. Salmin hapa kuhusu kipaumbele katika sekta ya afya ni muhimu kwa binadamu na sisi sote humu ndani ni mashahidi tukitizama tunaimarisha tu majengo mengi, vituo vingi vya afya tunavyo lakini matokeo yake hakuna watendaji, hakuna madaktari, hamna madawa hamna chochote, sasa hicho kipaumbele sijui kitakujaje. La kusikitisha zaidi Mhe. Naibu Spika, wewe utakapokwenda humo kwenye vituo ukifika hiyo hali utakayoiona ni ya kusikitisha, kitanda kimoja kinalala wagonjwa watatu na hilo silisemi kwa sababu ya kuambiwa na mtu, nimelishuhudia mimi mwenyewe wako wagonjwa watatu kila mmoja ana maradhi yake, leo wanalala katika kitanda kimoja, je hili ni kumfanyia mtu matitabu au ni kumuongeza maradhi mengine.

Mhe. Naibu Spika, halafu katika eneo hilo hilo la afya utakuta maeneo ya afya katika hospitali hasa hospitali yetu ya Mnazimmoja ambayo kuwa ni hospitali yetu kubwa tunayoitegemea watu wengi, Wazanzibari wengi tunaitegemea hospitali ile. Leo Hospitali ile ya Mnazimmoja kuna matatizo makubwa Mhe. Naibu Spika, hasa katika sehemu ya vyoo, afya ni muhimu kwa binadamu, vyoo vyetu haviridhishi, baada ya kutibu watu wataondoka pale na maradhi

mengine. Kwa hivyo katika kutoa kipaumbele cha afya Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri au naiomba Serikali kwa ujumla ilitizame sana suala la afya ya mwanadamu ukizingatia watu wengi wanatoka pale wanakimbilia hospitali zetu za Serikali ambapo hawana uwezo wa kwenda hospitali za *private*, sasa zile hospitali angalau ziboreshwe zionekane zina madawa, zionekane zina usafi wa kuridhisha. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Awali ya yote nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuja tukiwa wazima na afya njema. Vile vile nakuchukua fursa hii kwanza kuwapongeza wananchi wa Chambani kwa kufanya uchaguzi ulio na utulivu na amani, lakini vile vile nachukua fursa hii kukipongeza Chama cha CUF kwa kupata ushindi wa Jimbo la Chambani. Lakini vile vile nachukua fursa hii adhimu kuwapongeza wanachama wa CCM wa Jimbo la Chambani kwa kukipigia Chama cha CCM na Chama cha CCM kinajua ushindi ni wao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa sina mengi ya kusema kwa sababu mengi yameshazungumzwa na walionitangulia, kwa hivyo hayo machache ambayo nitayazungumza yatakuwa zaidi nafikiria kwamba ni ya kutia msisitizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii. Nampongeza kwa sababu hotuba yake imeweza kubeba yale yote ambayo yalikuwa na malengo ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Zanzibar. Tunazungumzia masuala ya MKUZA, tunazungumzia masuala ya MBG, tunazungumzia na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, kwa hilo kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wizara hii kwa sababu kwa kweli wamepiga hatua kubwa sana hata katika kipindi ambacho tunakimaliza.

Mhe. Naibu Spika, naanza na ukurasa wa 20 katika kitabu chetu ambacho kinazungumzia suala zima la utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele. Katika mwaka 2013 kipaumbele kilikuwa katika masuala mazima ya kuimarisha huduma za afya, kuimarisha ajira za vijana, kuimarisha ustawi wa wazee, kuimarisha elimu ya lazima, kuimarisha uchumi na kuimarisha mashirikiano ya sekta binafsi na umma.

Mhe. Naibu Spika, napenda kusema kwamba kutokana na taarifa ambazo tumezipata na ambazo zimetueleza namna gani utekelezaji wa hivi vipaumbele, mimi naweza kusema kwamba tumepiga hatua inayoridhisha.

Nasema hivyo kwa sababu sote tunafahamu namna ya mapato ambayo tunayapata katika maeneo mbali mbali, tunaona kuwa kwa kweli taasisi ambazo zinashughulikia masuala ya ukusanyaji wa mapato kama *ZRB*, *TRA* pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kweli kazi wanaifanya vizuri na wanastahiki kupongezwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nina wasi wasi mkubwa kiasi ambacho mapato haya yanavyokusanywa. Hofu yangu zaidi ni kwamba ninahisi bado taasisi hizi hazijapata ushirikiano mzuri kuanzia kwa wananchi mpaka kufikia katika taasisi ambazo zinaleta mapato haya. Huo ni wasi wasi wangu mkubwa, lakini wasi wasi wangu mwengine mkubwa ulikuwa ni wa kuangalia sheria ambazo tunazo na ambazo zinatupa njia ya kuweza kukusanya mapato hayo. Sasa nimeshukuru na nimeshukuru sana kwa sababu nimeona kwamba wizara imejikita katika kuzipitia upya sheria ambazo zitaweza kusaidia katika kukusanya mapato. Nashukuru na naipongeza sana wizara kwa mpango huo.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, ningependa kusema kuwa tunataka kuimarisha elimu. Kuimarisha elimu si jambo la siri sote tunafahamu kwamba kiwango cha elimu yetu kimeteremka kwa kiasi kikubwa na sababu zipo nyingi sana, huwezi kunyooshea sababu ya kitu kimoja, ziko sababu nyingi ikiwemo uhaba wa walimu, hali na mazingira ya skuli ambazo tunazo. Vile vile ukiwemo na utamaduni ambao sasa hatunao tena wa kujisomea. Hivyo ni vitu ambavyo vinasababisha lakini tunashukuru serikali yetu kwa kweli inajitahidi sana kwa hilo kwa sababu ajira za walimu mwaka jana zimeonekana nyingi zimetekelezwa, lakini vile vile kuna mpango wa kujenga maktaba na pia kuna mipango mengine ambayo inahakikisha kwamba basi wanafunzi katika vijiji mbali mbali wanapata vitabu vya kujisomea.

Mhe. Naibu Spika, katika mpango ambao kwa mwaka 2013/14 pia kuna bajeti maalum ambayo itasaidia katika kuhakikisha kwamba kwenye skuli zetu basi kutakuwa na vitabu pamoja na viti. Tuombe Mwenyezi Mungu kwamba kufikia mwisho wa mwaka 2014 basi skuli zote za Unguja na Pemba wameweza kupata vitabu pamoja na viti.

Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba vijana wetu wana matatizo ya ajira, kwa nini kuna tatizo la ajira? Kwa sababu vile vile ya ushukaji wa elimu yetu, nasema bado hatujaweza juu ya kwamba jitihada zinafanyika lakini bado hatujaweza kujipanga vizuri kwa kuweza kutoa elimu ambayo itakuwa na mwelekeo wa kiuchumi. Vijana wetu wengi wanapata elimu ambayo inawaandaa waweze kuwa na elimu nyengine ya juu ambayo ni kuwa madaktari na kuwa mainjinia. Lakini hawa ambao wanamaliza vidato, mtoto

anamaliza darasa la kumi kwa kweli anakuwa hana chochote cha kufanya kwa sababu ya msingi wa elimu ambao ameondokana nao kutoka chini.

Kwa hivyo, hiyo ni sababu na nataka kusisitiza kwamba iko haja sasa hivi ya kuhakikisha kuwa ubora wa elimu kuanzia skuli ya maandalizi mpaka kufikia sekondari ipo haja kubwa ya kutizama upya mitaala yetu na kuhakikisha elimu inayopatikana itakwenda na mazingira yetu. Tusijali kwamba mitaala sio lazima sasa hivi wataalamu wanasema, mitaala sio lazima iwe mitaala ya jumla kwa sababu vijana wetu wengi wanaishi katika mazingira mbali mbali, kuna ambao wanaishi katika mazingira ya pwani, kuna wanaoishi katika mazingira ya kilimo lakini pia kuna ambao wanaishi mjini. Sasa elimu ambayo itaweza kuwafaa hawa ni elimu ambayo itaweza kuwasaidia katika mazingira yao wanayoishi na itasaidia sana.

Leo Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia Mkoa wa Mjini/Magharibi na hasa kwamba kuna idadi kubwa ya watu wanaokwenda kuishi pale, lakini wengi wanakuwa kule kwa ajili ya kutafuta ajira wanahama katika maeneo yao. Kwa nini wanahama katika maeneo? Kwa sababu kule hakuna kazi ya kufanya sasa wanakimbilia huku ili angalau waweze kupata ajira ndogo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nitaingia katika ukurasa wa 22. Mhe. Naibu Spika, hotuba hii imenifurahisha kuwa imelitia suala zima la Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa wengi wamezungumzia suala hilo na ni kweli, alisema hapa Mhe. Mansoor kwamba kila mtu ana haki ya kuzungumza anachokifikiria na anachoona kwamba hiki kitaleta manufaa kwa Zanzibar. Huo ni ukweli ambao hauwezi kupingika kwa sababu tumeshapewa tayari nafasi hiyo kufanya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kitu kimoja ambacho tunasahau na ninakisema hiki kwa sababu nataka kila mmoja atambue, tunapoizungumzia Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunasahau kwamba kuna mengine zaidi ya Muungano. Rasimu ile haijazungumzia tu Muungano ndio pale tunapoambiwa kwamba tunazungumza kwa utashi sio Muungano tu, ime-*compile* mambo chungunzima na haya madogo madogo tuyazungumzie. Sisi wanawake tunataka usawa wa kijinsia, tunataka tujihisi kwamba sisi ni raia ambao tunapewa haki zetu na usawa wetu hilo hakuna mtu ambaye analizungumzia kwa nini? Tutalizungumza sisi, hatuwezi kuwa na serikali itakayokwenda sawa bila ya kuwa na watu walio sawa watu ambao wanapata haki sawa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kuna mambao mengi, nazungumzia masuala ya sheria za ardhi kwenye rasimu ipo, tunazungumzia masuala ambayo yanawahusu watoto yamo, sio *issue* moja tu. Mimi nilisikiliza na nimesikia

hotuba ambayo ameitoa Mhe. Jaji Warioba kazungumzia mambo mengi lakini kwa bahati mbaya kwa sisi Zanzibar sana tunazungumzia Muungano sawa tuzungumze na ni kweli kuna mambo ambayo yanataka kurekebishwa, ni sawa kabisa hakuna anayekataa hili, lakini na hivi vionjo vidogo vidogo vyengine tusije tukavisahau kwa sababu tukijiweka katika kulitizama suala moja tu mengine tutayasahau. Mimi nawahusia sana wanawake wenzangu na akinababa iko haja ya kuangalia usawa wa kijinsia katika Katiba hii, ina umuhimu wake kwa sababu na wanawake wako asilimia kubwa zaidi kuliko wanaume, wanawake wengi ni wakulima yote hayo tuyazungumza jamani tusije tukayasahau.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nizungumzie suala zima la maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi. Kwanza mimi nichukue fursa hii uniruhusu Mhe. Naibu Spika, kuwaombea dua waasisi wa Mapinduzi yetu, Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, awasamehe makosa yao, Mwenyezi Mungu awajaalie walale pahala pema peponi. Nasema hivyo kwa sababu, mimi najifikiria mwenyewe kama Mgeni leo ingekuwa sio Mapinduzi haya ya Zanzibar pengine nisingeweza kufika hapa na kusema haya, tumepata *freedom* ya *speech* kila mtu hapa tumetoka katika mazingira mbali mbali, lakini kila mtu kapewa uwezo leo baada ya Mapinduzi haya matukufu ya Zanzibar kuweza kusimama na kuzungumza na wananchi pia wana haki ya kutoa maoni yao tunataka nini zaidi ya Mapinduzi yetu, leo tunabeza kwa nini tubeze Mapinduzi yetu.

Kuna watu Mhe. Naibu Spika, wanabeza kuwa hakuna maendeleo, hakuna hili tutizame walikuwa wangapi waliosoma na leo wako wangapi, tutizame tulikuwa na vituo vya afya vingapi na leo viko vingapi, tutizame tulikuwa na barabara ngapi na leo tunazo ngapi. Waheshimiwa wenzangu tukosoe lakini tujue tumetoka wapi na tunakwenda wapi, tulichokipata hatuwezi kukijejea na hatuwezi kukibadilisha na kitu chochote. Yadumu Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika ukurasa wa 28 ambao unazungumzia maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2013/14. Mhe. Naibu Spika, hapa yamezungumziwa yale yale ambayo yalikuwa ni vipaumbele vya mwaka 2012/13. Mimi naipongeza sana wizara na najua kuna baadhi ya miradi haijakamilika tumeona katika wizara mbali mbali na kutokana na hali yetu ya kifedha. Lakini Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kidogo kuhusu suala zima la miradi ya maendeleo ambayo tunafadhiliwa na wafadhili mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hali inayoelekea sasa hivi na inayoonekana ile *trend* ya kupata fedha zile kutoka wafadhili inaanza kuwa mbaya, wenzetu wanaanza kutuacha mkono, ina maana iko haja tunapozungumzia kwamba tunataka

kuvipa vitu vipaumbele kama afya au elimu lazima tuanze kujipanga tuhakikishe kwamba mapato yetu yenyewe ya ndani yataweza kutosheleza katika kuendeleza mambo haya ambayo tunataka kuyapa kipaumbele. Inasikitisha sana kwamba wenzetu wanatuacha mkono lakini inasikitisha zaidi kwa kweli bado hatujaweza kupata kile kipato ambacho tunakuwa mara nyingi tunakitarajia.

Mhe. Naibu Spika, mimi huwa najiuliza siku zote kuna tatizo gani? Lakini vile vile ninahisi kwamba kwanza miundombinu ya kutafutia hayo mapato, tatizo ni kubwa wenzetu wako mbele sana wana njia ambazo zinasaidia sana mara moja katika kuweza kujua bidhaa yoyote ambayo inaingia nchini na vipi kodi itapatikana kutokana na bidhaa ile. Kama walivyotangulia wenzangu kusema unaweza ukenda dukani ukaambiwa kama unataka risiti au hutaki, kama hutaki utapunguziwa bei na kama unataka bei inakuwa kubwa. Sasa hivi ndivyo wanavyofanya wafanyabiashara ili kukimbia kodi na akikimbia kodi ina maana taifa linakosa mapato anasahau kwamba mapato yale ndio yanayosaidia kujenga barabara, skuli na dawa za hospitali. Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba bado wafanyabiashara wetu wa ndani hawajakuwa na taaluma ya kwa nini kodi inakusanywa. Sasa nimuombe Mhe. Waziri wafanyabiashara wahamasishwe kwa kila hali kuhakikisha kwamba kodi wanalipa ipasavyo.

Vile vile kuna suala zima la mambo mengine la kutafuta vyanzo vya mapato. Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyingi nikitembea njiani natizama majumba yalioko huku Chukwani, hilo niliwahi kumwambia waziri nikamwambia hivi hawa watu wenye majumba makubwa wanalipa kodi, kuna majumba mengine yamekaa tu hata watu hawaishi, lakini wale wanalazimika kulipa kama *council tax*. Mhe. Waziri akanijibu tuko katika mpango huu wa kusajili nyumba zile, mimi sizungumzii nyumba za maskini wenzangu huko ng'ambo hapana, wale waachiwe kama walivyo lakini wenye kipato, kwa sababu nchi nyingi duniani wanakusanya kodi kutoka kwa watu wenye kipato na hiyo ndio inasaidia kuweza kuweka ustawi wa wananchi walio maskini. Wananchi walio maskini wataishi maisha bora ikiwa serikali itaweza kukusanya mapato kutoka kwa wale wenye uwezo.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri kutaka kujua haya majengo yetu hata haya ya serikali yanalipa kodi, kuna umuhimu mkubwa na mimi naamini kabisa itaweza kutuongezea vyanzo vya mapato, tukae tutizame tutafute mbinu lakini sio kuwaumiza wananchi wadogo hawa hawana haja tena ya kutoa kodi na kila kitu kodi. Mhe. Waziri nakuomba sana hilo ulitizame na mimi naamini kabisa ikiwa kutakuwa na mpango huo basi tutaweza kufanikiwa kwa upande huo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nimetaka kulizungumzia ni suala zima la programu ambazo zimetayarishwa kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi. Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 32 kumezungumziwa suala zima la Programu ya Mageuzi ya Serikali ambayo ni kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na utoaji huduma kwa matokeo kwa utendaji, na utoaji huduma wa serikali kwa kupima viashiria vya msingi vya utendaji, kupambana na rushwa na kujenga uwezo.

Mhe. Naibu Spika, tuna tatizo kubwa, mipango tunayotaka ni mizuri tuna wataalamu wazuri, wasomi wazuri ambao wanatupangia mipango mizuri lakini hapa kati katika utendaji pana matatizo. Serikali imekuwa ikitoa mafunzo mbali mbali kuhakikisha kwamba watendaji wao wanakuwa na ufanisi mzuri wa kazi zao, lakini mimi mara nyingi nimekuwa nauliza kuna kipimo gani kinachotuonesha kwamba hawa watendaji kweli wanafanya kazi kama wanavyotakiwa kuzifanya, huwa ninajiuliza mara nyingi sana. Je, tuna mpango gani ambao tunakaa tunawa-*access*, amepata *train* lakini akirudi huku nyuma je kafanya nini. Mhe. Waziri hii ni changamoto kubwa wengine wanakwenda *trains* bure wakirudi hawana wanachokifanya huduma zinaongezeka zinakuwa bora lakini sio kwa kasi ambayo tunaitaka.

Mhe. Rais alitwambia tubadilike anataka wananchi wake wabadilike na sio wabadilike viongozi wa juu tu, lakini wabadilike mpaka wale watendaji ambao wanatoa huduma kwa wananchi bado huduma haziridhishi. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana hivi viashiria vya kupima huduma zinazotolewa vituletee kitu ambacho kimepatikana katika hiyo mipango ambayo imepangwa. Lakini vile vile suala zima la rushwa.

Mhe. Naibu Spika, hili nitakuja kulizungumza zaidi katika Wizara ya Nchi (OR) Katiba na Utawala Bora suala la rushwa linaturejesha nyuma na matumizi mabaya ya fedha za serikali, linarudisha nyuma serikali yetu, linarudisha sana na si rahisi kuweza kuendelea kupiga hatua kama hivi vitu viwili vitakuwa vimetuganda ndani ya mifuko yetu. Kuna watu bado hawajaweza kubadilika wanaendelea na mfumo ule ule wa *business as usually* na mtu anakuwa mkali akiulizwa halafu vitu vyengine havitaki tochi.

Mhe. Naibu Spika, mtu anafanya kazi sehemu fulani unamuona ana nyumba nne, tano au sita una hakika yule mtu hana biashara nyengine, jamani tujipange, ni kweli wananchi wanalalamika kwa sababu wanaona na wanamuona mtu kenda kufanya kazi pahala fulani baada ya miezi miwili mtu huyo ana uwezo pengine kuna aliyefanya kazi miaka 50 hana, lazima tuwaonee huruma wale wananchi wa chini watu wanafanya kazi miaka 30 mpaka 40, walimo wanasomesha, wafanyakazi wa afya wanafanya kazi lakini wanapata kipato kidogo akimaliza *incentive* ndogo yule akienda akiomba haki

yake inachukua miaka ndio apewe kwa sababu watu wanachukua pesa wanazitia mfukoni. Mtu akitaka kupata huduma anaambiwa lazima.

Mhe. Rais alitoa unafuu wa vifaa alisema vifaa vya kuzalia kwa wanawake viwe bure, kuna watu wanalalamika bado wanatoa pesa wanavilipia. Tumekwenda sisi Pemba tumesikia hayo watu wanatoa pesa sasa hiyo ni rushwa na mtu itabidi atoe kwa sababu rushwa tunaambiwa anayetoa na anayepewa lakini mzazi umekwenda naye ana uchungu asitoe na kishaambiwa toa pesa atatoa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili nimelitaja hapa lakini ni suala ambalo kwa kweli ni mtambuka na suala hili lazima tulifanyie kazi, matumizi mabaya ya fedha za serikali ikiwemo pia na vitu vya serikali kama magari yanatumika vibaya. Lakini vile vile watu wanajisahau wanajilimbikizia wao tu, kila siku watu wako safarini, leo hapa kesho kule watu wanajilimbikizia wao tujaribu kujipanga ili na wananchi wetu huku wafaidike. Juzi kuna mwananchi ananiambia sisi tumeshachoka nyinyi mnapiga kelele za bure hakuna tofauti tunayoiona. Nikamwambia tofauti ipo, lakini inabidi tufanye kazi tufunge vibwebwe ili tuhakikisha kwamba hii nchi inaendelea na mapato yetu ndio yatatusaidia katika kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia suala jengine la mtambuka. Tuzingatie sana mabadiliko ya tabia nchi, maafa uhifadhi wa mazingira jinsia na watu wenye mahitaji maalum. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaipongeza sana wizara ikiwa hili wataliwekea mikakati maalum, nasema hivyo kwa sababu hali ya mazingira yetu imeshakuwa mbaya sana, miti inakatwa na tunaisikia siku zote kila unapopita wewe unasikia msumeno wa moto unataka unamaliza mti ukipita kwengine halikadhalika. Lakini jana mhadhiri wetu mmoja alisema kuwa huwezi kumwambia mtu asikate mti kwa sababu hujamuwekea mazingira ambayo yatamzuia yeye kukata mti, muwekee yale mazingira mwananchi asikate mti. Sasa hili linataka mipango mizuri.

Halafu suala jengine la jinsia ni kwamba sasa hivi umeshafika wakati tukubali tunao wataalamu wengi wanawake waonekane, wataalamu wenye uwezo, wanasiasa wenye uwezo waonekane na wapewe nafasi na wao waweze kutumikia taifa lao. Mhe. Naibu Spika, mwanamke anaonekana kama hafai au hawezi, hakuna asiyeweza, hakuna aliyezaliwa anaweza zikitokea nafasi basi apewe mmoja mwanamke na mmoja mwanamme sawa sawa, kwa sababu wanawake wanaweza, tuko wengi, kwa hivyo tunayo haki ya kupewa kwa sababu mpaka dini zote zimetupa usawa mwanamke na mwanamme ni sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa mimi nataka kuzungumzia suala la mtambuka lenye mahitaji maalum. Mhe. Naibu Spika, tunayo makundi

ambayo yana mahitaji maalum makundi yenye mahitaji maalum tuyape kipaumbele kwa kuwatengenezea miundombinu ambayo itasaidia katika mambo yao mbali mbali. Lakini bado tumekuwa tunafanya mambo ambayo hayaangalii umuhimu wa kuwapa hawa miundombinu ambayo itaweza kuwasaidia katika maisha yao, pamoja na kuwezesha kuwapa mikopo ambayo wataweza kufanya miradi na kuwawezesha kiuchumi. Mhe. Naibu Spika, nimeshakuona namalizia sasa hivi.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nitaomba nijibiwe yale ambayo nimeyauliza lakini naunga mkono hotuba ya waziri kwa asilimia mia moja kwa niaba ya akinamama wenzangu wote na kwa niaba ya Jumuiya yangu ya UWAWAZA ya Baraza la Wawakilishi. Nashukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Wanu Hafidh Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti. Lakini pia nitoe pongezi kwa bajeti yenyewe kwa ujumla niipongeze Serikali kwa hatua za kuimairisha mapato ambayo imekuja nayo. Lakini pia niishauri Serikali na hasa katika wakati huu ambapo msaada ambao wa wenzetu ambao wanatusaidia inashukashuka sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niipongeze Serikali kwa kuona kwamba mwaka huo ulikuwa na haja ya kuja na bajeti ambayo imechukua huduma ya jamii kwa wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanzia katika maeneo ambayo Serikali imeyameona ni maeneo ya kipaumbele. Kwanza nianzie na maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, maji safi na salama kama eneo ambalo limepewa kipaumbele limetengewa Shilingi 55.4 bilioni. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kusema hivi kwa kweli fedha hizi zote na Mhe. Ali amesema kwamba hawaoni kwamba hii mamlaka ambayo inashughulika na maji mamlaka ya *ZAWA* kwamba inafanya hiyo kazi ya kutoa huduma kwa wananchi ya maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika,nasema hivi kwa sababu mpaka hivi sasa miaka 50 ya Mapinduzi kesho kutwa tunatimiza bado wananachi wa mjini wanatumia maji ya chumvi na sio Mjini/Magharibi, hivi haya ndio yale maji safi na salama ambayo ndio tuliyowaahidi wananchi kuwapa. Mhe. Naibu Spika, sasa niseme kwamba Serikali inaposema kwamba kuna maeneo yanapewa kipaumbele basi kipaumbele hicho kipewe kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, eneo la pili ambalo nimesema nigusie ni ajira kwa vijana. Niishukuru Serikali kwa kuona kwamba tatizo la ajira kwa vijana limekuwa ni kubwa na wakaona kwamba iko haja ya tatizo hili kupewa kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, wataalamu wametwambia kwamba tathmini ya *HBF* ya Zanzibar *unemployment* yetu ni 4.4 na *youth unemployment* 17.1 *percent* wastani wa vijana laki moja hawana ajira.

Mhe. Niabu Spika, kwa kweli tatizo hili ni kubwa inawezekana likawa kubwa zaidi kuliko tathmini ilivyotoka. Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kupitia kitabu hiki cha pili ambacho kinaelezea muelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo kwa mwaka nimepitia programu na miradi tofauti ambayo itatoa ajira kwa vijana. Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha kwamba katika miradi hii yote ambayo Serikali imeona inatoa kipaumbele kwa vijana elfu moja mia moja na thamannin tu ambayo ndio watakaopata ajira katika programu hii ya mwaka 2013/2014, ukilinganisha na ile tathmini iliyotolewa na *HBF* ya Zanzibar, kati ya wale vijana laki moja ambao hawana ajira na elfu moja mia moja na thamanini ndio watafaidika na ajira ambazo hizi za miradi hii ya *program* 2013/2014. Hapa Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ile hoja ya Mhe. Salmin Awadh Salmin lile swali alilouliza kwamba hivi kweli tunavyosema kuna maeneo tunayapa kipaumbele na tunatenga pesa nyingi kwa maeneo hayo. Kweli tunakwenda kuwapa kipaumbele maeneo hayo.

Mhe.Naibu Spika,vile vile Serikali ijue kwamba tatizo la ajira kwa vijana ni tatizo endelevu na kama ni maradhi basi tumeyafuga yameshakuwa sugu na hayatibiki tena, kwa sababu kila tukiendelea mbele watoto wanafeli wanaingia katika soko la vijana wasio na ajira. Hapa niunganishe na ile *point* aliyosema Mhe. Mgeni Hassan Juma kwamba ipo haja sasa ya kuimairisha elimu na pengine pia niunge mkono hoja ya Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba hivi sasa ipo haja ya kutoa elimu za mafunzo zaidi za mafundi kuliko inavyotolewa sasa kwa sababu inaonekana watoto wanafeli na kila siku wanaingia katika soko hili la vijana wasio na ajira.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, nitoe wito kwa vijana hawa kwamba wawe na tabia ya kutokuchagua kazi. Lakini pia wanatwambia kwamba wajikusanye katika makundi na kupewa taaluma wafanye hivyo ili kuisaidia Serikali kutatua hili tatizo. Lakini pia wajitatue wao wenyewe katika ukali wa maisha.

Mhe. Niabu Spika, kwa kumalizia wataalamu wanasema usawa wa jinsia katika uchumi na maendeleo ni jambo muhimu sana na kila jinsia zina umuhimu katika kujenga uchumi ulio imara. Lakini la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba bado taarifa nyingi zinaonesha kwamba wanawake ndio wanaoathirika zaidi na umasikini.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naunga hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba ipo haja ya kuanzisha Benki ya Wanawake kama alivyotoa ushauri kwa Serikali itakayowainua wanawake kimaendeleo. Lakini vile vile swali hili tumekuwa tukimuomba Mhe. Waziri wa Fedha kila siku kwamba aone namna ya kuanzisha Benki ya Wanawake hapa Zanzibar. Lakini hata kama kuna ugumu kwa namna mmoja au nyengine katika kuanzisha Benki hii wenzetu Bara wanayo *at least* afanye mazungumzo ili wale ambao wanatoa huduma kwa wanawake wenze kule Bara waanzishe kwao hapa Zanzibar itatusaidia. Mimi nashangaa katika mambo ya kijamii tunashirikiana na kijinsia ile nyengine lakini katika mambo ya uchumi mnatuweka nyuma nyuma. Sasa kwa hiyo tumuombe Mhe. Waziri wa Fedha kama kuna ugumu wa kuanzisha Benki wa wanawake basi wale wenzetu wanaotoa huduma Bara waje hapa waanzishe matawi ili na sisi yatukwamue katika ukali wa maisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imetusaidia sana wanawake wamechoka kila siku kuanika mwani hauna soko, dagaa halitoki wanalima kilimo ndio hicho kinarudi nyuma. Kwa hiyo Mhe. Naubu Spika, tunaiomba Serikali itusaidie sana itukwamue katika hali ya ugumu wa maisha wanawake. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuruni kwa ushirikiano wenu mzuri mlionipa na kuwa watulivu katika kipindi hiki cha jioni. Tumebakisha wachangiaji 10 tukijaaliwa kesho tuje mapema kila alieleta jina tukimaliza maswali na majibu tuweze kuendelea na michango yetu.

Kwa muda uliobakia kumpa Mjumbe dakika tano ni mdogo kwa hivyo naakhirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 18/06/2013 saa 3:00 barabara asubuhi.

(*Saa 1.40 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/06/2013 saa 3:00 asubuhi)*